# MATUMIZI YA RASILIMALI ZA KISWAHILI ZA MTANDAO WA KIAKADEMIA NA WANAFUNZI WA KISWAHILI WA CHUO KIKUU CHA MASENO


**NA**

**KHAKASA MUKACHELELWA SCOLASTICA**


**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KAMA SEHEMU YA KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI**


**IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA**

**CHUO KIKUU CHA MASENO**



**©2016**

## Ikirari

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa kwa minajili ya shughuli yoyote ile wala kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote kile. Ni hatia kutoa au kurudufu nakala au sehemu ya tasnifu hii bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Maseno.

Sahihi ..........................................

Jina Khakasa Mukachelelwa Scolastica

Nambari ya usajili PG/MA/021/2009 Tarehe .................................

Tasnifu hii imewasilishwa kwa minajili ya kutahiniwa kwa ridhaa yetu tulioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Maseno kama wasimamizi

Sahihi ..................................

Jina Prof. Indede Florence
Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika
Chuo Kikuu cha Maseno

Tarehe ...................................

Sahihi .......................................

Jina Prof. Mohochi Ernest
Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi
Chuo Kishirikishi cha Rongo

Tarehe .....................................

## Shukrani

Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunisaidia katika kufanikisha kazi yangu. Shukrani kwa wasimamizi wangu Prof. Indede Florence na Prof. Mohochi Ernest kwa juhudi walizofanya kwa kusimamia na kusahihisha kazi hii hadi kufikia upeo, kwa kunipa moyo ulioniwezesha kuifanya kazi hii kwa subira kubwa. Aidha ningependa kushukuru Chuo Kikuu cha Maseno, hasa shule ya Sanaa na Sayansi Jamii na Idara ya Kiswahili na lugha Nyingine za Kiafrika kwa ushirikiano mzuri ulioniwezesha kufanikisha kazi hii. Mwisho nawashukuru wanafunzi wa Idara ya Kiswahili na lugha Nyingine za Kiafrika kwa kukubali kunipa maoni yao kuhusiana na matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia.

## Tabaruku

Kazi hii ninaitabaruku kwa mume wangu Daniel Buriah,watoto Caleb, Dorothy  na Wazazi Bw. na Bi. Mukachelelwa.

## Ikisiri

Mtandao una rasilimali nyingi za kiakademia ambazo zina umuhimu kwa wanafunzi wa vyuo vikuu na utafiti kwani wanaweza kufanya tafiti zao mbalimbali kutegemea kozi. Tafiti zimechunguza matumizi ya mtandao miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu na inabainika wazi kuwa, wengi wao wanautumia mtandao sana kwa maswala ya burudani na si kiakademia. Baadhi ya tafiti zinasema kuwa baadhi ya wanafunzi wa vyuo vikuu hawafahamu rasilimali za mtandao zinazoweza kuwasaidia kufanya utafiti wao. Hivyo, utafiti huu unachunguza matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno. Madhumuni ya utafiti huu ni, kupambanua rasilimali za Kiswahili za kiakademia za mtandao, kutathmini matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno na kutathmini ufaafu wa rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia zinazotumiwa na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno. Nadharia ya Mawasiliano inayorejelea Matumizi na Utoshelezi iliyoasisiwa na Herzog (1944) na kuendelezwa na Gurevitch & Haas (1973), Katz & blumler (1974), Mc Quail (1983) na Ruggiero (2000) imetumiwa kuongoza utafiti huu. Mihimili ya nadharia hii ni uchaguzi wa chombo cha habari na hadhira tendi ili kutosheleza mahitaji yao. Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo ambapo mbinu za kithamano na kitakwimu zilitumiwa. Chuo Kikuu cha Maseno kilichaguliwa kimaksudi kama sampuli ambapo wanafunzi 54 wa Kiswahili wa mwaka wa nne shahada ya kwanza waliteuliwa kibahati nasibu kupata data. Vifaa vya ukusanyaji data vilihusisha hojaji iliyopewa wanafunzi wa Kiswahili wakiwa kwenye mhadhara, mtafiti alitumia orodha ya uchunzaji kuchunguza katika mtandao kuthibitisha kuwepo na ufaafu wa rasilimali za Kiswahili za mtandao. Data ilichanganuliwa kithamano, kiwingi idadi, kiuthibitishi na kuwasilishwa kimaelezo kwa viwango vya idadi na asilimia ya majibu yaliyotolewa na wanafunzi na kuwekwa katika majedwali. Mtafiti alithibitisha kuwa rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia zipo, zinafaa na zinatumiwa na wanafunzi wa Kiswahili kufanya utafiti. Wengi wa wanafunzi wa Kiswahili walifaidika na rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia kwani utafiti wa Kiswahili uliboreshwa kwa kuhusisha mambo ya kisasa. Mapendekezo ya utafiti ni kuwa, wahadhiri wa Kiswahili waendelee kuwaelekeza wanafunzi wa Kiswahili kutambua rasilimali zaidi ili waweze kuzitumia na wanafunzi wa Kiswahili wasisitize matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia.

**Abstract**

The Internet has a lot of academic resources that are of significance to university students and their research in regard to various courses. However, most studies have indicated that, most university students use the Internet for entertainment rather than academic purposes. Hence, a lot of Internet academic resources may not be utilised well since most students have no interest in them or they are not aware of their existence. This study has focussed on the use of Kiswahili academic internet resources by Kiswahili students of Maseno University. The objectives of the study included to find out Kiswahili academic internet resources, to determine the use of Kiswahili academic internet resources by Kiswahili students of Maseno University and determine the quality of Kiswahili academic internet resources used by Kiswahili students of Maseno University. The research was guided by the theory of Communication based on Uses and Gratification as explained by Gurevitch & Haas (1973), Katz & Blumler (1974), Mc Quail (1983) and Ruggiero (2000) and its founder Herzog (1944). The tenets of the theory are the choice of media by active audiences to satisfy their needs. Descriptive survey design was employed by use of both qualitative and quantitative approaches. Maseno University was purposefully selected to be used as a sample. Fifty four fourth year undergraduate Kiswahili students were randomly sampled from lecture halls to fill in questionnaires. The researcher administered questionnairres to Kiswahili students, observed Kiswahili resources on the Internet and used the checklist as a guide to identify Kiswahili resources. Data from the questionnaire and the internet was analysed qualitatively by giving explanations on availability and use of Kiswahili Internet resources and quantitatively by giving the number of resources they make use of them. Meta analysis was used to confirm the availability and quality of Kiswahili resources. Data was later presented in table as percentages of the number of responses given by students on the use of Kiswahili Internet resources. The researcher confirmed that the internet has Kiswahili resources and most of the students use them to carry out Kiswahili research. Some Kiswahili internet resources were not used frequently for example dictionaries because they had few words translated from other languages especially English to Kiswahili. The quality of Kiswahili Internet resources were that they are upto date and well developed. Recomendations were that Kiswahili lecturers should continue giving guidance to Kiswahili students on the availability of other Kiswahili Internet resources and that these students should continuosly use Kiswahili Internet resources to develop their Kiswahili studies.

**YALIYOMO**

Ikirari ii
Shukrani iii
Tabaruku iv
Ikisiri v
Abstract vi
YALIYOMO vii
Orodha ya majedwali xi
Orodha ya vifupisho xiii
Ufafanuzi wa dhana muhimu xiv
SURA YA KWANZA 1
UTANGULIZI 1
1.1 Usuli wa utafiti 1
1.2 Suala la utafiti 5
1.3 Maswali ya utafiti 5
1.4 Madhumuni ya utafiti 5
1.5 Misingi ya uteuzi 6
1.6 Upeo wa utafiti 6
1.7 Misingi ya kinadharia 7
1.7.1 Uasili wa nadharia ya Mawasiliano inayorejelea Matumizi na Utoshelezi 7
1.7.2 Mihimili ya nadharia ya Mawasiliano inayorejelea Matumizi na Utoshelezi 8
1.7.3 Matumizi ya nadharia katika utafiti huu 9
1.8 Hitimisho 11
SURA YA PILI 12
UHAKIKI WA MAANDISHI 12
2.1 Utangulizi 12
2.2 Maendeleo ya nadharia ya matumizi na utoshelezi 12
2.2 Historia ya mtandao 14
2.4 Rasilimali za mtandao wa kiakademia 16
2.4.1 Sifa za mtandao 16

2.5 Matumizi ya rasilimali za mtandao na wanafunzi wa vyuo vikuu........................................ 21
2.5.1 Ufahamu wa rasilimali za mtandao na wanafunzi wa vyuo vikuu ..................................... 22
2.5.2 Viwango vya matumizi ya rasilimali za mtandao na wanafunzi wa vyuo vikuu................ 23
2.5.3 Umuhimu wa matumizi ya rasilimali za mtandao na wanafunzi wa vyuo vikuu ................ 32
2.5.4 Changamoto zilizowakumba wanafunzi wa vyuo vikuu walipotumia rasilimali za mtandao ........................................................................................................................................ 38
2.6 Ufaafu wa rasilimali za mtandao wa kiakademia zinazotumiwa na wanafunzi wa vyuo vikuu ........................................................................................................................................ 40
2.7 Hitimisho.............................................................................................................................. 42
SURA YA TATU ..................................................................................................................... 43
NJIA NA MBINU ZA UTAFITI.............................................................................................. 43
3.1 Utangulizi............................................................................................................................. 43
3.2 Muundo wa utafiti................................................................................................................ 43
3.3 Eneo la utafiti........................................................................................................................ 43
3.4 Kundi lengwa ....................................................................................................................... 44
3.5 Sampuli na usampulishaji ..................................................................................................... 44
3.6 Njia na Mbinu za kukusanya data......................................................................................... 45
3.6.1 Utafiti wa kimajaribio ........................................................................................................ 45
3.6.2 Mbinu za kukusanya data.................................................................................................... 46
3.6.2.1 Hojaji.................................................................................................................................. 46
3.6.2.2 Orodha ya uchunguzi ......................................................................................................... 47
3.6.2.3 Mtandao .............................................................................................................................. 47
3.7 Udhibiti wa vifaa vya kukusanya data .................................................................................. 47
3.8 Uchanganuzi na uwasilishaji wa data ................................................................................... 48
3.8.1 Uchanganuzi wa data kithamano ........................................................................................ 48
3.8.2 Uchanganuzi wa data kitakwimu......................................................................................... 48
3.8.3 Uchanganuzi wa data kwa kuthibitisha................................................................................ 49
3.8.4 Uwasilishaji wa data ............................................................................................................ 49
3.9 Uzingatifu wa maadili.......................................................................................................... 49
SURA YA NNE........................................................................................................................ 50
MATOKEO NA UCHANGANUZI .......................................................................................... 50

4.1 Utangulizi ........ 50
4.2. Rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia ........ 50
4.2.1 Majarida ........ 52
4.2.2 Magazeti na idhaa za redio/ runinga ........ 52
4.2.3 Kamusi ........ 53
4.2.4 Mitandao ya Kiswahili ........ 53
4.3 Matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno. ........ 54
4.3.1 Ufahamu wa rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno ........ 55
4.3.2 Viwango vya matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno. ........ 56
4.3.3 Umuhimu wa matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia kwa utafiti wa Kiswahili ........ 70
4.3.4 Changamoto zinazowakumba wanafunzi wa Kiswahili walipotumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia ........ 73
4.4 Ufaafu wa rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia zinazotumiwa na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno ........ 76
4.4.1 Majarida ........ 77
4.4.2 Magazeti ........ 80
4.4.3 Idhaa za redio ........ 80
4.4.4 Kamusi ........ 80
4.4.5 Mitandao ya Kiswahili ........ 81
4.5 Hitimisho ........ 82
SURA YA TANO ........ 83
MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 83
5.1 Utangulizi ........ 83
5.2 Muhtasari ........ 83
5.2.1 Rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia ........ 83
5.2.2 Matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno ........ 83

5.2.3 Ufaafu wa rasilimali za Kiswahili za mtandao zilizotumiwa na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno ........ 84

5.2 Hitimisho ........ 85

5.4 Mapendekezo na Mapendekezo kuhusu utafiti zaidi ........ 87

5.4.1 Mapendekezo kiujumla ........ 87

5.4.2 Mapendekezo kuhusu utafiti zaidi ........ 88

MAREJELEO ........ 89

VIAMBATISHO ........ 100

a) Hojaji ya mwanafunzi ........ 100

B. Orodha ya uchunguzi ........ 104

## Orodha ya majedwali

**Jedwali** **Ukurasa**

**Jedwali 1** Rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia zinazotumika na wanafunzi wa Kiswahili 51

Jedwali 2 Majarida yaliyo na makala katika lugha ya Kiswahili 52

**Jedwali 3** Ufahamu wa rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno 55

**Jedwali 4** Matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili kufanya utafiti 55

**Jedwali 5** Lugha inayotumiwa na wanafunzi wa Kiswahili katika mtandao wa kiakademia kufanya utafiti 57

Jedwali 6 Muda wa matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili 58

**Jedwali 7** Tajriba ya kuzitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia 59

**Jedwali 8** Ujuzi wa wanafunzi wa Kiswahili wa kutumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia 60

**Jedwali 9** Njia za ujifunzaji wa namna ya kutumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia 61

**Jedwali 10** Umuhimu wa kozi ya Habari na Teknolojia kwa wanafunzi wa Kiswahili 62

**Jedwali 11** Kinachowasukuma wanafunzi wa Kiswahili kutumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia 63

**Jedwali 12** Mahali wanafunzi wa Kiswahili wanapata huduma na rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia 64

**Jedwali 13** Rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia zinazotumiwa zaidi na wanafunzi wa Kiswahili 65

**Jedwali 14** Njia zinazotumiwa na wanafunzi wa Kiswahili kudurusu kwenye mtandao wa kiakademia 66

**Jedwali 15** Injini pekuzi inayotumiwa zaidi na wanafunzi wa Kiswahili 67
**Jedwali 16** Sababu za wanafunzi wa Kiswahili kuzitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia 69
**Jedwali 17** Umuhimu wa matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia kwa utafiti wa Kiswahili 70
**Jedwali 18** Utoshelezi wa matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia 71
**Jedwali 19** Changamoto zinazowakumba wanafunzi wa Kiswahili walipotumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia 73
**Jedwali 20** Ufaafu wa rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia 76

## Orodha ya vifupisho

**ARPA -** *Advanced Research Projects Agency*

**ARPANET** – *Advanced Research Projects Network*

**BBA** - Shahada ya Usimamizi wa Biashara

**Bw.** – Bwana

**DARPA** - *Deffence Advanced Research Projects Agency*

**GRETSA** – Chuo Kikuu

**KENET** – Shirika la mtandao Kenya

**MSC.** – Uzamili katika sayansi

**TEKNOHAMA** – Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

**USAID** – *United States Agency for International Development*

**WWW -** Mtandao Wa Ulimwengu Nzima

## Ufafanuzi wa dhana muhimu

**Blogu –** Mtandao wa ubadilishanaji maoni

**Injini pekuzi** – Mashini zinazotumiwa kutafuta habari

**IP/ TCP** – Itifaki inayokubalika ya intanet 'Suite'

**Mtandao** – Mfumo unaowezesha tarakilishi mbalimbali duniani kuwasiliana kati zao

**Simu tamba** – Simu ya mkononi inayotumiwa kurahisisha mawasiliano

**WI FI** – Hutoa upatikanaji usiotumia waya wa mitandao ya tarakilishi

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

Sehemu hii ilishughulikia usuli wa utafiti, suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, umuhimu wa utafiti, upeo wa utafiti, misingi ya uteuzi na misingi ya kinadharia.

## 1.1 Usuli wa utafiti

Mtandao na tarakilishi ni sehemu muhimu ya maisha na vimekuwa vyombo muhimu katika elimu. Mtandao hutumika sana na watu ulimwenguni kote. Kwa sasa unatumiwa kufunza katika shule na vyuo mbalimbali. Asili ya mtandao ni miaka ya 1950 na ilihusishwa na mambo matatu, kwanza, wakati nchi ya Russia ilipoanzisha setalaiti iliyoitwa 'Sputnik', wakati wa vita vikuu na ukuaji wa mtandao wa 'ARPANET' (Advanced Research Project Agency Network) Shirika lililoshughulikia tafiti za mtandao kule Marekani.

Matumizi ya mtandao katika karne hii umekuwa jambo la muhimu. Uhitaji wa kutumia mtandao unatokana na jukumu lake kuu katika TE(KNO)HAMA na upatikanaji wa majarida, magazeti na habari nyingine kwenye rasilimali tofauti wakati wowote (Llo & Ifijeh, 2010). Mtandao una rasilimali ambazo huweza kutumiwa na watu katika sekta mbalimbali. Tafiti mbalimbali zimechunguza matumizi ya rasilimali za mtandao miongoni mwa wanafunzi na wasomi kwa ujumla bila kuzingatia masomo mahsusi (Badu & Markwei, 2005; Luambano & Nawe, 2004; Malik & Mahmood, 2009; Bankole & Babalola, 2012). Hivyo, utafiti huu ulichunguza matumizi ya rasilimali za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa somo la Kiswahili. Wengi wa wasomi na wanafunzi hawajui kuzitambua rasilimali hizi katika mtandao labda kwa sababu hawajafundishwa au hawajatafuta namna ya kuzifikia (Jones & Madden, 2002) na baadhi ya wanaozitumia rasilimali hizi, imekuwa vigumu wao kukadiria ufaafu wake kwa sababu hawafahamu vigezo muhimu vya kuwasaidia kufanya hivyo.

Tafiti zilizochunguza matumizi ya mtandao miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu, zilitambua kuwa, matumizi ya rasilimali za mtandao yalisaidia katika kupata habari za kiakademia kwa wakati mzuri hasa ikiwa wanafunzi walikuwa na ujuzi unaofaa. Tafiti zingine

zimejikita katika kuonyesha matatizo yanayotokana na matumizi ya rasilimali hizi za mtandao. Matatizo haya ni kama vile; uhaba wa tarakilishi na huduma za mtandao, kukwama au kujikokota kwa mtandao na kukatizwa kwa nguvu za umeme (Luambano & Nawe, 2004; Malik and Mahmood, 2009; Khan, Khan & Bhatti, 2011). Utafiti huu ulichunguza umuhimu wa matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia.

Baadhi ya tafiti kuhusu matumizi ya mtandao miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu zinaafikiana kuwa, wengi wa wanafunzi wa vyuo vikuu walitumia mtandao kufanya tafiti zao (Ani, 2010; Bankole & Babalola, 2012; Osunade, 2003). Hata hivyo, baadhi ya tafiti zimetambua kuwa wanafunzi wa vyuo vikuu waliutumia mtandao kuburudika na kuwasiliana na marafiki wao (Luambano & Nawe, 2004). Hata hivyo, wanafunzi wa vyuo vikuu walitumia mtandao kuwasiliana na wenzao, kufanya utafiti, kuwafikia maprofesa wao ili kutimiza mahitaji ya kiakademia na kuburudika. Utafiti huu ulizingatia mtandao wa kiakademia si mtandao kwa jumla.

Utafiti wa Khan, Khan & Bhatti (2011) wanasema kuwa, wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Islamia Kule Pakistan walikuwa na mielekeo chanya kuhusiana na matumizi ya mtandao. Matumizi ya mtandao yalitokana na ujuzi walionao hasa kutoka kwa marafiki au msukumo wa kibinafsi. Zhixian (2008) akiwataja Taylor, Zhu, Dekkers na Marshall (2003), waliosema kuwa, ni matarajio kuwa wanafunzi wa vyuo vikuu wanaosoma viwango vya juu vya elimu wanaweza kutumia mtandao kwa urahisi kwa sababu wana ujuzi wa yaliyomo na nafasi ya kuutumia. Hivyo, wanafunzi wa vyuo vikuu wanatarajiwa kuwa na ujuzi wa namna ya kuutumia mtandao (Stutzer, 2010) lakini hali sivyo kwa baadhi yao. Utafiti huu ulichunguza ujuzi wa wanafunzi wa Kiswahili wanapozitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia.

Mtandao una umuhimu mkubwa kwa watumiaji wake. Tafiti nyingi zimeangazia umuhimu wa matumizi ya rasilimali za mtandao miongoni mwa wanafumzi wa vyuo vikuu. Baadhi ya tafiti zilizozingatia athari ya matumizi ya mtandao kwa matokeo ya mitihani ni Tella (2007) na Osunade (2003), ambao wanasema kuwa rasilimali za mtandao ziliboresha matokeo ya mitihani. Umuhimu wa rasilimali za mtandao kwa utafiti zimeweza kushughulikiwa na baadhi ya wasomi kama vile (Luban, 2000; Llo & Ifijeh, 2010) walipata kuwa rasilimali za mtandao zilifanya

utafiti kuwa bora, wanafunzi waliutumia muda wao vizuri, tafiti kuandikwa kwa kasi na kuwa na maandishi bora. Wanafunzi wa vyuo vikuu walipata matokeo mazuri katika mitihani yao baada ya kuutumia mtandao Tella (2007). Hivyo, utafiti huu ulichunguza umuhimu wa rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia kwa utafiti wa Kiswahili.

Matumizi ya mtandao miongoni mwa nchi zinazoendelea yanazidi kuimarika kila uchao. Nchi ya Kenya ni mojawapo wa nchi hizi ambapo haijaachwa nyuma na maendeleo ya TE(KNO)HAMA na matumizi ya mtandao. Wengi wa wanafunzi wa vyuo vikuu nchini Kenya wanatumia mtandao. Baadhi ya tafiti zilizofanywa zinasema kuwa, wanafunzi hutumia mtandao hasa kutosheleza mahitaji ya burudani, mahusiano ya kirafiki, kupitisha wakati, kupata habari na kuhifadhi mawasiliano (Kaye, 1998). Wanafunzi hawa hutumia sana kurasa za mahusiano kama vile, *Facebook, Tweeter, na Linkedh.* Oduor (2010) anasema kuwa, kurasa hizi huwasaidia kukutana na marafiki kutoka pembe zote za dunia. Hata hivyo, mtandao umekuwa na manufaa kwa wanafunzi wa vyuo vikuu na vyuo vikuu vyenyewe. Utafiti huu ulitaka kujua ikiwa wanafunzi wa Kiswahili walizitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia .

Taasisi za kiakademia zinajaribu sana kuimarisha TE(KNO)HAMA. Hili limepelekea taasisi hizi kurahisisha upatikanaji wa huduma za mtandao kwa wafanyikazi wake pamoja na wanafunzi. Mtandao umeongeza nafasi mpya za kiakademia kwa wanafunzi wa vyuo vikuu (Jones & Madden, 2002) ambapo wameweza kupata habari za kiakademia zinazokuza tafiti zao. Hata hivyo, tafiti mbalimbali zimeonyesha kuwa wanafunzi nchini Kenya hutumia mtandao kwa upana sana lakini kwa nadra sana kwa masuala ya kiakademia (Waithaka, 2013). Haya ni sawa na maoni ya (Jones & Madden 2002) ambao walisema kuwa wengi wa wanafunzi wa vyuo vikuu hutumia mtandao kwa mawasiliano ya kijamii kuliko masuala ya kiakademia. Hivyo, tulichunguza wanafunzi wa Kiswahili kujua ikiwa walizitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia.

Nchini Kenya kuna takriban vyuo ishirini na viwili vya umma vilivyosajiliwa na vingine vishiriki. Miongoni mwao ni Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenyatta, Egerton, Moi, Jomo Kenyatta, Masinde Muliro, Maseno na kadhalika. Pia kuna vyuo vya kibinafsi kama Chuo Kikuu cha Daystar, Chuo Kikuu cha Methodist na vingine ambavyo vimejizatiti kuwawekea wanafunzi wao

maktaba za tarakilishi zilizounganishwa kwenye mtandao ili kuwawezesha kuzifikia rasilimali za mtandao. Baadhi ya vyuo vya umma vina maktaba zenye tarakilishi ambazo hazijaunganishwa katika mtandao au ikiwa zimeunganishwa ni tarakilishi chache (Shabaya, 2009). Lugha ya Kiswahili ni mojawapo ya masomo yanayofunzwa katika baadhi ya vyuo vya umma na vya kibinafsi nchini Kenya. Somo la Kiswahili katika vyuo vikuu nchini Kenya si la lazima. Hivyo jukumu lake ni dogo mno (Momanyi, 2007). Maktaba za vyuo hivi hazina vitabu vya kutosha vya Kiswahili hivyo mtandao huenda ndio suluhisho la kupata habari zaidi na wanafunzi wa Kiswahili.

Chuo Kikuu cha Maseno kilianzisha kozi za teknolojia na mawasiliano mwaka wa 2004 kama kozi za hiari lakini kuanzia mwaka wa 2005, kozi hizi zilifanywa za lazima. Wanafunzi wote wa chuo hiki walipaswa kusoma kozi hizi ili wahitimu na kupewa cheti. Mojawapo wa kozi hizi ni ile ya namna ya kutumia mtandao inayofundishwa mwaka wa tatu. Kozi hii humwezesha mwanafunzi kuwa na ujuzi wa kutosha wa kutafuta habari anazozihitaji na kuwasiliana na wenzake kutoka ulimwengu mzima. Zaidi ya hayo, kozi hizi zimewafaa wanafunzi wa Kiswahili kwani wengi wao wameweza kujua kutumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia kufanya utafiti wao. Hivyo, madhumuni ya kozi hii yanaafikiwa kwa sababu wanafunzi wana ujuzi wa kutosha.

Hivyo, tafiti zimeonyesha kuwa, matumizi ya rasilimali za mtandao ni muhimu katika elimu. Hata hivyo, ili kuhakikisha kuwa wamefanikiwa katika utafiti wao, wanafunzi wanapaswa kuzitazama vizuri rasilimali za mtandao ndipo wazitumie. Wanapotumia rasilimali za mtandao wanapaswa kuwa na nidhamu ili waepuke maeneo ambayo ni ya burudani ili waweze kupata matokeo mazuri ya utafiti wao. Matumizi ya mtandao yamekuwa na majukumu ya kuwasaidia watafiti wa shahada ya kwanza kupata habari nyingi kutoka sehemu mbalimbali za ulimwengu. Kwa kuzingatia mtazamo huu, utafiti huu ulichunguza kuwepo kwa rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia, matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Masneo na ufaafu wa rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia. Chuo Kikuu cha Maseno kiliteuliwa kwa sababu kinatoa kozi za Habari na Teknolojia kwa wanafunzi wote kama somo la lazima. Wanafunzi wa Kiswahili mwaka wa nne waliteuliwa kwa sababu ya tajriba yao ya kuwa chuoni na matumizi yao ya mtandao.

## 1.2 Suala la utafiti

Mtandao una umuhimu mkubwa kwa wanafunzi wa vyuo vikuu. Matumizi yake miongoni mwa baadhi ya wanafunzi yamekuza tafiti zao za kiakademia na kuboresha matokeo ya mitihani. Hata hivyo, wengi wa wanafunzi wa vyuo vikuu hawautumii mtandao kwa masuala ya kiakademia. Vyuo vikuu nchini Kenya vimejizatiti kuimarisha TE(KNO)HAMA ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wao wanapata huduma za mtandao. Chuo Kikuu cha Maseno ni mojawapo wa vyuo ambavyo hutoa masomo ya Habari na Teknolojia. Masomo haya ni ya lazima kwa wanafunzi wote wa chuo hiki. Utafiti wa kutathmini namna wanafunzi wanavyotumia mafunzo hayo kuzitumia rasilimali za mtandao wa kiakademia ni jambo ambalo halijashughulikiwa. Hivyo, utafiti huu ulichunguza rasilimali za Kiswahili, matumizi na ufaafu wa rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno.

## 1.3 Maswali ya utafiti

Ili kuchanganua matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno, utafiti huu uliongozwa na maswali matatu yafuatayo:

1. Rasilimali zipi za Kiswahili zinapatikana katika mtandao wa kiakademia?
2. Wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno wanazitumia vipi rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia?
3. Rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia zinazotumiwa na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno zinafaa?

## 1.4 Madhumuni ya utafiti

Utafiti huu ulilenga kuchanganua matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno. Lengo hili liliafikiwa kwa kuzingatiwa madhumuni yafuatayo:

1. Kupambanua rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia.
2. Kutathmini matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno.
3. Kutathmini ufaafu wa rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia zinazotumiwa na wanafunzi wa Kiswahili.

## 1.5 Misingi ya uteuzi

Mtandao kama ilivyo teknolojia nyingine, umerahisisha maisha ya wengi wa watumiaji wake (Luambano & Nawe 2004). Mada hii iliteuliwa kutokana na sababu za maendeleo ya teknolojia yaliyopo na usasa wa mawasiliano hasa miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu. Wanafunzi wa vyuo vikuu wanapaswa kutumia mtandao huu kwa sababu una maarifa na habari nyingi zitakazowafaa katika masomo yao. Kuna uhitaji mkubwa wa wanafunzi hawa kuwa na ujuzi huu. Chuo Kikuu cha Maseno kilianzisha kozi za lazima zinazohusu Habari na Teknolojia mwaka wa 2005. Miongoni mwa kozi zinazofundishwa ni zile zinazohusu mtandao. Wanafunzi wa Kiswahili wa mwaka wa nne kama ilivyo wanafunzi wengine wanatarajiwa kuwa na ujuzi huu kwa sababu kozi ya mtandao hufundishwa katika mwaka wa tatu. Chuo kikuu cha Maseno kiliteuliwa kwa sababu hutoa kozi za lazima za Habari na Teknolojia kwa wanafunzi wote na pia itakuwa rahisi kwa mtafiti kupata data.

Kutokana na juhudi zinazofanywa na wanasayansi kuhakikisha kuwa teknolojia imeenea kila pembe za dunia, utafiti huu utakuwa na umuhimu kadha. Kwanza, utafiti utawafaa baadhi ya wanafunzi wa Kiswahili ambao hawakuzingatia zaidi matumizi ya mtandao wa kiakademia kwa kutambua umuhimu wake katika masomo yao. Pili, utawafaa watoaji wa huduma za mtandao kwa kutambua mahitaji ya wateja wao ambao ni wanafunzi wa Kiswahili kama vile kuongeza kurasa nyingine katika lugha ya Kiswahili ili kujaribu kuhakikisha kuwa wanatosheleza mahitaji ya kila mtumizi wa mtandao. Hili litahusu kuwapa wateja wao rasilimali na huduma zinazowafaa. Tatu, waundaji sera watafaidika kwa sababu wataibuka na tovuti mbalimbali ambazo zitawafaa wanafunzi wa Kiswahili. Mwisho, wasomi wa Kiswahili watashawishika kuhakikisha kuwa tafiti zao za Kiswahili zinawekwa katika mtandao wa kiakademia ili kuwanufaisha wanafunzi wa Kiswahili.

## 1.6 Upeo wa utafiti

Utafiti ulichunguza rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia, matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno na ufaafu wa rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia zinazotumiwa na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno. Rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia

zilizochunguzwa ni katika lugha za Kiswahili na Kiingereza na zina mambo ya Kiswahili. Wanafunzi wa Kiswahili wa shahada ya kwanza wa mwaka wa nne wa Chuo Kikuu cha Maseno walitumiwa kwa sababu walikuwa na tajriba ya kuwa chuoni na kuutumia mtandao. Mihimili ya nadharia ya Mawasiliano inayorejelea matumizi na utoshelezi iliyotumiwa ni uchaguzi wa chombo cha habari na hadhira tendi ili kutosheleza mahitaji yao. Wakati wa utafiti ulikuwa kati ya mwaka 2013 hadi 2015.

## 1.7 Misingi ya kinadharia

### 1.7.1 Uasili wa nadharia ya Mawasiliano inayorejelea Matumizi na Utoshelezi

Nadharia hii iliasisiwa na Herzog (1944 na kuendelezwa na Lazrsfeld and Stanton (1944), Waner and Henry (1948), Gurevitch and Haas (1973), Blumler and Katz (1974), Mc Quail (1983). Nadharia ya Matumizi na Utoshelezi ilitokana na nadharia ya Uamilifu ambayo iliathiri sana tafiti za mawasiliano na ilihusiana na sayansi za kijamii. Nadharia ya Uamilifu ilitumika kuelezea athari ya vyombo vya habari kwa watumiaji wake. Baadaye kulikuwa na mabadiliko ambapo watafiti walitambua kuwa kulikuwa na uhusiano kati ya vyombo vya habari na watumizi wake. Hali hii ilipelekea kuzuka kwa nadharia ya Matumizi na Utoshelezi ambayo ilitumiwa kuelezea sababu zinazowafanya watumiaji wa vyombo vya habari kuchagua vyombo tofauti tofauti. Watafiti walitambua kuwa watumiaji walichagua vyombo fulani vya habari ili kutosheleza mahitaji yao (Blumler and Katz, 1974).

Miaka ya 1940, nadharia hii ilitumika na watafiti mbalimbali kujua sababu zinazowapelekea watu kusikiza vipindi tofauti katika redio na kusoma makala maalum katika magazeti. Tafiti hizi zilionyesha kuwa, yaliyomo katika chombo cha habari yalikuwa na umuhimu kwa watumiaji wake. Lazrsfeld & Stanton (1944) na Herzog (1944) walitumia nadharia hii katika tafiti zao ambapo waliweza kutambua majukumu ya vyombo vya habari kwa watumiaji wake. Kwa mfano, vipindi vya redio viliwapa wasikilizaji mawaidha na magazeti yaliyowawezesha watu kuzungumzia mada tofauti tofauti, hali iliyowapelekea wao kuchagua vyombo hivyo vya habari.

Miaka ya 1950 hadi 1980, nadharia hii ilikuzwa sana na watafiti kama Gurevitch, Haas and Katz (1973), Blumler and Katz (1974) na Mc Quail (1983). Wao walitumia nadharia hii kuelezea

matumizi mbalimbali ya vyombo vya habari. Walitambua kuwa watu walitumia vyombo mbalimbali vya habari ili kutosheleza mahitaji yao. Mahitaji haya yamo katika makundi manne (Katz, Gurevitch & Haas, 1973) nayo ni: mahitaji ya kiakili, ya kuvuta, kibinafsi na ya kuondoa wasiwasi. Kwa mujibu wa Mc Quail (1983) utoshelezi wa hadhira unaweza kutimia kupitia chombo cha habari ikiwa mtumiaji wake alikichagua. Alitambua kuwa watu walitumia chombo cha habari kupata habari, kuburudika kujituliza na kujitambua kama mtu binafsi.

Matumizi ya nadharia hii katika tafiti za wataalamu wa mawasiliano yalifaulu. Waliweza kutumia nadharia hii kueleza utoshelezi waliopata watumizi wa vipindi tofauti kwa kupata burudani na kujua yanayoendelea katika sehemu mbalimbali walizoishi. Hadhira ilielewa yaliyomo katika vipindi na ilichagua vipindi fulani ili kutosheleza mahitaji yao.

### 1.7.2 Mihimili ya nadharia ya Mawasiliano inayorejelea Matumizi na Utoshelezi

Nadharia hii ina mihimili ifuatayo iliyotumiwa katika utafiti huu;

Kwanza hadhira inajua yaliyomo katika chombo cha habari na chombo kipi kinachotosheleza mahitaji yao. Mahitaji yao yataathiri chombo cha habari atakachokitumia na namna atakavyotumia na utoshelezi anaopata kutokana na chombo cha habari. Kuongezea, huchunguza sababu zinazowapelekea watu kutumia chombo fulani cha habari na kutotumia kingine na utoshelezi wanaopata kwa kuzingatia mahitaji ya kibinafsi, kijamii na kisaikolojia (Severin & Tankard, 2001). Wanafunzi wa Kiswahili walizitumia rasilimali za Kiswahili za mtaandao wa kiakademia iiwa walizijua.

Kulingana na Blumler & Katz (1974), nadharia inasisitiza uchaguzi wa hadhira kwa kuangalia sababu zinazowafanya kutumia chombo fulani cha habari na kutotumia kingine. Sababu hizi huzingatiwa kwa kutazama utoshelezi wanaopata. Chombo cha habari ni mtandao ambao mwanafunzi wa Kiswahili anaweza kuamua kuutumia kwa sababu unampa habari nyingi zinazomsaidia kufanya tafiti zake za Kiswahili, kinafaa na ni bora kwake. Kwa upande mwingine, kuna wale ambao wanaweza kutumia vyombo vingine kwa sababu labda habari zinapatikana kwa urahisi ikilinganishwa na mtandao.

Chombo cha habari kinapaswa kumfanya mtumiaji wake kuwa tendi. Mtandao ni chombo cha habari ambacho humfanya mtumiaji wake kuwa tendi (Ruggiero, 2000). Mazoezi katika mtandao yanaweza kumfanya mwanafunzi kuwa mchangamfu anapotumia mtandao. Hii ni kutokana na hali kuwa, mihadhara kwa kiwango fulani humfanya mwanafunzi kuwa tuli, mchango wake ni mdogo mno kwa sababu wahadhiri ndio wanaopeana mafunzo. Wanafunzi wa Kiswahili wanapaswa kuhudhuria mihadhara, kusoma vitabu pamoja na kufanya mazoezi ya moja kwa moja hasa katika mtandao ili kupata habari zaidi kuhusiana na tafiti zao za Kiswahili.

Utoshelezi wa hadhira unaweza kutimia kupitia chombo cha habari (Mc Quail, 1983). Mtaalamu huyu anasema kuwa watu hutumia chombo cha habari ili kupata habari, kuburudika, kujituliza na kujitambua kama mtu binafsi. Mwanafunzi wa Kiswahili anapaswa kutumia mtandao kupata habari zitakazomsaidia kufanya tafiti zake za Kiswahili na kumuunganisha na wanafunzi wengine ulimwenguni.

### 1.7.3 Matumizi ya nadharia katika utafiti huu

Nadharia hii ina umuhimu ufuatao; kwanza, huheshimu uwezo wa kiakili yaani kuonyesha ufahamu wa yaliyomo wa watumizi wa vyombo vya habari (Baran & Davis, 2006). Uwezo huu uliheshimiwa wakati mwanafunzi wa Kiswahili alitumia rasilimali za mtandao kufanya tafiti zake za Kiswahili. Pili, hutuonyesha uchanganuzi wa tajriba ya watu kuhusiana na yaliyomo katika chombo cha habari. Wanafunzi wa Kiswahili mwaka wa nne wana tajriba ya kutosha ya kutumia mtandao ikilinganishwa na wale wa viwango vya chini. Itakuwa rahisi kwa mtafiti kupata data kamili kutoka kwa mwanafunzi wa mwaka wa nne kwa sababu ni mambo wanayoyafahamu. Wanaelewa yaliyomo yaani rasilimali katika mtandao hivyo, wataweza kujua umuhimu na changamoto zake.

Nadharia ilisaidia katika kueleza utoshelezi wa mtandao kwa wanafunzi wa Kiswahili wanapofanya tafiti za Kiswahili. Hivyo, nadharia ilisaidia kueleza umuhimu waliopata wanafunzi wa Kiswahili walipotumia rasilimali za Kiswahili za mtandao kufanya tafiti za Kiswahili. Pili, ujuzi wa wanafunzi wa Kiswahili ulijitokeza waziwazi kwa sababu inasisitiza kuwa hadhira huwa na ujuzi wa kutumia chombo cha habari. Utendi wa wanafunzi hawa

utadhihirika waziwazi kwa sababu iliwabidi wao kujihusisha na mtandao kibinafsi ili kutosheleza mahitaji yao. Umuhimu wa rasilimali za Kiswahili za mtandao zilidhihirika waziwazi kupitia utumizi wake na wanafunzi.

Mihimili ya nadharia ya Mawasiliano inayorejelea matumizi na utoshelezi ya uchaguzi wa chombo cha habari na hadhira tendi kutosheleza mahitaji yao ina manufaa kwani mtafiti aliweza kutambua rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia walizozifahamu wanafunzi wa Kiswahili . Hii ni kutokana na hali kuwa hadhira hujua yaliyomo katika chombo cha habari. Baadhi ya wanafunzi wa Kiswahili wanajua rasilmali za mtandao katika mtandao. Rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia zinazotumiwa zaidi na wanafunzi wa Kiswahili zitaweza kutambuliwa kutokana na mhimili kuwa hadhira huchagua chombo fulani cha habari ili kutosheleza mahitaji yao.

Utendi wa wanafunzi wa Kiswahili ulidhihirika wazi wakati ambapo mtafiti alitambua kuwa wanafunzi wa Kiswahili walizitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia kufanya tafiti za Kiswahili. Pia maelezo ya namna walivyozitumia rasilimali za mtandao yalielezwa. Utoshelezi wa kutumia rasilimali za mtandao na wanafunzi wa Kiswahili ulitambuliwa wakati ambapo wengi wa wanafunzi walizitumia rasilimali hizi ili kufanya tafiti za Kiswahili. Hili litapelekea kazi yao kurahisishwa na kufanywa kwa haraka.

Hata hivyo, kuna baadhi ya wataalamu kama vile, Defleur na Ball- Rokeach (1998) wanasema kuwa, nadharia hii ina udhaifu. Kwanza, nadharia hii imezingatia zaidi matumizi ya chombo cha habari kibinafsi na kupuuza miktadha ya kijamii. Wanaopinga nadharia hii wanasema kuwa, ikiwa utaeleza matumizi ya chombo cha habari ni lazima pia ueleze yaliyomo. Hivyo, udhaifu huu hautaathiri utafiti huu kwa sababu mihimili yake ni bora. Utafiti huu utajikita katika mihimili ya nadharia hii na udhaifu uliopo haukuathiri kwa vyovyote matokeo yake. Utafiti utaangazia athari za matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao na wanafunzi wa Kiswhili.

## 1.8 Hitimisho

Sura hii ilishughulikia matumizi ya mtandao miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu kwa kurejelea rasilimali za mtandao na athari ya mtandao kwa wanafunzi hawa. Madhumuni ya utafiti huu yametajwa, suala la utafiti lilijadiliwa na misingi ya kinadharia ilielezwa kwa kuzingatia mada ya utafiti.

# SURA YA PILI

# UHAKIKI WA MAANDISHI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inashughulikia maandishi mbalimbali yanayohusiana na nadharia ya mawasiliano inayorejelea matumizi na utoshelezi, historia ya mtandao, rasilimali za mtandao za kiakademia, matumizi ya rasilimali za mtandao na wanafunzi wa vyuo vikuu na ufaafu wa rasilimali za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa vyuo vikuu. Wataalamu mbalimbali wamefanya tafiti zinazohusiana na mada hii na kutambua mambo kadha wa kadha yaliyotumiwa kulinganisha na kutofautisha na utafiti huu. Uhakiki wa maandishi ni muhimu kwa sababu mtafiti hawezi kurudia kufanya tafiti za watu wengine, hupata habari muhimu na hutambua maana zinazokubalika za dhana mbalimbali asemavyo (Mouton, 2006). Maandishi haya yalichangia pakubwa katika kuijenga kazi hii kwa kusaidia kutoa maelezo kwa undani kuhusu matumizi ya mtandao miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu.

## 2.2 Maendeleo ya nadharia ya matumizi na utoshelezi

Nadharia ya Mawasiliano inayorejelea matumizi na utoshelezi imekuzwa na watafiti wa kisasa na imehusishwa na teknolojia ya kisasa. Kuchipuka kwa vyombo vipya vya habari kumesaidia kukuza nadharia hii. Baadhi ya wataalamu kama vile Ruggiero (2000) anasema kuwa nadharia ya matumizi na utoshelezi imetumiwa katika kuongoza tafiti mbalimbali zinazohusiana na vyombo vya habari kama vile magazeti, redio, runinga na kwa sasa mtandao. Nadharia hii inafaa kuongoza utafiti wa matumizi ya mtandao kwa sababu mazingira ya mtandao huifanya hadhira kuwa tendi kama washiriki wa mawasiliano ikilinganishwa na vyombo vya zamani vya habari.

Tafiti mbalimbali za kisasa zimetumia nadharia hii kueleza matumizi ya mtandao miongoni mwa watu mbalimbali katika jamii. Ryan (1995) ameitumia nadharia hii kuchunguza maeneo ya mtandao ambapo alieleza kuwa maeneo ya mtandao yaliwapa watu motisha ya kuzungumza wakiwa huru tofauti na ilivyo hali katika maisha halisi. Kaye (1998) anasema kuwa maeneo kama wavuti yalitumiwa kwa sababu za kisiasa, burudani na mawasiliano kati ya wanajamii. Wengi wa wataalamu walitambua kuwa watu waliutumia mtandao kuburudika, kupitisha wakati,

kupata habari na kupumzika (Ferguson na Perse, 2000; Luo, 2000). Kwa mujibu wa Charney (1996), wanafunzi wa vyuo vikuu waliutumia kupata habari, kuburudika na mawasiliano. Mtandao huipa hadhira yake mambo matatu makuu, nayo ni: mawasiliano, mahusiano na habari (December, 1996).

Clavio (2008) alitumia nadharia hii katika michezo ambapo alitafiti kuhusu sifa, matumizi na utoshelezi wa habari za michezo katika bodi za ujumbe kuhusu michezo katika mtandao. Alifaulu kuchanganua sifa, matumizi na utoshelezi unaopatikana kutokana na habari za michezo katika bodi hizo. Alipata kuwa wengi wa watumiaji wa habari hizi za michezo walikuwa wanaume wa takriban miaka 30. Wengi waliohojiwa walisema kuwa walitumia masaa kumi kwa wiki moja na michezo iliyowafurahisha sana ilikuwa ya kandanda na mchezo wa kikapu.

Chigona, Kankwenda & Manjoo (2008) wanasema kuwa, nadharia hii huruhusu kuchunguza motisha ya kutumia chombo cha habari. Wataalamu hawa walitaka kujua ni kwa nini watu hutumia mtandao katika simu za rununu, utoshelezi wanaopata na motisha wanayopata ili kuitumia katika kuufikia mtandao. Walichunguza wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Cape Town kule Afrika Kusini ambapo walitambua kuwa wanafunzi walitumia simu za rununu kuufikia mtandao kwa sababu walipata burudani, waliweza kuwasiliana na watu wengine na walipata habari zilizotosheleza mahitaji yao hasa ya kielimu.

Nadharia ya Mawasiliano inayorejelea Matumizi na Utoshelezi inaweza kutumiwa kueleza sababu zinazowafanya watu kutumia chombo fulani cha habari, namna wanavyokitumia kutosheleza mahitaji yao na kutambua athari chanya na hasi kwa mtumizi wa chombo cha habari (Lin, 1999). Nadharia hii husisitiza matumizi, utoshelezi, motisha ya kutumia chombo fulani cha habari na hadhira tendi. Hivyo, nadharia hii ilifaa kwani mtafiti alinuia kueleza rasilimali za Kiswahili katika mtandao, matumizi ya rasilimali hizi na athari yake kwa utafiti wa Kiswahili kwa jumla.

Jere & Davis (2011) walitumia nadharia hii katika sekta ya biashara ambapo walitaka kujua ni kwa nini wanawake wanaosoma magazeti walitumia sana magazeti yaliyochapishwa kuliko yale yaliyo katika mtandao. Alifaulu katika kuitumia nadharia hii kwani alitambua kuwa zaidi ya

watu 10,000 walitumia magazeti yaliyochapishwa ikilinganishwa na idadi ya watu 6,000 waliotumia magazeti katika mtandao. Kwa hivyo, wanafunzi wa Kiswahili pia hawatumii magazeti katika mtandao kutosheleza mahitaji yao ya kitafiti.

Mtandao una sifa za kipekee ambazo zinakuza mitazamo katika nadharia ya matumizi na utoshelezi. Kwa mfano, James, Wotring na Forrest (1995) wanasema kuwa ujifunzaji na mahusiano ya kijamii ndiyo motisha ya kutumia mtandao. Sifa ya upana na urefu wa habari na makala tofauti katika mtandao unasaidia katika kutumia nadharia ya matumizi na utoshelezi. Imewawezesha watafiti kujua namna hadhira inavyotazama chombo cha habari kwa kuzingatia upana na urefu wake. Hivyo, imetumika sana katika kueleza matumizi ya mtandao miongoni mwa watu mbalimbali (Ebersole, 1999).

Ni wazi kuwa nadharia hii imetumika sana katika maswala yanayohusu vyombo vya habari. Wengi wa wasomi wameshughulikia sana matumizi na utoshelezi unaotokana na matumizi ya chombo cha habari. Hivyo, mtafiti alinuia kutumia nadharia hii kuthibitisha rasilimali za Kiswahili katika mtandao, namna wanafunzi wanavyozitumia na ufaafu wa rasilimali hizi.
Mtandao umekuwepo kwa muda hivyo historia yake ni muhimu kuzingatiwa ili kuelewa matumizi yake hapo awali na sasa.

## 2.2 Historia ya mtandao

Mtandao huunganisha tarakilishi nyingi ulimwenguni kote na unaruhusu watu kupata habari, kujuliana hali na kusambaza habari mbalimbali. Mtandao ulitumiwa mara ya na wanasayansi pamoja na maprofesa wa vyuo vikuu kwanza (Defleur & Dennis, 2002). Maendeleo ya kiteknolojia wakati huo yalitokana na umoja wa wanajeshi wakati wa vita vya pili vya dunia. Hata hivyo, ilikuwa ni juhudi za serikali kuhakikisha kuwa mtandao unakua. Mwaka wa 1957 mradi wa utafiti ulioitwa ‘ARPA’( Advanced Research Projects Agency) ulianzishwa na ulishughulikia tafiti mbalimbali kule Marekani. Mwaka 1958, mradi ulioitwa ‘NASA’ ulianzishwa ambapo sasa ‘ARPA’ ilipewa majukumu mapya. ‘ARPA’ sasa ilianza kushughulikia sayansi ya tarakilishi na mchakato wa habari. Lengo lake lilikuwa kuunganisha tarakilishi mbalimbali katika vyuo vikuu vya nchi ya Marekani ili kuwezesha mawasiliano ya lugha moja (Ruggiero, 2000).

Mwaka 1960, tarakilishi zilipewa jukumu la kupasha habari za kisayansi na kijeshi. Kufikia mwaka 1962, mtaalamu Licklider alipendekeza kuunganishwa kwa tarakilishi ambapo aliibua nadharia ya Ubadilishaji. Mtaalamu Roberts alianza kwa kuunganisha tarakilishi za kule Massachuttes na zile za California kupitia nyaya za simu, mwaka 1965. Roberts baadaye alihamia 'DARPA' (Deffence Advanced Research Projects Agency) mwaka 1966 na kukuza mradi mwingine ulioitwa 'ARPANET' (Advanced Research Projects Agency Network). Mtandao huu ulianza kutumika mwaka wa 1969. Inasemekana kuwa neno intaneti lilitokana na 'ARPANET'. Wakati huu, mtandao ulitumiwa na wajuzi wa tarakilishi, wahandisi, wanasayansi na wasimamizi wa maktaba. Miaka hii ya 60 na 70, wasomi waliibuka na tafiti mbalimbali zilizopelekea kuibuka kwa mitandao mitatu, nayo ni, 'ARPANET, Telenet na X.25 Protocols'. Wataalamu hawa ni kama vile, Vinton Cerf, Donald Davies, Paul Baran na Leonard Klein (Ruggiero, 2000).

Mwaka 1972, matumizi ya barua pepe yalianzishwa na mtaalamu Ray Tomlison, ambaye aliibua ishara @ iliyotumiwa kuunganisha jina la mtumizi (Username) na anwani yake (Address). Miaka ya 80, mtandao ulifanywa chombo cha biashara na sasa kukawa na ubinafsishaji. Kufikia 1990, matumizi ya mtandao yalianza kupanuka na athari zake zilianza kudhihirika kitamaduni na kibiashara. Wakati huu kulikuwa na matumizi ya barua pepe, matini za majadiliano na mtandao wa ulimwengu nzima. Mitandao ya kwanza kutumika Afrika miaka ya tisini ilikuwa 'X.25 IPSS' na '2400 Daud Madem', iliyotumiwa kuunganisha tarakilishi za kimataifa ili kurahisisha mawasiliano. Huduma za mtandao ziliwezeshwa kupitia satalaiti kule Uganda na mashirika ya 'Infor Communication na Clear Channel'.

Mwaka 1996, shirika lisilo la kiserikali la USAID ( United States Agency for International Development) lilianzisha mradi ulioitwa 'Leland'. Mradi huu ulishughulika na kuunganishwa kwa mtandao katika bara la Afrika. Nchi zilizounganishwa kwa mtandao huu ni Guinea, Mozambique, Madagascar na Rwanda. Nchi zingine mbili zilizounganishwa na baadaye mwaka 1998 ni, Cote d' Ivoire na Benin (Ruggierro, 2000). Hata hivyo, Afrika inajizatiti kuhakikisha kuwa mtandao umeenea barani. Hivyo, kumeanzishwa mradi unaoitwa 'AfriNIC' ambao makao yake ni kule Mauritius. Jukumu lake ni kusimamia anwani za 'IP' na kuzisambaza barani. Baadhi ya injini pekuzi zilizoibuliwa miaka ya tisini ni kama vile, Lycos, Yahoo, Alta-Vista na Google.

Historia hii itachangia pakubwa utafiti huu kwa sababu ilijaribu kueleza lengo la wasomi wa jadi la kukuza utumizi zaidi wa mtandao. Mtandao wakati huo ulitumika sana katika masuala ya kisayansi. Maprofesa wa vyuo vikuu ndio waliohusika sana kuhakikisha kuwa mtandao ulienea ulimwengu wote ili kuwawezesha kusambaza mawazo yao mbalimbali ya kitaalamu. Hata hivyo, historia hii ina mwanya kwa utafiti huu kwa sababu haijatoa ufafanuzi wa rasilimali zilizo katika mtandao na namna zilivyotumiwa na wanafunzi wa vyuo vikuu. Hivyo, mtafiti alinuia kuchunguza matumizi ya rasilimali za mtandao wa kiakademia miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu.

### 2.4 Rasilimali za mtandao wa kiakademia

Huduma za mtandao ni namna unavyoweza kutumia mtandao ili kutekeleza mambo fulani asemavyo Okinda (2007). Rasilimali za mtandao ni vifaa au mali katika mtandao zinazoweza kutumiwa ili kutekeleza mambo fulani. Mtandao una masuala ya kijamii, kielimu, kibiashara na kidini. Hivyo, mtandao una sifa za kipekee zinazouwezesha kuwa na huduma au rasilimali zake.

#### 2.4.1 Sifa za mtandao

Kuwepo kwa mtandao kunaashiria kuwa kuna sifa bainifu zinazouwezesha kutambuliwa nazo ni kama wanavyoeleza wataalamu wafuatao; Severin na Tankard (2001), wanasema kuwa, mtandao una sifa zifuatazo; Mahusiano, Umatinishaji na Wingi wa habari. Mahusiano kama sifa ya mtandao huifanya hadhira kuwa tendi na watumiaji hutawala mchakato wote wa mawasiliano na huweza kubadilisha majukumu yake. Watumiaji hutawala habari wanazopata kwa kutumia muda wanaotaka kuzichunguza na kuchagua watakazozitumia. Hivyo, ni kupitia sifa hii ambapo mtumizi anatawala mtandao na kuruhusiwa kufanya lolote. Wanafunzi wa vyuo vikuu huchukua fursa hii kutawala mtandao kwa aidha kusoma barua pepe ili kuwasiliana na wenzao au kupata habari zitakazowasaidia kufanya tafiti zao. Wanafunziwa Kiswahili wa vyuo vikuu watakuwa na nafasi ya kutawala rasilimali walizozipata katika mtandao kwa kuchagua data wanazozitaka ili kufanya utafiti.

Umatinishaji ni sifa inayomruhusu mtumiaji wa mtandao kubofya kurasa mbalimbali kama vile ule wa mfumo enezi wa habari (Severin & Tankard, 2001). Mtumiaji anaweza kuhamisha ukurasa mmoja hadi mahali pengine au mfumo enezi mwingine. Sifa hii ni muhimu kwa

mwanafunzi anayetaka kupata habari nyingi kutoka kwa kurasa tofauti. Mwanafunzi hupata fursa ya kukusanya data pamoja na kisha kuzichanganua na maelezo kamili kutolewa. Wanafunzi wa Kiswahili wataweza kutalii sehemu mbalimbali katika mtandao ili kutambua rasilimali mbalimbali zitakazowawezesha kufanya tafiti zao.

Mwisho, mtandao humwezesha mtumiaji wake kupata mchanganyiko wa huduma za kuwepo kwa matini, picha, sauti, video na vibonzo (Severin & Tankard 2001). Kwa sasa mfumo enezi wa habari umezinduliwa kushughulikia usikilizaji na kuona video moja kwa moja kupitia wavuti. Wanafunzi wanaweza kufaidika kwa sababu wanaweza kusikiza yanayoendelea katika semina kadhaa katika sehemu mbalimbali za kitaifa na kimataifa. Sifa hii ni muhimu kwa sababu mwanafunzi anaweza kupata habari anazohitaji aidha kwa kuona picha au video na kusikiliza. Mambo haya yanaweza kufanywa kwa wakati mmoja yaani unaweza kusikiza huku ukiwa na matini na pia kuona picha au video. Wanafunzi wa vyuo vikuu watafaidika ikiwa watapata habari hizo kwa picha au video kwa sababu itarahisisha uelewa wao na hivyo kuandika tafiti zilizokomaa.

Sifa zingine za mtandao ni kuwa, huweza kuwafikia watu wengi katika masafa marefu. mtandao una habari nyingi zisizohesabika na zilizo na umuhimu. Urefu wake hauwezi kupimika. mtandao huruhusu mawasiliano kwa hadhira yaliyo na habari nzito. Ni kupitia habari hizi ndipo tutazingatia ni huduma zipi za mtandao zinazowafaa watumiaji wake. Wanafunzi wa Kiswahili katika vyuo vikuu watatoshelezwa pakubwa hasa kwa kupata habari nyingi na haraka ili kufanya tafiti zaidi. Hili litakuza tafiti zao za Kiswahili kwa upana sana.

Mtandao una sifa zinazowafanya wanafunzi wa vyuo vikuu kuutumia sana ili kufanya kazi zao mbalimbali. Bashir, Mahmood & Shafique (2001) walifanya utafiti wao wa matumizi ya mtandao miongoni mwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Punjab ambapo walitambua kuwa, mtandao ulikuwa na sifa zilizowawezesha wanafunzi hawa kuutumia sana. Asilimia 44 walisema kuwa mtandao ulirahisisha kazi, asilimia 43 uliokoa wakati, asilimia 35 una vifaa vya utafutaji, asilimia 15 huwa na habari zilizokubalika, asilimia 10 habari bora, habari zinapatikana wakati wowote, uliimarisha ujuzi, waliburudika, kupata ujuzi wa hali ya juu,walifanya tafiti na walipata huduma za barua pepe. Hivyo utafiti huu una mchango mkubwa kwani ulisaidia kujua umuhimu wa matumizi ya rasilimali za mtandao za kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili.

Kuwepo kwa sifa hizi ni dhihirisho la kutosha kuwa rasilimali au huduma zipo katika mtandao. Okinda (2007) anaeleza kuwa, huduma za mtandao ni kama vile, barua pepe, mfumo enezi wa habari, uhamishaji wa mafaili, makundi ya habari, uandishi wa ujumbe wa papo hapo na orodha ya barua pepe. Huduma hizi zinahusiana na habari, mawasiliano na uhamishaji wa data. Kama anavyoeleza Okinda (2007) ili wanafunzi watumie mtandao, lazima waelewe au wajue namna ya kutumia huduma na rasilimali zake. Huduma za mtandao zinaweza kugawanywa kutegemea mambo matatu muhimu nayo ni; habari, mawasiliano na uhamishaji wa data. Hivyo, wanafunzi wa Kiswahili watapaswa kuwa na uelewa wa huduma za Mtandao na namna ya kuzitumia. Hili litasaidia katika kurahisisha kazi zao hasa wakati wa kufanya utafiti.

Mawasiliano ndiyo lengo kuu la wengi wa watumiaji wa mtandao. Huduma za barua pepe zinatumiwa sana na watu. Mtumiaji wa mtandao anaweza kutuma na kupokea ujumbe kupitia barua pepe. Mtumiaji anaweza kutuma ujumbe pamoja na picha, makala au mafaili kadhaa. Barua pepe zinaweza kutumwa kwa watu wengi wakati mmoja. Wanafunzi wa vyuo vikuu wanatumia sana barua pepe (Luambano & Nawe, 2004). Barua pepe hizi zinaweza kutumiwa kupata habari kutoka kwa watu mbalimbali kwa mfano, wanafunzi wa Kiswahili wanaweza kupata data ya utafiti anaofanya kutoka kwa wanafunzi wenzao kutoka maeneo mengine. Hili litasaidia kukuza tafiti zao.

Uhamishaji wa data pia huwa huduma inayowezesha mtumiaji wa mtandao kupata anachotaka. Mafaili huweza kutumwa kwa marafiki, vyuo na wateja. Vyombo vya habari kama vile runinga na redio huunganishwa kupitia mtandao. Mtumiaji anaweza kusikiliza redio au kutazama runinga ikiwa mtandao wake ni mzuri. Kamera zinaweza kuunganishwa kwa tarakilishi ambapo itamwezesha mtumiaji kutazama kwa mfano wanyama wa Afrika karibu na mito, meli katika kanali ya panama na msongamano wa magari karibu na mji ulio karibu (Okinda, 2007). Huduma ya *YouTube* ilianzishwa Februari 2005 ambapo mafaili ya video yalionyeshwa bila kipimo. Hivyo ni mojawapo wa rasilimali katika mtandao ambayo inaweza kutumiwa na wanafunzi wa Kiswahili wa vyuo vikuu ili kutosheleza mahitaji yao mbalimbali.

Mojawapo wa huduma za mtandao ni mfumo enezi wa habari. Ni katika kurasa hizi ambapo tunapata makala mbalimbali yanayowafaa wengi katika taaluma zao mbalimbali. Huduma za mfumo enezi wa habari ni kama vile, *Microsoft Internet Explorer*, *Mozilla Firefox*, *Opera*,

*Apple's Safari, Google Chrome* na kadhalika. Huduma hizi huwaruhusu watumiaji wake kutalii ukurasa mmoja hadi mwingine (Okinda, 2007). Hivyo, wanafunzi wa Kiswahili watautumia mfumo enezi wa habari kwa sababu uliwaruhusu kutalii popote pale mradi wapate habari wanazohitaji kufanya tafiti zao. Katika kupata habari, huduma zingine zilizopo zinazotokana na injini pekuzi kama vile, *Yahoo*, *Google*, *Infor*. Huduma hizi huwawezesha watu na makampuni kusambaza habari na maoni yao kwa hadhira kubwa. Huduma zingine ni kama, *Angel fire*, *Geocities*, *Facebook na My Space.*

Lugha inayotumiwa kwa wingi katika mtandao ni ya kimataifa yaani Kiingereza. Korpela (2014) Alitafiti kuhusu matumizi ya Kiingereza katika mtandao. Anasema kuwa Kiingereza ni lugha kuu inayotumiwa sana katika mtandao. Mtumiaji wa mtandao ataweza kuutumia mtandao ikiwa ana uelewa wa lugha ya Kiingereza. Uelewa uhusishe kuandika na kusoma kazi zilizoandikwa katika lugha ya Kiingereza. Hivyo, ni muhimu kujua lugha ya Kiingereza ili utumie vyema rasilimali za mtandao. Wengi wa watu ulimwenguni wanaelewa lugha ya Kiingereza, hivyo ni huduma inayowawezesha wengi wa watu kuwasiliana, kupata habari na kueleza hisia na fikira zao. Baadhi ya lugha zilizopendekezwa kutumiwa katika mtandao ni Kichina (asilimia 23), Kiispania (asilimia 8) Kijerumani (asilimia 5) Kireno na Kijapani (asilimia 3 kila moja).

Kwa sasa lugha hizi zina watumiaji wengi katika mtandao. Katika orodha hii lugha ya Kiswahili haipo hivyo, kuna uhitaji wa wasomi wa Kiswahili kusisitiza matumizi ya lugha hii kwani hivi sasa inaanza kutambulika kama lugha ya mawasiliano mapana. Wanafunzi wa Kiswahili watapata habari kwa kutumia lugha ya Kiingereza kisha kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili. Hii ilikuwa changamoto kwao kwa sababu walipata ugumu kutafsiri tafiti za watu wengine. Hata hivyo baadhi ya habari zinapatikana katika lugha ya Kiswahili.

Rasilimali za mtandao kama anavyoeleza Okinda (2007) ni makala yoyote yaliyomo au yanayo-patikana katika mtandao kwa mfano majarida, magazeti, vitabu na kadhalika. Rasilimali katika mtandao zimewanufaisha watu kwa sababu hakuna mzigo unaohitajika kubebwa. Mtandao hutuwezesha kutuma makala marefu kwa muda mfupi bila kuyabeba kama mzigo kutoka tarakilishi moja hadi nyingine. Wanafunzi wa vyuo vikuu wanaweza kupata habari nyingi kutoka kwa majarida na magazeti kwa muda mfupi hivyo wamerahisishiwa kazi ya kubeba vitabu ili kuvisoma.

Baadhi ya rasilimali katika lugha ya Kiingereza zinazoweza kutumiwa na wanafunzi kufanya utafiti ni kama vile; 4000+ Research Paper Topic Ideas http://www.questia.com/library/research-topics/a, A Research Guide for students http://www.aresearchguide.com/, Citation machine http://www.citationmachine.net/index2.php, How to write a term paper http:/www.gale.cengage.com/fre resources/term paper/index.htm, Online Research tools http://www.OnlineResearchTools.infor/, Research Blogs and the Discussion of scholarly Information http://www.plosone.org/article/infor%3Adoi%2F10.1371%2Fjournal.pone.0035869, Searching the Internet http://www.SearchingTheInternet.infor/, Research Resources http://www.ReferenceResources.infor/, World Wide Web Resources http://www.WWW Reference.infor/,The Basic element of English http://www.ucalgary.ca/UOFC/eduweb/grammar, WebMATH http://www.webmath.com, Bartleby.comhttp://www.bartleby.com, The world Fact book-http://www.cia.gov/library/publications/the-world-fact-booknaLangenberg.com http://www.langenberg.com

Rasilimali za mtandao zilizotajwa hapo juu ni muhimu sana kwa mwanafunzi yeyote anayetaka kufanya tafiti. Rasilimali hizi zinaweza kutumiwa na wanafunzi wa Kiswahili lakini watahitajika kutafsiri kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili. Baadhi ya kazi za Kiswahili zinapatikana katika makala yaliyoandikwa kwa Kiingereza. Hili litamtaka mwanafunzi wa Kiswahili awe na ujuzi wa hali ya juu wa kusoma kazi hizi ili aeleze kazi yake vizuri. Hali hii imepelekea mtafiti kutambua rasilimali za Kiswahili katika mtandao ili kumsaidia mwanafunzi wa Kiswahili kuzifikia kwa haraka na kufanya kazi za kisasa na zilizokua kitaaluma.

Nazaryan & Gridchin (2006) wanasema kuwa kuna matini katika mtandao kama vile maandishi ya kiakademia na habari kutoka vyombo vya habari. Matumizi katika mtandao hasa ni mazungumzo kupitia mtandao ingawa analalamika kuwa katika mazungumzo haya wakati mwingine sarufi haizingatiwi, pia kuna makosa ya hijai na kazi kutohaririwa. Anamtaja Crystal (2001) ambaye alisema kuwa mawasiliano katika mtandao si sanifu, hayafuati sheria za kisarufi, yana makosa ya hijai na yana maneno mapya. Anasisitiza utafiti ufanywe kuhusu muundo na ukuzaji wa lugha katika mtandao.

Vyombo muhimu katika elimu ni mawasiliano, rasilimali, tarakilishi na mtandao (Sahin, Balta & Ercan, 2010). Wanaendelea kusema kuwa, wengi wa wanafunzi na wataalamu hutumia mtandao

kufanya utafiti wa kisayansi na kutayarisha miradi kwa sababu ni rahisi kutumia, ni haraka na si njia ghali ya kupata habari Sahin, Balta & Ercan (2010). Miongoni mwa rasilimali wanazotaja ni kama vile, majarida ambayo huwa na habari na hutumiwa na wanafunzi na wasomi wengi. Injini pekuzi hutumiwa na wanafunzi kukusanya habari zinazotumiwa kwa miradi yao. Maktaba za mtandao pia ni rasilimali nyingine. Maktaba hizi huwa wazi au funge kwa watumiaji wake. Rasilimali za vyuo vikuu katika maktaba hizi kama vile majarida na vitabu huwa funge. Hivyo, ni muhimu sana kwa wanafunzi wa vyuo vikuu kuzitumia kwa sababu ubora wake ni wa hali ya juu. Hata hivyo, nyingi ya mada zilizo katika injini pekuzi zimeandikwa katika blogu na majarida mbalimbali.

Miongoni mwa rasilimali za Kiswahili zinazopatikana katika mtandao zinahusu; kamusi za Kiswahili, makala ya fasihi, makala kuhusu lugha na masuala ya kitamaduni. Kuna baadhi ya magazeti ya Tanzania na Kenya kwenye mtandao. Vyombo vya habari kama vile redio au runinga pia vipo kwa mfano nchini Kenya kuna runinga za Citizen, Nation, KTN miongoni mwa nyingine. Katika mataifa ya nje kwa mfano, kuna redio ya Ujerumani ya 'Deutche Welle' ambayo ina vipindi kama vile taarifa ya habari, matukio, kipindi cha Afrika magazetini, orodha ya vipindi, jinsi ya kupokea matangazo. Wanafunzi wa vyuo vikuu wana rasilimali nyingi sana ambamo mna habari wanazoweza kupata ili kufanya tafiti zao. Rasilimali hizi zimewafaa sana wanafunzi wa isimu, lugha na fasihi wa vyuo vikuu vya nje kwa sababu wanazitumia kufanya tafiti zao mbalimbali.

### 2.5 Matumizi ya rasilimali za mtandao na wanafunzi wa vyuo vikuu

Wanafunzi wa vyuo wanapaswa kujua yaliyomo katika mtandao ili waweze kuutumia kutosheleza mahitaji yao ya kielimu na kijamii. Yaliyomo ni kama vile rasilimali za mtandao ambazo wanafunzi wanaweza kuzitumia kupata habari za kukidhi mahitaji yao ya kielimu. Hivyo, sehemu hii ilieleza ufahamu na matumizi ya rasilimali za mtandao na wanafunzi wa vyuo vikuu mbalimbali kama walivyotafitia wataalamu mbalimbali.

### 2.5.1 Ufahamu wa rasilimali za mtandao na wanafunzi wa vyuo vikuu

Ufahamu wa rasilimali za mtandao ni kuwa na maarifa kuhusu mambo. Ufahamu wa rasilimali za mtandao ni muhimu kwa mtumiaji yeyote wa mtandao. Ufahamu wa rasilimali za mtandao umeweza kutafitiwa na wataalamu mbalimbali katika vyuo mbalimbali vya ulimwengu. Hivyo, maelezo yatatolewa kwa kuzingatia vyuo vya kimataifa, vya kiafrika na vyuo nchini Kenya.

Baadhi ya wanafunzi wa vyuo vikuu vya kimataifa wana ufahamu wa mtandao, rasilimali zake na huduma zake. Shailendra, Lailai, Poh, Soh & Wong (1995) walitafiti kuhusu ufahamu wa rasilimali za mtandao miongoni mwa wanafunzi wa shahada ya kwanza na kutambua kuwa asilimia 78 walizifahamu. Adithya, Mahadevamurthy & Hydarali (2003) walipata kuwa wanafunzi waliofuzu wa Taasisi ya masomo ya usimamizi ya Vidya Vikas ambapo walipata kuwa wanafunzi wote 78 (Asilimia 100) walifahamu rasilimali za mtandao. Kwa hivyo, ni muhimu wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno kuzijua rasilimali za Kiswahili za mtandao ili kuzitumia katika kozi zao kukuza tafiti zao. Utafiti huu ulichunguza wanafunzi wa shahada ya kwanza.

Wanafunzi wa vyuo vikuu Afrika walikuwa na ufahamu wa rasilimali za mtandao. Baadhi ya waandishi waliwachunguza wanafunzi waliofuzu kwa mfano Okite – Amughoro & Lefose (2014) ambapo walipata kuwa, walikuwa na ufahamu wa rasilimali za mtandao lakini hawakuzitumia kwa sababu ya kukosa ujuzi wa kuzitafuta. Chinwe (2010) alipofanya utafiti kuhusu matumizi ya TE(KNO)HAMA miongoni mwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Obafemi Awolowo ambapo asilimia 50.5 walifahamu rasilimali za mtandao ndiyo maana waliutumia mtandao kufanya utafiti. Hivyo, wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno wapaswa kufahamu rasilimali za mtandao wa kiakademia ili wautumie mtandao vyema.

Nchini Kenya wanafunzi wa vyuo vikuu hawajaachwa nyuma kwa kuzifahamu rasilimali za mtandao. Waithaka (2013) anasema kuwa wanafunzi wa Chuo kikuu cha Nairobi walizifahamu rasilimali za mtandao kwa kiwango cha juu katika maktaba. Hata hivyo, tovuti ya chuo kikuu ina makala ya matumizi ya mtandao miongoni mwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mt Kenya na GRETSA ambao hawakuwa na ufahamu wa rasilimali za kielektroniki za mtandao. Hivyo, ni wazi kuwa wengi wa wanafunzi wa vyuo vikuu wanazitumia rasilimali za mtandao kwa sababu

wana ufahamu wa rasilimali zilizomo. Utafiti huu hautazingatia rasilimali katika maktaba ya Chuo Kikuu cha Maseno bali rasilimali za Kiswahili zinazopatikana katika mtandao wa kiakademia.

### 2.5.2 Viwango vya matumizi ya rasilimali za mtandao na wanafunzi wa vyuo vikuu

Wengi wa wanafunzi wa vyuo vikuu hutumia mtandao kufanya utafiti au kupata habari zinazowakuza kitaaluma. Baadhi ya wataalamu wameeleza matumizi ya mtandao miongoni mwa wanafunzi. Stutzer (2010) anasema kuwa, mwanafunzi anapofika chuo kikuu anatarajiwa kuwa na ujuzi wa namna ya kuutumia mtandao. Ujuzi huu ulimsaidia kupata au kutafuta habari ambazo zilimfaa katika tafiti zake mbalimbali. Wanafunzi wa vyuo vikuu wanatarajiwa kuwa na ujuzi wa kutumia mtandao kwa sababu wanatarajiwa kuwa na nafasi nzuri ya kupata vifaa na huduma hizi. Hili lilipelekea mtafiti kuchunguza matumizi ya mtandao miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu hasa wa Kiswahili kwa kutumia Chuo Kikuu cha Maseno kama kigezo.

Luban (2000) alitafiti athari za mtandao kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Duke ambapo alipata kuwa, asilimia 79 walitumia mtandao katika maktaba na asilimia 8 waliutumia katika mikahawa iliyomo chuoni. Miongoni mwa rasilimali walizotumia wanafunzi hawa ni kama vile majarida asilimia 36.9, vitabu asilimia 24.1, makala yaliyoandikwa asilimia 9.9, utafiti asilimia 11.3, magazeti asilimia 14.9 na makala yasiyo kwa majarida asilimia 2.9. Maktaba za vyuo vikuu zinapaswa kuwa na tarakilishi zilizounganishwa na mtandao ili wanafunzi waweze kutumia mtandao. Hata hivyo, wanafunzi wanaoweza kununua tarakilishi za kibinafsi wazinunue ili wawe na muda wa kutosha kupata habari. Maktaba ya Chuo Kikuu cha Maseno ina tarakilishi na baadhi yazo zimeunganishwa na mtandao, hivyo wanafunzi wa Kiswahili wana nafasi nzuri ya kuutumia mtandao. Ni vyema ikiwa wanafunzi wa Kiswahili walitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao kufanya utafiti wao wa Kiswahili ili kuukuza.

Jones & Madden (2002) wanasema kuwa, utafiti wa kwanza wa mradi wa PEW kule Marekani ulibaini kuwa mwaka 2000, asilimia 64 ya wanafunzi waliutumia mtandao kudurusu Mtandao wa Ulimwengu Mzima. Mwaka wa 2002, asilimia 78 ya wanafunzi walitumia mitandao ya utafiti kufanya tafiti zao na kazi za ziada. Wengi wa wanafunzi waliwasiliana kupitia mtandao na

marafiki wenzao. Mwaka 2006, kulikuwa na ongezeko la matumizi ya mtandao miongoni mwa wanafunzi wa vyuo kufanya utafiti. Mwisho wa mwaka 2007, wanafunzi wa miaka kati ya 18 hadi 20 walitumia maabara kwa sababu kulikuwepo na tarakilishi zilizounganishwa kwenye Mtandao. Hivyo, matumzi ya mtandao miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu yanakadiriwa kuongezeka miaka ijayo kwa sababu utumizi wake kwenye vyuo vikuu ni wa haraka sana. Vyuo vingi vya kimataifa na kitaifa vinajitahidi kuhakikisha kuwa vimekua kiteknolojia hasa katika usambasaji wa habari, utoaji wa habari na utafiti katika vyuo vyao. Matarajio ni kuwa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno waliutumia mtandao kwa masuala ya kiakademia.

Malik & Mahmood (2009) walipofanya utafiti wa tabia za wanafunzi katika wavuti wa Chuo Kikuu cha Punjab, walipata kuwa wanafunzi waliutumia mtandao kupata habari. Asilimia 59.9 waliutumia wakiwa nyumbani, asilimia 25 wakiwa chuoni na asilimia 15 wakiwa nyumbani na chuoni. Injini pekuzi waliyotumia sana ni ya *Google* asilimia 97 ikifuatiwa na *Yahoo* asilimia 72. Matatizo yaliyowakumba wanafunzi hawa wakiutumia mtandao ni kujikokota kwa mtandao, habari nyingi kupita kiasi na zenye ubora wa chini sana. Wanafunzi wa vyuo vikuu wanapaswa kutumia mtandao kwa sababu ni muhimu kwa kupata habari zitakazotumika kufanya utafiti wowote ule. Haijalishi atautumia wapi mradi zinapatikana kwa urahisi bila kujikokota. Wanafunzi wazingatie injini pekuzi inayofaa ili kuepuka habari za kupotosha. Hivyo, utafiti huu ulisaidia wanafunzi kutambua rasilimali za Kiswahili kwa kulinganisha na zile alizozitaja.

Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sardar Patel hutumia sana mtandao (asilimia 52.86) kuliko maktaba. Injini pekuzi ya *Google* na *Yahoo* ndizo zinazotumiwa sana (Dave, 2012). Wanafunzi hawa hutumia mtandao kutuma au kupokea barua pepe, kuwasiliana kijamii, burudani na maongezi na marafiki. Kiakademia wao hutumia mtandao kufanya utafiti, kufikia majarida, kupata matini na majadiliano. Maeneo wanapopata huduma na rasilimali za mtandao ni mikahawa ya mitandao asilimia 47.17, nyumbani asilimia 37.14 na chuoni asilimia 15.72. Mikahawa ya mitandao iliyo nje na ndani ya vyuo vikuu vinapaswa kutoa huduma bora kwa watumiaji wake ambao ni wanafunzi kwa kuhakikisha kuwa wanawapa rasilimali na huduma za kutosha. Hivyo, wengi wa wanafunzi wa vyuo vikuu vya kimataifa wana ufahamu mtandao ndio maana wanautumia. Wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno wanapaswa kuwa na ufahamu wa rasilimali za Kiswahili za kiakademia ili wazitumie kufanya utafiti.

Osunade (2003) alifanya utafiti wa wanafunzi wa kiwango cha chuo cha kiufundi kule Nigeria ambapo alitathmini athari za kudurusu mtandao kwa matokeo ya mtihani ya wanafunzi. Alipata kuwa wanafunzi waliotumia mtandao na wale hawakuutumia walikuwa na matokeo tofauti katika mitihani. Wanafunzi wanaume walishiriki sana katika utafiti huo kuliko wa kike. Baadhi ya wanafunzi walikubali kuwa wao hutumia mtandao kufanya utafiti. Sababu za wao kuutumia mtandao ni kwanza, kutafuta maoni mbalimbali kuhusiana na kazi au tafiti zao. Pia waliutumia kujadiliana na wengine kupitia makundi mbalimbali katika mtandao na wahadhiri waliutumia kuaandaa makala ya wanafunzi. Wanafunzi wanaotumia mtandao huwa na matokeo ya juu katika mtihani tofauti na wale wasioutumia. Hivyo, ni muhimu kwa wanafunzi wa Kiswahili kutumia rasilimali za mtandao za Kiswahili ili kuwa na matokeo mazuri katika mitihani yao. Utafiti ulitaka kujua umuhimu wa rasilimali za Kiswahili za mtandao kwa utafiti wa Kiswahili.

Nchini Tanzania, katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wataalamu Luambano na Nawe (2004) wanatambua kuwa, wanafunzi hutumia mtandao katika masomo yao lakini wao hukumbwa na matatizo mbalimbali. Hata hivyo, wanaendelea kusema kuwa, wanafunzi hufaidika na mtandao kwa namna tofauti tofauti kwa mfano kupata habari, kueneza habari hizi kwa hadhira kubwa, kubadilishana maoni na kuimarisha mawasiliano baina ya wanafunzi na wahadhiri. Wengi wa wanafunzi walipata ujuzi wa kuutumia mtandao kutoka kwa marafiki asilimia 53.8, kibinafsi asilimia 37.5, maktaba asilimia 5 na wengine kwa kusoma kwa vitabu na kuhudhuria mihadhara ya kozi ya Habari na Teknolojia. Hivyo, ujuzi wa mtumiaji wa mtandao ni muhimu katika kuzifikia rasilimali za mtandao. Wanafunzi wa Kiswahili wanahitajika kuwa na ujuzi ili kuzitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia.

Tella (2007) katika utafiti wake wa wanafunzi 39 wa shahada ya kwanza wa Chuo Kikuu cha Botswana, alichunguza matumizi ya mtandao na athari zake kwa matokeo ya mtihani. Alipata kuwa, mtandao huwawezesha wanafunzi kupata habari na kuwasiliana na wengine. Mtandao uliboresha matokeo ya mitihani ya wanafunzi hawa. Mtafiti anaunga mkono utafiti huu kwani wanafunzi wa shahada ya kwanza wanahitaji habari nyingi na za kiakademia ili kuandika tafiti nzuri. Kuongezea, wataweza kusoma habari hizi na kufaidika sana wanapofanya mitihani yao. Hivyo, ni muhimu wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno kuzitumia rasilimali za Kiswahili ili kuboresha matokeo ya mitihani.

Wanafunzi wa shahada ya kwanza asilimia 92 wa Chuo Kikuu cha Obafemi Awolowo waliutumia mtandao (Awoleye, 2008). Wengi wa wanafunzi wa kiume hutumia mtandao kuliko wa kike. Wanafunzi hawa walikuwa na tajriba ya miaka minne katika matumizi ya mtandao. mtandao ulitumiwa kupata habari, kutuma barua pepe na kuzungumza mtandaoni na marafiki. Watu wengi katika mikahawa ya mtandao hutalii maeneo ya ponografia. Kama ilivyo kwa wanafunzi wa Kiswahili wa mwaka wa nne wa Chuo Kikuu cha Maseno, ni wazi kuwa wanafunzi wanapaswa kuwa na tajriba itakayowawezesha kuutumia mtandao. Tajriba hii itamsaidia mwanafunzi wa kiwango hiki kuudurusu mtandao kila mahali hivyo kupata data ya kutosha ya kumwezesha kufanya utafiti.

Llo & Ifijeh (2010) walisema kuwa, wanafunzi wa mwaka wa mwisho wa Chuo Kikuu cha Covenant ambapo walisema kuwa waliutumia mtandao kufanya utafiti wao. Wengi wa wanafunzi (asilimia 36.9) walitumia sana majarida kama rasilimali ya kupata habari zilizowawezesha kufanya utafiti wao. Waliweza kuzifikia rasilimali hizi kwenye maktaba chuoni (asilimia 52.7), mikahawa ya mitandao nje ya chuo (asilimia 25.3), mikahawa ya mitandao ndani ya chuo (asilimia 8). Hivyo, wengi wa wanafunzi walitumia maktaba ya chuo kuzifikia rasilimali za mtandao. Maktaba hizi zimeunganishwa kwenye mtandao ili kurahisisha upatikanaji wa rasilimali za mtandao wa kiakademia. *Google* (asilimia 40) ni injini pekuzi iliyotumiwa sana na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Covenant kupata huduma za mtandao ikifuatiwa na Yahoo (asilimia 28) na kisha nyingine. Wanasema kuwa mtafiti bora ni yule aliye na ujuzi wa kutumia mtandao ili asiweze kupoteza muda mwingi wakati anapotafuta habari fulani. Hivyo, ni muhimu kwa mtumiaji yeyote wa mtandao kuwa na ujuzi wa kutosha ili aweze kutimiza malengo yake ipasuavyo haswa wanafunzi wa vyuo vikuu.

Ani (2010) alitafiti upatikanaji na matumizi ya mtandao miongoni mwa wanafunzi wa shahada ya kwanza wa vyuo vya Calabar, Uyo Uyo na Rivers State. Anasema kuwa wengi wa wanafunzi katika vyuo hivi hutegemea mikahawa ya mitandao ya kibinafsi na umma kupata huduma za mtandao. Si rahisi wanafunzi hawa kuzifikia huduma za mtandao kwenye maktaba za vyuo, maeneo ya TE(KNO)HAMA, kwenye vitivo na idara kwani huduma hizo ni duni. Vyuo hivyo vilikuwa na miundo msingi duni na huduma ghushi za mtandao. Alipendekeza kuwa, kulikuwa na haja ya kutoa elimu kuhusu matumizi ya mtandao kwenye maktaba ya vyuo hivyo. Hivyo,

maktaba katika Chuo Kikuu cha Maseno inapaswa kuwa na tarakilishi zilizounganishwa katika mtandao ili kuwawezesha wanafunzi wa Kiswahili kuzipata na kuzitumia rasilimali za Kiswahili.

Bankole & Babalola (2012) katika utafiti wao wa matumizi ya mtandao miongoni mwa wanafunzi wa shahada ya kwanza wa Chuo Kikuu cha Olabisi Onabanjo nchini Nigeria, alipata kuwa asilimia 97.6 waliutumia mtandao na asilimia 2.4 hawakuutumia hasa kwa masuala ya kiakademia.  Sababu za kutotumia mtandao zilikuwa ni kuwa hawakuwa na ujuzi na hawakuwa na muda. Walipendekeza kuwa walihitaji mafunzo ya kutumia mtandao na chuo kiwape huduma za mtandao bila malipo. Asilimia 60.6 ya wanafunzi walitumia saa 1-5 katika mtandao kwa wiki, asilimia 23.8 saa 6-10 na asilimia 9.9 saa 10-15. Wanafunzi wahimizwe kuutumia mtandao kufanya utafiti au kwa shughuli nyingine tofauti. Wasiutumie mtandao kwa kukosa ujuzi kwani vyuo vikuu vinaweza kuandaa kozi zitakazowapa ujuzi wa kuutumia mtandao. Wanafunzi wa vyuo vikuu wakipewa mafunzo hawana budi kuutumia mtandao kufanya utafiti. Hivyo, ni vyema ikiwa wanafunzi wa Kiswahili wanapewa mafunzo ya kutumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na Chuo Kikuu cha Maseno ili waweze kutambua rasilimali za Kiswahili za mtandao.

Mambo waliyofanya wanafunzi wakiwa katika mtandao ni kama vile, mawasiliano asilimia 90.6, kufanya kazi za ziada asilimia 43.5, kujua yanayoendelea asilimia 32.9, kuongeza habari zaidi za makala ya mihadhara asilimia 26.7, kufanya utafiti asilimia 17.2 na burudani asilimia 11.9. Vyombo vilivyotumiwa katika mtandao vilivyotumiwa na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Olabisi Onabanjo kule Nigeria ni barua pepe asilimia 87.0, *WWW* asilimia 85.1 na kupiga gumzo asilimia 40.8. Injini pekuzi ya *Google* ndiyo iliyotumiwa sana na wanafunzi hawa. Ujuzi wa kuutumia mtandao ulitokana na juhudi za kibinafsi na usaidizi wa marafiki. Ni wazi kuwa wanafunzi wa chuo hiki hawazingatii sana utumizi wa mtandao kufanya utafiti. Hivyo, mtafiti alitaka kutambua ikiwa wanafunzi wa Kiswahili hutumia mtandao wa kiakademia kufanya utafiti wa Kiswahili.

Fasae & Aladeniyi (2012) walifanya utafiti kuhusu matumizi ya mtandao miongoni mwa wanafunzi wa kitivo cha sayansi vyuo vya Fideral na Adekunle Ajasin ambapo walipata kuwa, asilimia 89 ya wanafunzi waliohojiwa walitumia mtandao kupata habari. Asilimia 99 walitumia Mtandao wa Ulimwengu Mzima na waliipata huduma hii kwenye mikahawa ya mtandao nje ya

vyuo. Matumizi ya mtandao yamewakuza wanafunzi hawa kitaaluma na kiakademia. Asilimia kubwa ya wanafunzi (Asilimia 65) katika vyuo hivi, walikuwa na tajriba ya kutumia mtandao zaidi ya miaka mitatu hivyo wengi waliutumia mtandao mara mbili tatu kwa wiki (Asilimia 44). Wanafunzi 176 (Asilimia 83) waliutumia rasilimali ya mtandao ya majarida ikilinganishwa na vitabu (asilimia 45). Hivyo, wengi wa wanafunzi katika kitivo cha Sayansi hawakutumia vitabu ipasuavyo. Hii ndiyo maana walitumia sana huduma ya barua pepe (Asilimia 100), Mtandao wa Ulimwengu Mzima (Asilimia 87) na injini pekuzi (Asilimia 58). Utafiti huu utachunguza matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi kutoka shule ya sana na sayansi jamii.

Wakati huu wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia, matumizi ya mtandao yamekuwa mambo ya kawaida. Nchi zinazoendelea kama Kenya hazijaachwa nyuma katika maendeleo haya. Hali hii imepelekea baadhi ya wataalamu kuchunguza namna mtandao unavyotumiwa hasa na wanafunzi wa vyuo vikuu kwa sababu kuna hisia kuwa wao ndio wanaoutumia sana ilikinganishwa na watu wengine nchini hasa kwa masuala mbalimbali. Kenya imekua sana kuhusiana na matumizi ya mtandao. Waithaka (2013) anasema kuwa, Kenya imeorodheshwa nambari tano dhidi ya nchi kumi barani Afrika kwa matumizi ya mtandao miongoni mwa watu. Hata hivyo, Afrika Mashariki Kenya inaongoza kwa watumiaji wa mtandao (Kenya ICT Stratedgy 2006).

Nyamboga & Ongondo (2004) walitafiti kuhusu tajriba ya wanafunzi, wanaofanya kazi katika maktaba na wanaofanya kazi kwenye vitivo mbalimbali vya Chuo Kikuu cha Egerton kwenye maktaba wanapotumia mtandao. Wengi wa waliohojiwa walisema kuwa hajafundishwa kuhusu namna ya kuutumia mtandao. Wanafunzi wa kiume ndio walioutumia sana mtandao ikilinganishwa na wa kike. Injini pekuzi na barua pepe ndizo zilizotumiwa sana mingoni mwa waliohojiwa. Hivyo, ni wazi kuwa matumizi ya mtandao katika Chuo Kikuu cha Egerton yanaendelea hata ingawa wengi wa wanafunzi na wanaofanya kazi katika idara mbalimbali hawana ujuzi wa hali ya juu. Hivyo, mafunzo zaidi kuhusu matumizi ya rasilimali za mtandao wa kiakademia yanapaswa kutolewa kwa wanafunzi wa vyuo vikuu.

Okinda (2007) alifanya utafiti wa wanafunzi 294 wa chuo cha mafunzo cha elimu ya kitaaluma nchini Kenya kwa kuchunguza matumizi na utoshelezi wa mtandao. Alisema kuwa wanafunzi wa chuo hiki waliutumia mtandao kwa mawasiliano, kupata habari, kuhusiana na wengine na

burudani. Huduma za mtandao zilizotumiwa sana na wanafunzi wa chuo hiki ni barua pepe na mtandao wa ulimwengu mzima. Utambuzi wake ni sawa na wa utafiti huu kwa sababu baadhi ya wanafunzi waliohojiwa walidai kuwa wahadhiri walikuwa na mchango mdogo katika kuwahimiza wautumie mtandao. Ni muhimu wanafunzi wa Kisdwahili wa Chuo Kikuu cha Maseno waelekezwe na wahadhiri wao katika kutambua rasilimali za Kiswahili za mtandao.

Nchini Kenya wanafunzi wa vyuo vikuu vya kibinafsi na vya umma hutumia mtandao kwa ushirikiano na baadhi ya mashirika yanayosaidia katika kusambaza huduma, rasilimali na miundo misingi ya mtandao. Nchi ya Kenya ina sera zifuatazo kuhusu TE(KNO)HAMA (Farrell, 2007), kuendeleza ukuzaji wa rasilimali za mtandao, kuibua rasilimali ili kusaidia ujifunzaji wa kielektroniki, kuendeleza ukuzaji wa ujifunzaji wa mtaala wa kielektroniki ili kusaidia elimu ya Teknohama, kuendeleza masomo ya mbali, kutoa muuundo msingi usio ghali ili kurahisisha usambazaji wa elimu na ujuzi kupitia ujifunzaji wa kielektroniki, kurahisisha ushirikiano wa rasilimali za mtandao kati ya taasisi mbalimbali na kuunganisha rasilimali za mtandao na rasilimali zingine zilizopo.

Hivyo, nchi ya Kenya inajizatiti kuhakikisha kuwa matumizi ya TE(KNO)HAMA yamezingatiwa katika nyanja zote za kielimu. Ni mwanzo mzuri hasa kwa sababu kuna sera zilizoundwa. Sera hizi zinapaswa kufuatwa na washikadau wahakikishe kuwa zinatimizwa. Haya yatatendeka ikiwa watu wote yaani, serikali, mashirika na washikadau watashirikiana pamoja kutimiza malengo haya. Mojawapo wa mashirika yanayosaidia kuendeleza matumizi ya mtandao ni KENET (Shirika la Mtandao Kenya) (Farrel, 2007). Lengo kuu la shirika hili ni kuimarisha na kuhifadhi mawasiliano miongoni mwa taasisi za kielimu nchini Kenya ambazo zitaendeleza matumizi makubwa ya teknolojia ya mtandao katika kufunza, utafiti na ushirikiano wa habari za rasilimali kwa watu wote kwa gharama isiyo ghali. Hivyo, ni muhimu kwa shirika hili kuhakikisha kuwa huduma zake zinawafikia wanafunzi wa vyuo vikuu wakiwemo wa Chuo Kikuu cha Maseno.

Shirika la KENET lilianzishwa kwa madhumuni yafuatayo; Kuimarisha muundo msingi wa mtandao, kutolewa kwa bei rahisi ya huduma na rasilimali za mtandao, kukuza watu walio na habari kuhusu, maendelezo ya yaliyomo, usimamizi wa habari na mawasiliano ya kiteknolojia ili kusaidia kufanya kazi na kusimamia KENET na kukuza na kustawisha yaliyomo nchini. Shirika

la KENET linapaswa kuhakikisha kuwa wanafunzi wana ujuzi wa kiteknolojia katika elimu yao. KENET kutoa vifaa vya kiteknolojia kwa vyuo vikuu nchini Kenya kutasaidia sana kusambaza matumizi zaidi ya Mtandao miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu. Hivyo, mafunzo ya kiteknolojia yatolewe na KENET ili kuwasaidia wanafunzi wa vyuo vikuu kuutumia mtandao.

Wanachama wanafaidika kwa bei ya chini ya kuunganisha mtandao, kusaidiwa katika uundaji wa vyombo vya mtandao na kuwafunza wafanyakazi. Shibanda (2006) anataja wanachama wa KENET wakiwa 26 kutoka vyuo vya umma na vya kibinafsi, Vyuo vya kiufundi vya umma na taasisi nyingine za kielimu. Kuna vyuo vikuu vya Moi, Methodist, Daystar, Kenyatta, Egerton, Jomo Kenyatta, Masinde Muliro miongoni mwa vyuo vingine. Kwa sababu KENET imeeneza huduma zake hivyo kuwepo na TE(KNO)HAMA nchini Kenya kutarahisisha mambo. Hivyo, ni muhimu kwa Chuo Kikuu cha Maseno kujihusisha na shirika hili ili wanafunzi wa Kiswahili wafaidike kwa kupata huduma za mtandao kwa bei rahisi. Hili litasaidia wanafunzi hawa kuzipata na kuzitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia.

Baadhi ya changamoto zinazokumba vyuo vikuu kuhusiana na kuwepo kwa TE(KNO)HAMA ni vyuo vikuu vingi havina sera na mikakati ya kuimarisha TE(KNO)HAMA. Pili, vyuo vikuu vimeweka asilimia moja ya mapato yao kwa TE(KNO)HAMA na vinaona ugumu kudumisha muundo msingi wa TE(KNO)HAMA kwa sababu ya gharama. Mwisho, vyuo vimeshindwa kutoa huduma za Teknohama darasani au kuweka tarakilishi katika ofisi za vitivo (Rodriques, 2008). Haya ni tofauti katika Chuo Kikuu cha Maseno kwa sababu usimamizi wa chuo hiki umejizatiti kuunganisha Mtandao katika ofisi za idara na vitivo. Hata hivyo, vyuo vikuu vijisatiti kuwa na sera au mikakati ya kuimarisha TE(KNO)HAMA. Asilimia kubwa ya mapato ya vyuo iekezwe kwa TE(KNO)HAMA ili kurahisisha matumizi ya teknolojia vyuoni.

Haya ni maoni sawa na yale ya Shabaya (2009) aliposema kuwa, shirika la KENET lililofanya utafiti mwaka 2006 kuhusu matayarisho ya vyuo vikuu kujihusisha katika ulimwengu ulioounganishwa katika utafiti na usimamizi kuhusu TE(KNO)HAMA, lilitambua kuwa, zaidi ya asilimia 50 ya vyuo hivi na vya kiufundi havikuwa na TE(KNO)HAMA ya kutosha kusaidia katika utafiti. Mwaka 2007, KENET pamoja na serikali zilianzisha mradi wa kuunganisha zaidi ya vyuo 40 vya elimu ya juu kwa mtandao mmoja. Madhumuni yakiwa ni kutilia nguvu ujifunzaji wa mtandao kwa kutumia wavuti, majarida, blogu na machapisho. Mradi huu

unapaswa kuenezwa katika vyuo vilivyobakia na ukamilishwe kwani utasaidia katika kueneza habari vyuoni. Wanafunzi wengi wa Kiswahili watafaidika kwa kupata habari kutoka vyuo vingine.

Vyuo vya Kenyatta na Baraton, vikiwa vyuo vilivyo na uanachama na KENET, vinatofautiana katika matumizi ya rasilimali za mtandao katika maktaba husika. Oyieke (2008) alifanya utafiti kuhusu matumizi ya teknolojia katika ufundishaji na ujifunzaji. Alitambua kuwa, kulikuwa na tofauti ya matumizi ya rasilimali za mtandao. Asilimia 60.4 ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Baraton walitumia rasilimali za mtandao na Chuo Kikuu cha Kenyatta ni asilimia 27.7. Wengi wa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kenyatta hawakufaidika na matumizi ya rasilimali katika maktaba zao ilhali wale wa Baraton walifaidika pakubwa. Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kenyatta hawana ujuzi wa kutumia rasilimali za mtandao na wale wa Chuo Kikuu cha Baraton wana ujuzi wa kutosha. Hivyo, ni muhimu kwa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno kufahamishwa kuhusu kuwepo kwa rasilimali za mtandao wa kiakademia katika chuo ili wawe na habari na waelezwe na wahadhiri wao kuhusu umuhimu wa matumzi yake.

Rasilimali nyingi katika vyuo hivi ni msaada kutoka kwa mashirika kama KENET na PERI. Nazo ni majarida, vitabu, sidii, vifaa vya kusikiliza, mtandao na Mtandao wa Ulimwengu Mzima. Wanafunzi na wasimamizi wa maktaba walikubaliana kuwa, rasilimali muhimu katika maktaba zao ni majarida (asilimia 73.9), vitabu (asilimia 54.5), rasilimali za mtandao (asilimia 69.6) na kanda za kunasa sauti na video (asilimia 47.6). Vyuo vikuu vinapaswa kujisatiti kuongeza rasilimali zaidi katika tarakilishi zao ili kukuza tafiti za wanafunzi wao. Hivyo, shirika hili lijaribu kuibua rasilimali za Kiswahili za mtandao na shirika hili lihusishe vyuo vyote ili wanafunzi wa Kiswahili wafaidike na huduma zao za mtandao.

Nchini Kenya, baadhi ya wanafunzi hutumia mtandao katika kufanya tafiti na wengine huutumia kwa njia ya kujiburudisha kupitia kurasa za mahusiano. Oduor (2010) anasema kuwa, baadhi ya wanafunzi wanautumia vibaya kwa sababu wanapopewa kazi kufanya wao huchukua tafiti za watu na kuzinakili moja kwa moja bila kuwatambulisha. Kutokana na wavuti wa Chuo Kikuu cha Nairobi wa Habari na Mawasiliano, utafiti ulifanywa kuhusu matumizi na utoshelezi wa mtandao wa wanafunzi wa vyuo vikuu vya Mount Kenya na GRETSA. King’ori (2010) aliwahoji wanafunzi 100 kutoka idara tofauti ambapo alipata kuwa, wanafunzi waliutumia

mtandao kwa mawasiliano, kupata habari ambazo hazipo katika maktaba, kutafuta kazi na kukusanya makala ya kiakademia. Miongoni mwa matatizo ni kama vile kukosa ujuzi wa kuutumia mtandao, uhaba wa tarakilishi zilizo na mtandao, kukosa kufahamu rasilimali za Mtandao, habari nyingi kupita kiasi na kukosa maelekezo kutoka kwa wahadhiri. Hivyo, utafiti huu utatoa mwelekeo katika kutambua matumizi na athari za matumizi za rasilimali za mtandao.

King'ori (2012) alifanya utafiti wake wa namna wanafunzi wa vyuo vikuu nchini Kenya wanavyotumia simu ya rununu ili kupata huduma za mtandao. Alipata kuwa wanafunzi wa vyuo vikuu hupata huduma za mtandao kupitia simu ya rununu kupata habari. Ni muhimu ikiwa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno watautumia mtandao kupata habari hasa huduma ya WI FI.

Waithaka (2013) alitafiti kuhusu matumizi ya mtandao miongoni mwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Nairobi ambapo alitambua kuwa wengi wa wanafunzi waliutumia Mtandao kwa mawasiliano (Asilimia 50.8), utafiti (Asilimia 48.5), kufundisha (Asilimia 38.6), burudani (Asilimia 16.7) kujifunza (Asilimia 15.9) na kusoma wavuti (Asilimia 11). Wanafunzi hawa walikuwa na tajriba ya miaka 4 – 5 (Asilimia 43.3), 3 – 4 (Asilimia 37.9), 2 – 3(Asilimia 12.5) na 1- 2 (Asilimia 6.4). Wengi wa wanafunzi walitumia injini pekuzi ya Yahoo (Asilimia 73), Google (Asilimia 8) na zingine ambazo zilitumiwa kwa uchache. Wengi waliweza kuzifikia huduma za Mtandao kwenye mikahawa ya mitandao (Asilimia 97.7), nyumbani (Asilimia 83.0) na maktaba (Asilimia 46.2). Hili ni kwa sababu maktaba ya Chuo Kikuu cha Nairobi ina huduma chache hivyo hawawezi kuzifikia wazitakapo. Hivyo mikahawa ya mitandao itafaa kutumiwa na wanafunzi wa Kiswahili ikiwa hawana tarakilishi za kibinafsi.

### 2.5.3 Umuhimu wa matumizi ya rasilimali za mtandao na wanafunzi wa vyuo vikuu

Matumizi ya mtandao yana majukumu makuu katika kuwasaidia watafiti wa shahada ya kwanza kuzifikia na kuzitumia rasilimali mbalimbali kutoka sehemu mbalimbali za dunia (Llo & Ifijeh, 2010). Mtandao ni mojawapo wa maendeleo ya kiteknolojia yaliyo na nguvu za kusababisha kuwepo kwa mawasiliano miongoni mwa wasomi watu mbalimbali wakiwemo wasomi. Mtandao unatumiwa kusambasa na kupata habari kutoka sehemu mbalimbali za ulimwengu (Waithaka, 2013).

Mtandao hutosheleza mahitaji ya habari na mawasiliano katika taasisi mbalimbali kwani kuna uwezekano wa kuzifikia habari nyingi kama ripoti za kiakademia kutoka sehemu yoyote ya dunia (Parameshwar & Patil, 2000). Mtandao unatumiwa na watafiti wa Chuo Kikuu cha Gulbarga India kufanya utafiti (Asilimia 76), masuala ya elimu (Asilimia 53), burudani (Asilimia 33) na mawasiliano (Asilimia 45) (Parameshwar & Patil, 2000). Hivyo, lengo kuu la watafiti hawa lilikuwa hasa kufanya utafiti kwa kuutumia mtandao. Wanafunzi wa vyuo vikuu wanaweza kuwekwa katika kundi hili la watafiti kwa sababu wamekuja vyuoni kusomea taaluma mbalimbali zinazohitaji kufanyiwa utafiti. Ni muhimu ikiwa wanautumia mtandao kufanya utafiti wao ili kuziboresha. Wanafunzi wa Kiswahili kama watafiti wengine walitarajiwa kuzitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia ili kutosheleza tafiti zao.

Jones & Madden (2002) walipofanya utafiti wa athari za mtandao kwa wanafunzi wa vyuo katika maisha yao ya kila siku, walitambua kuwa mtandao una jukumu kubwa sana katika sekta ya elimu. mtandao ulisaidia kukuza tajriba ya wanafunzi hawa walipokuwa chuoni na kufahamu mambo mengi. Pia wanafunzi waliweza kuwasiliana na wahadhiri wao, kufanya utafiti au shughuli za kielimu (Anunobi, 2006) na kuvifikia vifaa vya maktaba kupitia mtandao. Hivyo, ni muhimu kwa wanafunzi wa vyuo vikuu kusisitiza matumizi zaidi ya mtandao ili kukuza kozi zao. Ikiwa mtandao uliwawezesha wanafunzi kupata habari kutoka kwa maktaba mbalimbali basi tafiti zao zilikubalika kwani zilikuwa za kisasa.

Usun (2003) alifanya utafiti wa matumizi ya mtandao na wanafunzi wa idara ya tarakilishi shahada ya kwanza Chuo Kikuu cha Mart na kutambua kuwa, matumizi ya mtandao miongoni mwa wanafunzi ni ya kuvutia kwa sababu, huokoa wakati, huimarisha mahusiano ya kimataifa, hurahisisha ubadilishanaji wa maoni na kuimarisha utafiti. Wanafunzi wa vyuo vikuu wanapotumia mtandao wanaweza kuokoa wakati kwa sababu wanaweza kupata habari nyingi kwa wakati mmoja. Mahusiano yao na wahadhiri au wanafunzi wa vyuo vingine yanaweza kuimarishwa ili kukuza taaluma zao mbalimbali. Hivyo, wanafunzi wa Kiswahili wanahimizwa wazitumie rasilimali za mtandao wa kiakademia kwa sababu zitakuza utafiti wao wa kiakademia. Utafiti huu utachunguza wanafunzi kutoka idara ya Kiswahili.

Mtandao umekuza burudani. Hivi sasa ni nadra sana kwa watu kujumuika kwenye vyumba vya burudani ili kuona sinema. Sinema hizi zinaweza kutazamwa ikiwa tarakilishi imeunganishwa na

mtandao. Wanafunzi hutumia mtandao kuburudika kama anavyosema Anunobi (2006). Wanafunzi wa Kiswahili wanaweza kupata burudani kwa kutazama michezo ya kuigiza, fasihi simulizi na fasihi andishi. Baadhi ya bidhaa zinauzwa katika mtandao. Bei ya bidhaa hizi huwekwa kupitia tovuti zinazoorodhesha bidhaa hizo pamoja na bei yazo. Malipo huweza kufanywa kupitia mtandao halafu kisha baadaye ukatumiwa bidhaa hizo. Wanafunzi wa vyuo vikuu wanaweza kupata bidhaa kama vile vitabu na majarida ambayo wanaweza kuyanunua ili kusoma na kukuza tafiti zao.

Suhail & Bargees (2006) walifanya utafiti wa athari za matumizi ya mtandao na wanafunzi wa shahada ya kwanza kule Pakistan. Walitambua kuwa asilimia 84 walisema waliweza kuwasiliana na watu ulimwengu mzima. Asilimia 78 waliweza kupata alama nzuri katika mitihani yao, asilimia 74 waliweza kukuza usomaji na uandishi wa habari na kuwa na ujuzi wa kuchakata habari. Asilimia 48 walisema kuwa, mtandao uliwafanya kuwa wanafunzi wazuri kiakademia. Hivyo, wanafunzi wengi wa vyuo vikuu watapaswa kuutumia mtandao ili wawe na ustadi wa kutosha katika kusoma, kuandika na kufanya vizuri katika mitihani yao. Hivyo, mwanafunzi kuwa bora. Kwa sasa mtandao umefanya dunia kuwa katika chumba kimoja. Kila kitu kimo mikononi kuanzia habari, ununuzi wa bidhaa au vitu. Baadhi ya wataalamu wanasema kuwa mtandao umekuwa wa kutegemewa kwa sababu mambo mapya huzuka pale. Kwa mfano, maendeleo ya kiteknolojia katika taifa na mataifa mbalimbali. Hata hivyo, kama anavyoeleza Ambeka (2008) mtandao una faida zake lakini madhara yake hujitokeza kwa kiwango fulani. Hivyo, wanafunzi wa Kiswahili wanapaswa kusisitiza matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao kwa sababu faida zake zinashinda madhara yake.

Mtandao una athari hasi na chanya kwa watumiaji wake. Mtandao umerahisisha mawasiliano kupitia barua pepe. Ambeka (2008) anasema kuwa barua pepe hii huweza kutumwa pamoja na rasilimali au picha mbalimbali. Mawasiliano na watu wa mataifa mengine huchukua sekunde chache. Wengi wa wataalamu wanasema kuwa, kuwepo kwa barua pepe kumewezesha mawasiliano na tunaowafahamu. Wengi wamepata marafiki kutoka mataifa ya nje ambao wanashirikiana kimaoni na kufahamishana kuhusu tamaduni zao mbali mbali. Kila wakati mambo mapya huzuka kwenye mtandao ambayo hurahisisha maisha ya watu wengi. Habari nyingi zinapatikana kwa urahisi kupitia teknolojia hii. Wanafunzi wa vyuo vikuu wanapotumia mtandao kufanya utafiti, watapata habari za kisasa zitakazowawezesha kujua mambo mapya

katika taaluma yao. Hili litawezekana kupitia mawasiliano na wahadhiri au wanafunzi wenzao kupitia barua pepe ambapo wanaweza kutumia barua pepe kutuma au kupata makala mbalimbali ya kiusomi. Wanafunzi wa Kiswahili wanaweza kutumia barua pepe ili kuzifikia rasilimali za mtandao zitakazowawezesha kukuza tafiti zao.

Injini pekuzi zinatumiwa kupata habari kuhusu mada mbalimbali. Watu wa pande zozote za ulimwengu wanaweza kujadiliana au kushirikisha maoni yao kwenye tovuti tofauti tofauti. Habari hizi katika mtandao haziongezi ujuzi tu bali husaidia kuokoa wakati ambao ulipotezwa kwa kutumiwa njia za zamani za kuzuru maktaba ili kufanya tafiti. Injini pekuzi *Google, Yahoo, Bing* zinatumiwa sana. Habari ni nyingi kuhusu mada zinazotafitiwa kwa mfano, zinaweza kuwa za sheria na huduma za serikali, kitaaluma, makongamano, habari za soko, fikra ngeni, msaada wa stadi mbali mbali na kadhalika. Habari hizi ni muhimu kwa wanafunzi kwa sababu wanaweza kuzitumia kukamilisha miradi na kazi zao kwa wakati unaofaa na kutambua mapya yanayojitokeza katika masomo yao. Hata hivyo, wanafunzi wa vyuo vikuu wasiutegemee tu mtandao bali wavisome vitabu maktabani ili kukuza tafiti zao. Hivyo ni muhimu kwa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno kutafuta vitabu vya Kiswahili katika mtandao ili wavisome na kisha wavitumie kuandika utafiti wao.

Matumizi ya mtandao miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu huwa na madhara. Ponografia ina madhara makubwa kwa watumiaji wa mtandao hasa vijana anavyosema Okinda (2007). Mtandao una ponografia ambazo zimepelekea kudorora kwa maadili katika jamii. Uwazi katika tovuti za mtandao umepelekea watu kuzifikia kwa urahisi. Wengi wao wana shauku ya kujaribu mambo haya ambayo katika jamii zetu hasa za Kiafrika si ya kupendeza. Kwa maoni ya kibinafsi, Masuala ya ushoga yameanza kujitokeza wazi wazi. Kuna ongezeko la matumizi ya madawa ya kulevya. Hivyo, utafiti huu umenuia kutahadharisha watumiaji wa mtandao kuhusiana na madhara haya ya kuwepo kwa ponografia. Wanafunzi wa Kiswahili wanapaswa kutahadhari wanapotumia rasilimali za Mtandao ili wasijipate katika hali ambayo haieleweki, wajikite sana katika masuala ya kiakademia.

Mtandao kama ilivyo teknolojia nyingine, una madhara ambayo wengi wa watumiaji huyapuuza. Ambeka (2008) anasema kuwa, ule uhuru wa mtumiaji unamfanya kutazama na kufanya lolote analotaka kwenye mtandao. Mtumiaji wa mtandao anaweza kupata habari zozote anazotaka. Ni

baadhi tu ya makala ambayo watu hawaruhusiwi kutoa kwani yamezuiliwa kupitia neno au nambari ya siri. Kwamba wapaswa kuingiza nambari hiyo ili uyasome. Makala mengi hayana usiri. Hali hii imepelekea baadhi ya watu kuiba kazi za wengine na kuzifanya zao. Hili hupelekea kodorora kwa viwango vya kitaaluma kwa sababu watu hawataki kufanya tafiti zaidi, wao wamekuwa wazembe. Hivyo, ni muhimu kwa wanafunzi wa Kiswahili kukumbuka kuwa, ni vyema kuzitumia rasilimali za mtandao wa kiakademia kujenga mitazamo yaobkuhusu mada mbalimbali. Hata hivyo waepuke unakili wa moja kwa moja wa kazi zilizo katika mtandao.

Virusi kwenye mtandao vimepelekea wasomi au watu kupoteza habari au makala yao. Baadhi ya barua pepe huwa na virusi hivi. Hili hutokea wakati barua pepe nyingi zinapotumwa kwa mtumiaji mmoja wa mtandao. Hali hii huathiri habari zilizomo katika tarakilishi ya mtumiaji ambapo huweza kupotea au kutosomeka kabisa Ambeka (2008). Wakati mwingine virusi huharibu tarakilishi hata kuizima kabisa. Utafiti huu una mchango katika kutahadharisha kuhusiana na matumizi ya teknolojia hii ambayo mwanafunzi wa Kiswahili anaweza kukumbana nayo wakati wowote, Hivyo, wanafunzi wa Kiswahili wanafaa watambue kuwa wanapotumia rasilimali za mtandao, wanaweza kukumbana na virusi ambavyo huenda vikaathiri kazi zao.

Llo & Ifijeh (2010) walipotafiti athari za matumizi ya mtandao kwa utafiti, walitambua kuwa, wanafunzi (Asilimia 94) walidai kwamba mtandao ulikuwa na umuhimu na wanafunzi (Asilimia 6) wakapinga. Mtandao ulifanya kazi ya utafiti kuwa bora (Asilimia 31.9), kutumia wakati vyema (Asilimia 19.1), miradi kuandikwa kwa kasi (Asilimia 27.0) na maandishi ya kisasa (Asilimia 22.0). Hivyo, ni wazi kuwa athari kuu ya kutumia rasilimali za mtandao na wanafunzi kwa utafiti ni kuwa kazi zilizotokana na utafiti wa mtandao zilikuwa bora, utafiti ulirahisishwa kwani iliandikwa kwa haraka na ulihusisha mambo ya kisasa. Kwa hivyo wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno wanatarajiwa kuzitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia ili kuboresha utafiti wao.

Agil & Ahmad (2011) walifanya utafiti wa matumizi ya mtandao na watafiti na wanafunzi wa uzamili na uzamifu wa kitivo cha sayansi wa Chuo Kikuu cha Waislamu cha Aligarh. Walipata kuwa, watafiti na wanafunzi hawa waliutumia mtandao kufanya utafiti (Asilimia 51.2), mawasiliano (Asilimia 19.5), kujua yanayoendelea (Asilimia 16.46) na kujiendeleza kitaaluma (Asilimia 12.8). Haya yanalingana na utafiti alioufanya Ebersole (2000) ambapo alitambua kuwa

wanafunzi hutumia wavuti kufanya utafiti (Asilimia 52), kuwasiliana na wengine (Asilimia 7), kufikia rasilimali za kozi yao (Asilimia 5), kutafuta habari (Asilimia 8), kupitisha muda (Asilimia 5) na kupata habari za spoti (Asilimia 1). Hivyo, rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia zitawafaa wanafunzi wa Kiswahili ikiwa watazitumia kuboresha utafiti wao wa Kiswahili.

Mtandao ulikuwa na umuhimu mkubwa kwa wanafunzi wa kisayansi wa vyuo vikuu viwili kule Nigeria (Fasae & Aladeniyi, 2012). Umuhimu wa mtandao kwa masuala ya kiakademia ulikuwa kama ifuatavyo, urahisi wa kufanya utafiti (Asilimia 91), ongezeko la habari za kisasa (Asilimia 94), kukua kitaaluma (Asilimia 62), kufikia ufadhili (Asilimia 79), kuufikia ulimwengu (Asilimia 81) na kadhalika. Hivyo, mtandao una habari zinazowawezesha wanafunzi wa vyuo vikuu kuufanya utafiti hivyo kurahisisha utafiti wao.

Bankole & Babalola (2012) walipofanya utafiti wa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Olabisi Onabanjo kule Nigeria walitambua kuwa wengi wa wanafunzi waliutumia mtandao kwa mawasiliano (Asilimia 90.6), kufanya kazi za ziada (Asilimia 43.5), kupata ujuzi (Asilimia 32.9) na kufidia mihadhara (Asilimia 77). Mawasiliano ni muhimu kwa mwanafunzi yeyote haswa wa chuo kikuu. Hii ni kwa sababu mwanafunzi anaweza kuwasiliana na wenzake kwa masuala ya kiakademia na kupata mambo mageni ambayo hakutarajia kupata. Kupita huduma ya barua pepe mwanafunzi wa chuo kikuu anaweza kuwasiliana na wenzake kwa kusambaza au kupokea habari kulingana na kozi waliomo. Mawasiliano kati ya wanafunzi yanawezekana kwa kutumia huduma mbalimbali za mtandao. Mhadhiri anaweza kuweka kazi zake katika mtandao kisha wanafunzi wakazipata na hivyo kuendelea na masomo yao. Hivyo, wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Maseno wanaweza kuweka kazi zao katika mtandao wa kiakademia ili wanafunzi wazifikie haraka na kuzitumia.

Kiai (2013) alipofanya utafiti wa matumizi na utoshelezi wa mtandao kwa wanafunzi wa shahada ya kwanza vyuo vikuu vya Mount Kenya na GRETSA, alisema kuwa, wanafunzi waliutumia mtandao kuwasiliana na wenzao, kupata habari zisizo katika maktaba, kupitia rasilimali za mtandao, kutafuta kazi na kukusanya habari kutoka kwa majarida na vitabu. Kwa jumla wengi wa wanafunzi na wasomi hutumia rasilimali za mtandao kufanya utafiti. Hivyo, ni

muhimu wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno kuzitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia ili kutosheleza mahitaji yao ya kielimu.

Waithaka (2013) alifanya utafiti wa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Nairobi ambapo aliwahoji wanafunzi 381 na kutambua kuwa mtandao ulikuwa na athari kubwa katika masuala ya kiakademia. Nayo ni kuwa, wanafunzi waliweza kuwasiliana na wahadhiri wao (Asilimia 40.7), kutoa na kupokea kazi za ziada (Asilimia 48.5), kufikia habari bora (Asilimia 79.2) na kusambaza habari (Asilimia 69.7). Wengi wa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Nairobi waliutumia mtandao kufikia habari bora ambazo huenda ziliwasaidia kufanya utafiti wao. Hivyo, ni muhimu wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno kuzitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao kukuza tafiti zao.

Hivyo, utumizi wa mtandao umekuwa ni mazoea kwa baadhi ya watu. Ukuaji wa mtu binafsi umeathiriwa sana. Mahusiano ya moja kwa moja na wanajamii wengine hayapo kwa mfano mtu anaweza kutumia mtandao kwa masaa 15 au 16 kwa siku. Hili linakuwa jambo la kawaida kwake na inakuwa vigumu kuwacha. Baadhi ya watu hasa vijana wamesikika wakisema kuwa, “Mimi ni facebook damu” au “Am addicted to facebook 99%” maana kuwa wao hutumia sana mtandao wa *Facebook* wako pamoja na ameshikika kule. Wanafunzi wa Kiswahili hawapaswi kuzitegemea sana rasilimali za Kiswahili za mtandao bali wajihusishe katika kusoma vitabu maktabani. Wanafunzi waunde makundi ya majadiliano ili kujadiliana mada mbalimbali. Hili litakuza mahusiano mazuri kati yao na kuwawezesha kufahamishana mambo mengi.

### 2.5.4 Changamoto zilizowakumba wanafunzi wa vyuo vikuu walipotumia rasilimali za mtandao

Wanafunzi wa vyuo vikuu walikumbwa na changamoto mbalimbali walipoutumia mtandao aidha kwa kutosheleza mahitaji ya kiakademia au kijamii. Luambano & Nawe (2004) wanasema kuwa baadhi ya matatizo ni kama vile, uhaba wa tarakilishi na huduma za tarakilishi, kukatizwa kwa nguvu za umeme na kukwama kwa mitandao. Haya yalisemwa na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Awoleye (2008) anasema kuwa changamoto walizokumbana nazo wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Obafemi Awoloyo wakiutumia mtandao ni kukosa fedha, matatizo ya umeme, kukosa

wakati, hawawezi kuufikia mtandao kibinafsi na hawakuwa na ujuzi wa kuutumia mtandao. Hivyo utafiti huu ulitaka kujua changamoto zinazowakumba wanafunzi wa Kiswahili walipotumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia.

Wanafunzi waliofuzu wa Chuo Kikuu cha Makerere waliutumia mtandao kufanya utafiti na kuwasiliana na wanafunzi wengine (Okello Obura & Magara, 2008). Wanafunzi hawa walikumbwa na matatizo mbalimbali walipotumia mtandao nayo ni; uhaba wa ujuzi, mtandao kudorora, uhaba wa tarakilishi ambazo hazijaunganishwa kwenye mtandao, kutofunguliwa kwa maabara ya tarakilishi na kutojitolea kwa wafanyakazi wa maktaba kuwasaidia namna ya kuutumia mtandao. Hivyo matatizo yanayowakumba wanafunzi wa Kiswahili wa vyuo vikuu yanapaswa kushughulikiwa ili kuwawezesha kuzitumia rasilimali za mtandao.

Wanafunzi wa vyuo vya Fideral na Adekunle kutoka kitivo cha sayansi walikumbwa na matatizo walipotumia mtandao kama vile, ugumu wa kupata habari, uchelewaji wa mtandao na gharama ya juu ya kuzifikia huduma za mtandao. Hivyo, sababu ya wao kutotumia baadhi ya rasilimali za mtandao kwa upana (Fasae & Aladeniyi, 2012). Hili litasuluhishwa ikiwa vyuo vikuu vitawajibika kuweka huduma za mtandao karibu na wanafunzi wao na kwa bei nafuu. Wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno watafaidika pakubwa ikiwa watakuwa na ujuzi wa kutosha ili kupata habari katika mtandao.

Okinda (2007) anasema kuwa baadhi ya matatizo yaliyowakumba wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo ya Kitaaluma ni kuwa hawakuwa na ufahamu wa rasilimali za kielimu, hawakupata maelekezo kutoka kwa wahadhiri wao na hivyo hawakuutumia mtandao sana. Wanafunzi wa vyuo vikuu hukumbwa na changamoto kama vile, kutokuwa na ujuzi wa kutosha wa kudondoa mambo katika mtandao wa kiakademia, ugumu wa kutafuta habari, uhaba wa tarakilishi na kukosa motisha kutoka kwa wahadhiri wao (Oduor, 2010). Hivyo, ikiwa matatizo haya yanaweza kusuluhishwa basi wanafunzi wa vyuo vikuu watafaidika pakubwa. Wahadhiri wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno wanapaswa kuwaelekeza wanafunzi wao wa Kiswahili kuutumia mtandao ili waweze kukuza tafiti zao.

## 2.6 Ufaafu wa rasilimali za mtandao wa kiakademia zinazotumiwa na wanafunzi wa vyuo vikuu

Rasilimali za mtandao zinapaswa kuwa na umuhimu mkubwa kwa watumiaji wake. Rasilimali hizi zitafaa ikiwa zitakuwa na habari zitakazotosheleza mahitaji ya watumiaji wake na ikiwa zitatumiwa na watu hao. Kuwepo kwa habari nyingi katika mtandao kumepelekea kuwepo kwa ugumu kujua habari zinazofaa na zisizofaa. Nazim (2008) alifanya utafiti kuhusu utafutaji wa habari katika mtandao na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Aligarh, alitambua kuwa, asilimia 59.93 walikubali kuwa habari katika mtandao zilifaa, asilimia 23.90 walisema habari hizi ni nzuri sana na asilimia 6.16 hawakutosheka na matumizi ya mtandao. Hivyo, ni muhimu kwa mtumiaji yeyote wa mtandao kutambua ufaafu wa yaliyomo katika chombo hiki cha habari. Wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno wanapaswa kuwa na uwezo wa kutambua rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia zinazofaa na zisizofaa.

Wand & Wang (1996) waliibuka na vipengele muhimu vya kuzingatia ikiwa habari katika mtandao inafaa au haifai. Habari inapaswa kuwa kamilifu, kueleweka, yenye maana na sahihi. Haya ni maoni sawa na ya Cho (2009) ambaye alisema kuwa habari zitafaa zikizingatia muundo sawa, maana na usahihi. Hivyo, ni muhimu kwa habari zilizo katika mtandao ziwe sahihi, zenye maana na kueleweka vizuri.

Lee, Strong, Kahn & Wang (2002) walitambua makundi manne ya ufaafu wa habari katika mtandao, ambayo ni; Habari zinazofaa kisheria, ufaafu wa habari za matini, ufaafu wa muundo wake na ufaafu wa kuzifikia. Hivyo, habari zitafaa ikiwa ni halisi, sahihi na zilizokamilika. Habari hizi zinafaa ziwe zinazotafsiriwa kwa urahisi, rahisi kuelewa, rahisi kubadilishwa, zimewakilishwa kifupi, rahisi kupatikana na salama. Maelezo kuhusu ufaafu wa habari katika mtandao yametolewa na ni wazi kuwa habari hizi huweza kupatikana katika rasilimali mbalimbali za mtandao. Hivyo, maelezo haya yanaweza kutumiwa kueleza ufaafu wa rasilimali za mtandao ili kutambua ikiwa zinafaa kukidhi mahitaji ya watumiaji wake hasa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno.

Ufaafu wa rasilimali yoyote katika mtandao utategemea vigezo vifuatavyo; elimu na tawasifu ya mwandishi, chanzo cha habari za mwandishi zilizozingatia sarufi, uhalisia wa habari katika

rasilimali hiyo, habari zinazohusiana na taaluma inayohusika kwa mfano Kiswahili, rasilimali zenye habari za kumsaidia mtafiti kufanya utafiti, taasisi zinazofadhili rasilimali hizo ziwe zinajulikana na ziwe na rasilimali zilizo na habari zilizopangwa vizuri.

Sahin, Batta & Ercan (2010) wanasema kuwa, rasilimali iliyo bora kutumiwa na wanafunzi ni ile iliyo na sifa zifuatazo. Kwanza, ujuzi wa habari katika rasilimali hizo yaani tajriba ya mwandishi, hadhi yake kielimu na namna anavyounganisha hoja mbalimbali. Pili iwe na habari za hali iliyopo na zinazohusiana na mada husika. Rasilimali hizi lazima ziwe na marejeleo na mambo yaliyopo yanayohusiana na makala ya kiakademia. Mwisho, iwe na tovuti iliyo na uhusiano mzuri na watumiaji wake yaani inazingatia mahitaji na uhakiki wa watumiaji wake. Kuwepo kwa marejeleo katika rasilimali za mtandao ni ishara kuwa zimetafitiwa kwa undani na mchango wa watu wengine umezingatiwa.

Wanaendelea kusema kuwa rasilimali katika mtandao hazitakuwa bora ikiwa, mwanzo, hakuna uzuiaji wa maandishi yanayoandikwa kuwekwa pale, hakuna wahariri au warejelewa, hakuna majarida au magazeti, mtu yeyote anaweza kuweka habari zake na ikiwa imeundwa kwa sababu za kibiashara. Rasilimali katika mtandao zinapaswa kuwa na wahariri maalum waliobobea katika Kiswahili. Hili litaleta usawa wa kuwepo kwa makala sawa yatakayotumiwa na wasomi wote. Ikiwa mtu ataruhusiwa kuweka habari zake basi apate ruhusa kutoka kitengo fulani kinachoshughulikia ufaafu wa rasilimali katika mtandao. Hili litasaidia pakubwa kuwepo kwa habari za kuaminika na zilizokuzwa kitaaluma.

Maeneo ya mtandao yanapaswa kuwa na sifa zifuatazo kwa mujibu wa Sahin, Batta & Ercan (2010); Rahisi kupatikana na zipo wakati wowote ule. Zinaaminika kwa sababu ya uhalisi wa yaliyomo, zina waandishi walio na ujuzi wa juu, zinaweza kuunganishwa na mitandao ya nje na zinafuata sheria zilizopo. Ikiwa rasilimali katika mtandao itapatikana kwa urahisi basi watumiaji wake watafaidika zaidi hasa wanafunzi wa vyuo vikuu katika kutafitia taaluma zao. Rasilimali zizingatie uhalisia ambapo masuala ibuka yajitokeze wazi kuhusiana na taaluma fulani. Uhalisi wa habari au data unaweza kumkuza mtumiaji wa rasilimali husika. Hivyo, ufaafu wa rasilimali za Kiswahili ulijikita katika vigezo vifuatavyo; mwandishi ni nani, lugha iliyotumiwa (Usanifu), taasisi, marejeleo, uhusiano na taaluma ya Kiswahili na upatikanaji wake.

## 2.7 Hitimisho

Waandishi mbalimbali wamechangia pakubwa katika mada matumizi ya mtandao miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu. Tunatambua kuwa matumizi ya mtandao yamekuwepo kwa muda mrefu kuanzia miaka ya hamsini hadi sasa. Teknolojia hii ilipoanzishwa, wahadhiri na wataalamu wa Kisayansi ndio walioutumia sana. Kufikia sasa matumizi yake yameongezeka miongoni mwa watu hasa wanafunzi wa vyuo vikuu. Wengi wa wanafunzi wa vyuo vikuu wanaufahamu mtandao na rasilimali zake lakini hawazitumii sana rasilimali za mtandao wa kiakademia. Wao wanautumia mtandao kuburudika na kuwasiliana na wenzao. wanafunzi walioutumia mtandao waliweza kukuza tafiti zao, kupata matokeo bora ya mitihani yao na kurahisishiwa mawasiliano miongoni mwao na wahadhiri. Baadhi ya wanafunzi wa vyuo vikuu katika nchi zinazoendelea kama Kenya hawakuwa na ufahamu wa rasilimali za mtandao wa kiakademia. Hali hii ilichangiwa na kukosa ujuzi wa kuwawezesha kuzitambua. Hata hivyo, baadhi ya vyuo vinatoa mafunzo kuhusu matumizi ya mtandao na hili na utathmini wa kujua ikiwa wanafaidika na mafunzo haya bado haujashughulikiwa. Baadhi ya maktaba ya vyuo vikuu vya umma hazina tarakilishi zilizounganishwa katika mtandao. Vyuo vikuu vinapaswa kuhakikisha kuwa vinaunganisha tarakilishi zao na mtandao ili wanafunzi waweze kuutumia kutosheleza mahitaji yao ya kielimu. Vyuo vikuu vihusishe mashirika yasiyo ya kiserikali katika kuimarisha TE(KNO)HAMA ili kuwasaidia wanafunzi. Baadhi ya wahadhiri hawawaelekezi wanafunzi wa vyuo vikuu kuzitumia rasilimali za mtandao wa kiakademia. Hivyo, ni muhimu kwa wahadhiri kuwaelekeza na kuwafahamisha wanafunzi wazitumie rasilimali za mtandao wa kiakademia ili kutosheleza mahitaji yao ya kitafiti.

## SURA YA TATU

## NJIA NA MBINU ZA UTAFITI

### 3.1 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia mbinu zilizotumiwa kukusanya data, muundo wa utafiti, eneo la utafiti, kundi lengwa, sampuli, majaribio ya utafiti na maadili yaliyozingatiwa na mtafiti.

### 3.2 Muundo wa utafiti

Muundo wa utafiti uliotumiwa ni muundo wa maelezo ya data kwa kutumia mbinu mseto za kithamano na kitakwimu. Muundo huu unapendekezwa kuwa muhimu kwani humwezesha mtafiti kupata majibu mwafaka ya maswali ya utafiti wasemavyo Johnson na Onwuegbuzie (2004). Mtafiti alitumia mbinu ya kithamano kueleza ufahamu, kuwepo na ufaafu wa rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia. Mbinu hii ilisaidia kuelewa matukio mbalimbali yanayojitokeza katika hali halisi (Strauss & Corbin, 1999). Mtafiti alitumia mbinu ya kitakwimu kuelewa tukio ambalo halijulikani (Luvaha, 2009). Mtafiti aliweza kufahamu utendi wa wanafunzi wa Kiswahili walipotumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia, kupambanua rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia zilizotumiwa na wanafunzi wa Kiswahili na ufaafu wa rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia zilizotumiwa na wanafunzi wa Kiswahili. Tafiti zilizojishughulisha na uchanganuzi wa matini zilitumiwa ili kusisitiza vipimo pamoja na uhusiano wa vipengele. Hivyo, data za kimsingi zitatoka kwa wanafunzi wa Kiswahili na data za sekondari zitahusisha mtandao, vitabu, magazeti na majarida ambazo zilichanganuliwa kwa kutumia vipengele vya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia, kuthibitisha kuwepo na ufaafu wa rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na namna wanafunzi wa Kiswahili wanavyozitumia na kufanya utafiti katika Kiswahili. Data iliwasilishwa kwa kutumia viwango vya idadi na viwango vya asilimia.

### 3.3 Eneo la utafiti

Utafiti wowote ule hufanyika mahali au eneo fulani ili kutimiza malengo yaliyodhamiriwa asemavyo Kombo & Tromp (2006). Malengo ya mtafiti yalimsaidia kuchagua Chuo Kikuu cha Maseno kama eneo la utafiti. Chuo hiki ni cha umma na kinapatikana kaunti ya Kisumu kilomita

25 kutoka Kisumu mjini ukielekea Busia na kozi za Habari na Teknolojia ni za lazima kwa wanafunzi wote. Ingawa vyuo vingine nchini Kenya vinafundisha kozi hizi za habari na teknolojia, masomo haya si ya lazima kwa wanafunzi wote kama ilivyo Chuo Kikuu cha Maseno. Rasilimali za Kiswahili za kiakademia zilizozingatiwa ni katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza na zilizokuwa na mambo ya Kiswahili.

## 3.4 Kundi lengwa

Kundi lengwa ni watu, vitu na mambo yote katika ulimwengu unaoweza kutumiwa katika utafiti Mugenda & Mugenda (1999). Nchini Kenya kuna takriban vyuo ishirini na viwili vya umma vilivyosajiliwa na vingine vishiriki. Chuo Kikuu cha Maseno kiliteuliwa kwa sababu kozi za Habari na Teknolojia ni za lazima kwa wanafunzi wote. Utafiti huu uliwahusisha wanafunzi hamsini na nne wa shahada ya kwanza wa Chuo Kikuu cha Maseno. Wanafunzi hawa waliteuliwa kutokana na wanafunzi takriban mia moja na themanini kutoka Idara ya Kiswahili. Walikuwa hasa wanafunzi wa Kiswahili mwaka 2014/2015. Wanafunzi wa mwaka wa nne waliteuliwa kwa sababu wao walikuwa na tajriba ya kutosha ya kuwa chuoni na kuzitumia rasilimali za mtandao. Utafiti ulilenga watu au kundi fulani ili kukamilisha kazi (Kombo & Tromp, 2006). Watu au kundi la watu hutoa habari ambazo ni muhimu kwa mtafiti kumwezesha kufanya utafiti wake. Mtafiti alipata data kutoka kwa wahojiwa ambapo baadaye huzichanganua ili kutimiza malengo ya utafiti wake. Hivyo, watu au kundi la watu ni muhimu sana ili kuhakikisha kuwa utafiti umekamilika. Watu au kundi la watu walitolewa kutoka sehemu fulani ili kukuza utafiti fulani.  Hivyo, eneo na kundi lengwa huhusiana kwa pamoja ili kuhakikisha kuwa mtafiti anatimiza haja zake za kiutafiti.

## 3.5 Sampuli na usampulishaji

Usampulishaji hufanywa kwa kundi ndogo linalotokana na kundi kubwa wasemavyo Leedy & Ormrod (2005). Utafiti wa kundi dogo huwezesha kupata habari kuhusu kundi kubwa linalohusika. Utafiti huu ulichanganua athari za matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno. Kuna takriban wanafunzi mia moja themanini wa Kiswahili wa mwaka wa nne (2014 /2015). Wanafunzi hamsini na wanne waliteuliwa kwa njia ya bahati nasibu na walipewa hojaji kujaza. Hii ni

asilimia thelathini ambayo inapendekezwa na Mugenda & Mugenda (1999) kuwa inatosha katika utafiti wowote ule hasa chini ya idadi ya watu elfu moja.

Wanafunzi waliopewa hojaji kujaza walitoka Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Maseno kilichoteuliwa kimaksudi wakiwa kwenye mhadhara mmoja wa somo la Kiswahili. Mtafiti alichagua wanafunzi wa mwaka wa nne kwa kuchagua wanafunzi hamsini na nne kwa kutumia sampuli kimaksudi ambao walikuwa asilimia thelethini ya wanafunzi mia moja na themanini. Wanafunzi wa Kiswahili walitakiwa kutoa majibu ya mada ya utafiti. Wanafunzi walikuwa wamefundishwa matumizi ya mtandao mwaka wa tatu hivyo waliweza kuyajibu maswali itakikanavyo. Wanafunzi wa mwaka wa nne waliutumia mtandao kufanya utafiti wa Kiswahili. Hii ni kwa sababu, walikuwa na tajriba ya kutosha wakiwa chuoni pamoja na ujuzi waliopata kutoka kwa marafiki na kozi ya tandao ya mwaka wa tatu. Mtafiti alisampulisha pia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia zilizoandikwa katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza na zinazohusu mambo ya Kiswahili.

### 3.6 Njia na Mbinu za kukusanya data

Data ilikusanywa kwa kutumia mbinu kadha za utafiti. Mtafiti aliweza kukusanya data nyanjani na katika maktaba. Maktabani alichunguza katika mtandao ili kupata habari kuhusu mada kuu. Mtafiti alikusanya vifaa vyote anavyohitaji kufanya utafiti ikiwemo barua ya kumruhusu kufanya utafiti**.** Baadaye mtafiti aliweka bayana madhumuni ya utafiti kwa wanafunzi wa Kiswahili kisha akawapa hojaji. Wanafunzi waliteuliwa kimaksudi ambao na walikua wa mwaka wa nne 2014/2015, Chuo Kikuu cha Maseno. Matumizi ya hojaji yalirahisisha ukusanyaji wa data kwa sababu walioteuliwa walifikiwa kwa wakati mmoja. Hivyo, maelezo zaidi kuhusu namna data ilikusanywa ni yametolewa katika sehemu zifuatazo

#### 3.6.1 Utafiti wa kimajaribio

Utafiti wa awali ulikuwa muhimu kwa sababu ulimsaidia mtafiti kuelewa kundi lengwa. Mtafiti aliwapa wanafunzi watano hojaji kujaza kuhusu mada ya utafiti huu. Wanafunzi watano wa lugha ya Kiswahili mwaka wa nne walitambuliwa na mtafiti kupitia mtafiti msaidizi ambaye alipewa hojaji ili kuwapa wanafunzi kujaza papo hapo kisha mtafiti akachukua. Wanafunzi hawa walichaguliwa kimaksudi ambapo wanafunzi watano wa Kiswahili waliomfikia mtafiti kwanza

walipewa hojaji bila kuzingatia jinsia ila tu awe mwanafunzi wa kozi ya Kiswahili mwaka wa nne.

Wanafunzi wote watano walijaza hojaji na kisha mtafiti akachanganua ili kutambua uelewa wao wa mada ya utafiti. Utafiti wa kimajaribio ulimsaidia mtafiti kujua ikiwa mada ilieleweka au haikueleweka. Pia mtafiti aliweza kutambua ufaafu wa hojaji. Matokeo yaliyopatikana kutoka kwa utafiti wa kimajaribio yalipelekea mtafiti kufanya marekebisho katika hojaji ili kuifanya ieleweke na kufasiriwa vizuri na wahojiwa. Utafiti wa kimajaribio huu haukuwa sehemu ya utafiti.

### 3.6.2 Mbinu za kukusanya data

Mbinu zifuatavyo zilitumiwa kukusanya data;

#### 3.6.2.1 Hojaji

Hojaji ni makala yaliyo na maagizo na maswali yaliyowekwa pamoja kupata majibu kutoka kwa wahojiwa (Waithaka, 2013). Hojaji huwasilishwa kwa njia sawa kimaandishi na kipangilio kwa wahojiwa wote (Kothari, 2004). Hojaji hutoa majibu kwa maswali magumu (Mugenda & Mugenda, 1999). Mtafiti alipomaliza kuunda hojaji, aliifanyia majaribio nyanjani kwa kuwapa wanafunzi watano wa Chuo Kikuu cha Maseno. Wanafunzi hawa walikuwa wa Kiswahili ambao walizijaza na kisha kuzirudisha kwa mtafiti ili afanye marekebisho yaliyopelekea kuwepo kwa usahihi na uelewa wa data iliyopatikana. Mtafiti alitambua udhaifu wa hojaji na hapo hapo akafanya marekebisho yaliyopelekea kuundwa kwa maswali upya yaliyoeleweka na rahisi kujibiwa na wahojiwa. Maswali yalihusu rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia, matumizi ya rasilimali hizi na wanafunzi na ufaafu wa rasilimali zinazotumiwa na wanafunzi wa Kiswahili wa Chu Kikuu cha Maseno. Hojaji ilikuwa na maswali funge na maswali wazi. Maswali funge yalihitaji aliyehojiwa kusema ndiyo au la kwa kuweka alama iliyotakikana kuashiria kuwa lilikuwa ni jibu sahihi. Maswali wazi yalimpa aliyehojiwa nafasi ya kueleza kwa upana kuhusu lile aliloulizwa. Mwanafunzi hakuruhusiwa kuandika jina lake katika hojaji. Alipewa uhuru wa kueleza maoni yake akiwa huru mradi yaliambatana na maswali yaliyoulizwa. Mtafiti aliwapa wanafunzi hamsini na nne hojaji ambapo walitumia muda wa dakika ishirini kujaza wakiwa kwenye mhadhara kisha wakarudisha wakati huo huo. Hii ni mojawapo wa

mbinu inayotumiwa kukusanya data kupitia hojaji wasemavyo Kombo na Tromp (2006). Kwa ujumla, data iliyopatikana ilikuwa takriban asilimia 98 kwa sababu baadhi ya wahojiwa hawakujaza sehemu nyingine. Matumzi ya hojaji yaliweza kuleta matokeo ambayo yalikuwa karibu zaidi na wa hali halisi. Hojaji hiyo inapatikana katika kiambatisho A.

#### 3.6.2.2 Orodha ya uchunguzi

Mtafiti aliunda orodha ya uchunguzi iliyotumiwa kutambua rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia ili kuthibitisha kuwa zipo na zinafaa ilihusu, majarida, magazeti, idhaa za redio, kamusi na mitandao ya Kiswahili. Mtafiti alichunguza katika mtandao kutambua rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia zilizopo na kuthibitisha ikiwa zinafaa kutumiwa na wanafunzi wa Kiswahili. Mtafiti alitumia injini pekuzi ya *Google* kutafuta rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na kutambua ufaafu wake. Maswali yaliwekwa katika injini pekuzi kisha data ilichanganuliwa na habari kutolewa na mfumo enezi wa habari. Baadaye mtafiti alihifadhi habari hizi katika diski tepetevu na kuzihamisha katika tarakilishi yake ya kibinafsi.

#### 3.6.2.3 Mtandao

Mtandao ulitumiwa kupata habari kuhusu historia ya mtandao, matumizi ya mtandao miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu, rasilimali za mtandao, huduma za mtandao na umuhimu wa mtandao kwa watumiaji wake. Mtafiti alitumia maktaba ya Chuo Kikuu cha Maseno ya wanafunzi wa uzamili na uzamifu ambayo ina tarakilishi zilizounganishwa kwenye mtandao. Pia mtafiti alitumia tarakilishi ya kibinafsi kuufikia mtandao na kupata data iliyohitajika. Mtafiti alitumia injini pekuzi za *Google* kutafitia mada husika ambapo aliweza kufikia mitandao ya Kiswahili, majarida, kamusi na magazeti pamoja na idhaa za redio. Habari zilipochanganuliwa na tarakilishi kupitia mtandao, mtafiti alizihifadhi katika diski tepetevu ambapo baadaye alizihifadhi katika tarakilishi ya kibinafsi.

### 3.7 Udhibiti wa vifaa vya kukusanya data

Hojaji ambazo baadhi ya maswali hayakujibiwa hayakujumuishwa katika matokeo. Majibu ya udanganyifu hayakuzingatiwa katika kuandika matokeo. Hili lilinuia kuhakikisha kuwa matokeo

ya utafiti yalikuwa bora. Mtafiti alipata kibali kutoka kwa kitengo cha maadili cha Chuo kikuu cha Maseno kilichomruhusu kuwahoji wanafunzi wa Kiswahili. Hojaji zilitolewa katika mihadhara ili kuhakikisha kuwa kulikuwa na utulivu wa kuwawezesha wanafunzi wa Kiswahili kujibu maswali. Muda wa dakika ishirini ulitumiwa ili kuepuka majadiliano baina yao. Majadiliano hayakuruhusiwa baina ya wahojiwa . Karatasi zilikusanywa baada ya dakika ishirini na majibu yao yalikuwa ya usiri.

### 3.8 Uchanganuzi na uwasilishaji wa data

Data ilichanganuliwa kithamano, kitakwimu na kiuthibitishi

#### 3.8.1 Uchanganuzi wa data kithamano

Habari kutoka katika mtandao zilipitiwa na mtafiti ambapo alizikusanya, kunakili, kupanga na kutathmini kwa kuzingatia madhumuni ya utafiti. Mtafiti alianza kunakili hoja kuu kwa kuzingatia kila lengo na kuzipanga ili kutoa taarifa kamili. Mtafiti alitaja rasilimali za Kiswahili za mtndao wa kiakademia pamoja na tovuti zao. Maelezo yalitolewa kuhusiana na kuwepo kwa rasilimali za Kiswahili na ufaafu wa rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili. Data kutoka hojaji yenye maswali wazi zilipangwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti na maelezo ya kinathari kutolewa.

#### 3.8.2 Uchanganuzi wa data kitakwimu

Data zilizopatikana kutoka kwa hojaji zilihakikiwa na kupitiwa kwa undani ili zichujwe na matokeo yake kupangwa kadri ya mgawanyo wa makundi. Data hizi ziliwasilishwa katika majedwali ili kurahisisha usomaji wa maudhui yatokanayo na uchanganuzi wa data husika. Aghalabu uchanganuzi wa data husika ulihusishwa na lengo kuu na madhumuni mahsusi ya utafiti. Baada ya kuzikusanya na kuzipanga habari zilizopatikana ziliwekwa katika majedwali. Mtafiti aliendelea na hatua ya uchanganuzi wa data yenyewe. Ili mtafiti kuweza kuona ukweli unaotawala katika data hizo na kupata msimamo kuhusu mada ya utafiti, mbinu zifuatazo zilitumiwa kwanza kwa kuunda majedwali yaliyowezesha kupata takwimu zilizopelekea kuafiki au kutoafiki kwa malengo mahsusi ya utafiti. Pili, kuchanganua data kitakwimu na kuhakiki kimaelezo iwapo wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno walizitumia rasilimali za

Kiswahili. Takwimu zilizojitokeza kwenye data ni majibu yatatokana na baadhi ya maswali, kwenye kiambatisho A.

### 3.8.3 Uchanganuzi wa data kwa kuthibitisha

Mtafiti alizingatia majibu yaliyotolewa na wanafunzi ambayo ilikuwa data ya kimsingi kisha alithibitisha ikiwa kweli rasilimali za Kiswahili zipo katika mtandao wa kiakademia na kueleza ufaafu wake kwa kutoa mifano. Rasilimali ziliorodheshwa pamoja na tovuti zao.

### 3.8.4 Uwasilishaji wa data

Data iliwasilishwa kwa njia ya majedwali na kisha maelezo kutolewa. Data kutoka katika hojaji iligawanywa katika makundi matatu. Sehemu hizi tatu zilizingatia madhumuni ya utafiti. Hoja kutoka kwa mtandao zilikuwa tofauti na zilipatikana kutokana na hojaji kisha maelezo kutolewa kwa kutoa mifano zaidi na ithibati kutoka kwa wataalamu mbalimbali. Data kutoka kwa hojaji zilichunguzwa kwa undani kwani mtafiti alifanya hesabu kiasilimia kisha kupanga matokeo hayo katika majedwali.

## 3.9 Uzingatifu wa maadili

Kombo & Tromp (2006) wanasema kuwa, watafiti wanaotafitia watu au wanyama, wanapaswa kuzingatia maadili katika tafiti zao ili utafiti wao uwe kamili. Onwuegbuzie & Collins (2007) wanasema kuwa, mtafiti mzuri ni yule anayefuata kanuni za maadili ya utafiti kama anavyoelezwa na bodi za taasisi mbalimbali ili wanaohojiwa waweze kulindwa. Utafiti huu ulizingatia maadili ya utafiti kama ifuatavyo; Mtafiti alitaja majina ya watafiti mbalimbali katika marejeleo ili kutambua mchango wao katika utafiti huu. Mtafiti alihakikisha kuwa mbinu za kukusanya data ni sawa, kweli na sahihi. Wahojiwa walipaswa kujaza hojaji lakini hawakuruhusiwa kuandika majina yao. Wahojiwa hawakulazimishwa kujaza hojaji na hawakuadhibiwa kwa maoni yao katika hojaji. Mtafiti hakuruhusu msimamo wake kuathiri utafiti. Mada ilichanganuliwa kulingana na malengo ya utafiti na maoni ya wahojiwa. Utafiti nyanjani ulifanywa baada ya mtafiti kuruhusiwa na kitengo cha maadili cha utafiti cha Chuo Kikuu cha Maseno. Barua ya kufanya utafiti iliandikwa na bodi hii ili kumruhusu mtafiti kuendelea na utafiti wake.

# SURA YA NNE

# MATOKEO NA UCHANGANUZI

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inashughulikia data iliyopatikana kutokana na utafiti uliofanywa kuhusu athari za matumizi ya rasilimali za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno. Wanafunzi hamsini na wanne walitumiwa thelathini wa kike na ishirini na wane wa kiume. Matokeo yamewasilishwa kwa kuzingatia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia, matumizi ya rasilimali za Kiswahili na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno na ufaafu wa rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia zinazotumiwa na wanafunzi wa Kiswahili.

## 4.2. Rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia

Madhumuni ya kwanza yalipambanua rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia kwa sababu utafiti uliofanywa miongoni mwa wanafunzi katika hojaji ulionyesha kwamba zipo. Baada ya kutambua kuwa zipo mtafiti alitaka kujua ikiwa zinafaa kutumiwa na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno. Kwa kuzingatia mhimili wa uchaguzi wa chombo cha habari, mtafiti alitambua kuwa chombo cha habari katika muktadha huu ni mtandao ambao una rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia.

Wanafunzi wa Kiswahili walitakiwa kutaja rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia walizozijua ambapo walitaja majarida, magazeti, kamusi na mitandao ya Kiswahili. Matokeo yao kuhusu kuwepo kwa rasilimali za Kiswahili katika Mtandao yalitumiwa kuthibitisha ikiwa ukweli zipo. Hii haimaanishi kuwa mtafiti alitarajia majibu ya uongo kutoka kwa wanafunzi bali ni kusaidia kuyaweka mambo wazi na kisayansi. Swali la kwanza (b) lilitupa matokeo yafuatayo;

**Jedwali 1: Rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia zilizotumika na wanafunzi wa Kiswahili**

| Rasilimali ya Kiswahili | Idadi ya wanafunzi | Asilimia |
|---|---|---|
| Majarida | 36 | 66.7 |
| Kamusi | 10 | 18.5 |
| Mitandao ya Kiswahili | 15 | 27.8 |
| Magazeti | 26 | 48.1 |

Wanafunzi wote wa Kiswahili waliohojiwa walitaja rasilimali za Kiswahili ambapo wanafunzi 36 (Asilimia 66.7) walitaja majarida, wanafunzi 10 (Asilimia 18.5) kamusi, wanafunzi 15 (Asilimia 27.8) mitandao ya Kiswahili na wanafunzi 26 (Asilimia 48.1) walitaja magazeti. Hivyo, wanafunzi wengi walitaja majarida kama mojawapo wa rasilimali za Kiswahili. Hii ni kweli kuwa wanafunzi hawa walitumia rasilimali hii sana. Kuna wale waliotaja kamusi kama rasilimali ya Kiswahili na waliokuwa idadi ndogo. Idadi ya wastani ya wanafunzi walitaja mitandao ya Kiswahili kama rasilimali ya Kiswahili. Hivyo, kuna uwezekano kuwa baadhi ya wanafunzi wa Kiswahili hawajajua kuwepo kwa rasilimali ya mitandao ya Kiswahili ambayo huwapa makala ya mtandao katika lugha ya Kiswahili. Mwisho wanafunzi wengine walitaja kuwepo kwa magazeti katika mtandao. Baadhi ya wanafunzi wa Kiswahili walisoma magazeti katika mtandao kujua yanayoendelea au kuendeleza taaluma yao.

Kutokana na hali kuwa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno walifahamu rasilimali za Kiswahili za mtandao, hawakuweza kutoa mifano pamoja na wavuti zinazopatikana. Hivyo, mtafiti aliamua kuorodhesha rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia kwa kuzingatia majibu yaliyotolewa na wanafunzi wa Kiswahili ambayo yalitajwa bila kuzingatia mahali zinapopatikana na kuongezea panapohitajika. Uthibitishaji huu utawafaa wanafunzi wa Kiswahili kwa sababu wataweza kuzifikia kwa haraka na kuzitumia katika kufanya utafiti wao. Baadhi ya rasilimali za Kiswahili zilizo katika mtandao ni kama vile, majarida, vitabu, magazeti, kamusi, mitandao ya Kiswahili na idhaa za redio.

### 4.2.1 Majarida

Mifano ya majarida kama anavyotaja Mohochi (2011), ni kama vile jarida la *Nordic Journal of African Studies*. Jarida hili lina makala 33 yaliyoandikwa katika lugha ya Kiswahili. Makala haya yanahusu masuala mbalimbali katika lugha ya Kiswahili. Anataja jarida la *Swahili Forum* ambapo makala 38 yamechapishwa katika lugha ya Kiswahili. Makala haya yanahusu mambo ibuka katika lugha ya Kiswahili. Kuongezea, kuna majarida mengine ambayo yanahusisha masuala ya kiafrika hasa lugha, utamaduni na fasihi. Majarida mengine yaliyo na makala yanayohusiana na lugha ya Kiswahili ni kama ilivyobainika katika jedwali.

**Jedwali 2: Majarida yaliyo na mambo ya Kiswahili**

| **Jarida** | **Tovuti** |
|---|---|
| Swahili Forum | www.uni-leipzig.de/afrika/swafo |
| Journal of Pan African Studies | www.jpanfrican.com/../vol2no8.htm |
| Nordic Journal of African Studies | www.njas.helsinki.fi. |
| African Journal Online | www.ajol.infor/index |

### 4.2.2 Magazeti na idhaa za redio/ runinga

Wanafunzi wa Kiswahili hawakutaja idhaa za redio, hivyo mtafiti aliziongezea kwa sababu zina mchango mkubwa katika ukuaji wa lugha hasa ya Kiswahili. Baadhi ya idhaa za redio zinapatikana katika Mtandao na zinaweza kuwasaidia wanafunzi wa Kiswahili. Magazeti na idhaa za redio katika mtandao ni kama vile Majira, Taifa leo, Alasiri, Nipashe, Raia Mwema, 'Deutsche Welle' katika Kiswahili na Habari leo. Nchini Kenya kuna idhaa za redio /runinga zinazopeperusha habari kwa lugha ya Kiswahili kwa mfano 'KBC, Citizen, Nation, KTN na K24.Baadhi zina tovuti kama vile; Magazeti mtandaoni nchini Kenya http://www.africaonline.co.keMagazeti Tanzania- http://www.onlineneswpapers.com/tanenia.htm, Swahili News http://www.swahilinews.com/, Taifa Kenya http://www.kbc.co.ke/, Habari Newsletterhttp://www.afrst.uiuc.edu/Habari06.pdf,RedioUingerezahttp://www.bbc,co.uk/swahili Idhaa ya Kiswahili ya KBC http://www.kbc.co.ke/channel/asp?ID=3 Sauti ya Marekani http://www.VOA.gov/swahili, Redio Ujerumani http://www.dwele,de/kiswahili

### 4.2.3 Kamusi

Kamusi ni rasilimali muhimu sana kwa mwanafunzi wa Kiswahili. Kamusi husaidia katika kuelewa misamiati ambayo haifahamiki kwa urahisi. Hivyo, wanafunzi wa Kiswahili walizitumia kuendeleza utafiti wao. Baadhi ya Kamusi katika mtandao ni kama vile, Wikipedia kamusi elezi huru, kamusi ya Kiswahili -Kiingereza/Kamusi ya Kiingereza - Kiswahili na 'Kamusi project'. 'Kamusi Project' bado inaendelea kuundwa na wataalamu wa Kiswahili kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha Yale. Baadhi ya tovuti za kamusi hizi ni kama vile; Wikipedia http://en.wikipedia.org/wiki/swahili, Kamusi Project http://www3.iath.virginia.edu/swahili, Kamusi ya Kiswahili Kiingereza http://www.cis.yale.edu/swahili/, Kamusi ya Kiswahili www.glcom.com/hassan/dictionary/swa, Kamusi ya tafsiri Kiswahiliwww.lexicool.com>Home> Online dictionary by language

### 4.2.4 Mitandao ya Kiswahili

Mitandao ya Kiswahili ni rasilimali ya Kiswahili iliyo na makala mengi ya Kiswahili ambayo yanaweza kumfaidi mwanafunzi wa Kiswahili. Mitandao ya Kiswahili ina makala mengi kuhusu lugha, fasihi na isimu ambazo ndizo nguzo za mwanafunzi yeyote wa Kiswahili. Mitandao hii imeorodheshwa kwa kuzingatia umuhimu wake kwa mwanafunzi wa Kiswahili kutokana na tajriba ya mtafiti. Ufaafu wa mitandao ya Kiswahili pia ulizingatiwa. Baadhi ya makala katika mitandao ya Kiswahili ni kama vile; Kiswahili kwenye mitandaowww.dw.com/../a17888607, Idhaa za kimataifa na Kiswahili sanifu kwenyewe .wordpress.com/2014/03/12/j… na Tafsiri imachangia pakubwa katika ukuaji wa Kiswahili www.swahili hub.com/../index.html

Blogu za Kiswahili huweza pia kuwekwa katika kundi la rasilimali za Kiswahili za mtandao. Blogu ni tovuti yenye maingizo yanayoitwa machapisho (Posts) ambayo huonekana katika utaratibu wa kutangulia chapisho jipya kwanza na kufuatizwa na machapisho ya nyuma. Huhusisha machapisho, viungo (Links) na maoni ya watembeleaji ili kuongeza maingiliano ya kimawasiliano kati ya blogu na watembeleaji wa blogu hiyo. Mifano wa blogu ni ya Dafina ya Kiswahili na Nakungah ambazo zina maarifa kuhusu lugha ya Kiswahili. Hivyo, kuwepo kwa rasilimali za Kiswahili za mtandao kumewafanya wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno kutumia chombo hiki cha habari ili kutosheleza mahitaji yao ya kufanya utafiti. Mtafiti

ameongezea mifano mingine ya viunganishi vya kielimu vya Kiswahili katika mtandao ambavyo vinafunzwa katika vyuo mbalimbali vya kimataifa kupitia mtandao. Navyo ni; Aina za nomino katika Kiswahili http://www.g/com.com/cyberswahili/swahili.html, Ushairi wa Kiswahili http://www.humnet.ucla.edu/humnet/aflang/swahili/excercises/index.html, Kiswahili lugha na utamaduni http://www.g/com/hassan/other res/other resources.html, Historia ya lugha ya Kiswahili http://www.g/com.com/hassan/swahilihistory/html, Namna ya kutamka sauti za Kiswahili http://www.yale.edu/swahili/sound/pronounciation, Maandishi ya kanga za Kiswahili http://www.g/com.com/hassan/kanga.html, Muziki wa Kiswahili http://www.kiswahili.net/kis-videos-net.html, Kazi za marudio za kusikiliza na kusoma kutoka Chuo Kikuu cha Pennyslavania http://ccat.sas.upenn.edu/pic/kiswahili,ManenomuhimuyaKiswahilihttp://www.g/com.com/hassan/swahili.html, Viunganishi vya sahili moja http://www.moja.com/Swahili/, Kitabu cha lugha za kiafrika http://www.isp.msu.edu/AfrLang/hiermenu.html

## 4.3 Matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno.

Madhumuni ya pili ya utafiti huu yalikuwa kueleza matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Maseno. Mambo yaliyozingatiwa ni ufahamu wa rasilimali za Kiswahili na wanafunzi wa Kiswahili, viwango vya matumizi, umuhimu wa matumizi ya mtandao wa kiakademia kwa utafiti wa Kiswahili na changamoto zinazowakumba wanafunzi wa Kiswahili wanapotumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia. Utendi wa wanafunzi wa Kiswahili kwenye mtandao uliwawezzesha kufahamu baadhi ya rasilimali za kiakademia. Hivyo, ufahamu wa rasilimali za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno ni ifuatavyo;

### 4.3.1 Ufahamu wa rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno

Ufahamu wa rasilimali za mtandao ulitajwa na wanafunzi wa Kiswahili ambapo walielekezwa kupitia swali la kwanza (a) katika hojaji ambalo lilitaka wataje rasilimali hizo ikiwa walizifahamu katika swali (b). Muhimili wa hadhira tendi katika nadharia ya Mawasiliano inayorejelea matumizi na utoshelezi umesaidia kueleza matumizi ya rasilimali za Kiswahili na wanafunzi wa Kiswahili ambao huwa tendi katika matumizi yao ya rasilimali za Kiswahili. Wao wenyewe hujihusisha na matumizi ya rasilimali za mtandao ndio maana inawabidi kufahamu rasilimali hizi katika mtandao.

**Jedwali 3 : Ufahamu wa rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno**

| **Ufahamu** | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Ndiyo | 50 | 92.6 |
| La | 4 | 7.4 |
| Jumla | 54 | 100 |

Wanafunzi 50 (Asilimia 92.6) walisema kuwa wana ufahamu wa kuwepo kwa rasilimali za Kiswahili. Wanafunzi 4 (Asilimia 7.4) walisema kuwa hawana ufahamu wa rasilimali za Kiswahili za mtandao. Mtumiaji yeyote wa chombo cha habari anapaswa kujua yaliyomo ili aweze kukitumia ipasuavyo kutosheleza mahitaji yake. Wanafunzi wa Kiswahili kama ilivyo watumiaji wengine wa mtandao wanahitajika kufahamu rasilimali za mtandao ili waweze kuzitumia kutosheleza mahitaji yao ya kielimu na hata kijamii. Mwanafunzi anaweza kukosa kufahamu kuwepo kwa rasilimali fulani kwa sababu labda hajafundishwa au hana ujuzi wa kumwezesha kutambua rasilimali hizi za mtandao.

Baadhi za tafiti zinakubaliana na utafiti huu kuwa wengi wa wanafunzi wa vyuo vikuu wana ufahamu wa kuwepo kwa rasilimali za mtandao. Luambano & Nawe (2004) wanasema kuwa, wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam walifahamu kuwepo kwa majarida, magazeti na kamusi. Haya ni maoni sawa na ya Waithaka (2013) alifanya utafiti uliohusisha wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Nairobi ambapo wanafunzi walisema kuwa, walifahamu kuwepo kwa rasilimali

za mtandao za kiakademia kwenye maktaba zao. Nazo zilikuwa ni majarida, magazeti, vitabu, kamusi, ensaiklopidia na kadhalika. Wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno waliweza kutaja majarida walikuwa 36 (Asilimia 66.7), waliotaja magazeti walikuwa 26 (Asilimia 48.1) waliotaja kamusi walikuwa 10 (Asilimia 18.5) na mitandao ya Kiswahili walikuwa wanafunzi 15 (Asilimia 27.8).Wengi wa wanafunzi wa Kiswahili wana ufahamu zaidi wa majarida ikilinganishwa na mitandao ya Kiswahili au kamusi. Kuwepo kwa vitabu, ensaiklopidia na rasilimali nyingine haukuzingatiwa na wanafunzi wa Kiswahili. Huenda hawafahamu kuwa zipo kwa sababu ya kukosa ujuzi wa kuzitambua. Hivyo, ni muhimu wanafunzi wa Kiswahili kufahamu kuwa rasilimali za Kiswahili zipo aina mbalimbali na zinapaswa kutumiwa ili kukuza utafiti wao.

### 4.3.2 Viwango vya matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno.

Baada ya wanafunzi kusema wanazifahamu na kutaja rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia, mtafiti alitaka kujua viwango vya matumizi. Matumizi ya rasilimali za mtandao yalihusisha mambo yafuatayo; ikiwa walizitumia kufanya utafiti, lugha waliyoitumia, muda walioutumia, tajriba ya kuzitumia, ujuzi wa kuzitumia, njia za ujifunzaji wa namna ya kuzitumia, ikiwa ni kozi wanayofundishwa chuoni ya Habari na Mawasiliano na ikiwa ilikuwa na umuhimu, kilichowasukuma kuzitumia rasilimali, mahali walipozifikia, rasilimali zinazotumiwa zaidi, njia za kudurusu katika mtandao ili kuzifikia na changamoto wanazokumbana nazo wanapozitumia rasilimali hizi.

**Jedwali 4 : Matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili kufanya utafiti**

| | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Ndiyo | 49 | 90.7 |
| La | 5 | 9.26 |
| Jumla | 54 | 100 |

Swali la tatu katika hojaji lilinuia kutupa majibu ikiwa wanafunzi wa Kiswahili walitumia rasilimali za Kiswahili kufanya utafiti. Jedwali hili linaonyesha kuwa wanafunzi 49 (Asilimia

90.7) waliutumia mtandao kufanya utafiti wa Kiswahili na wanafunzi 5 (Asilimia 9.26) hawakuzitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia kufanya utafiti. Hili linaonyesha kuwa wanafunzi wengi wa Kiswahili walidhihirisha utendi walipozitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia kufanya utafiti wao kwa sababu uliwapa habari walizohitaji. Wanafunzi ambao hawakuzitumia rasilimali kufanya utafiti walitumia vitabu, majarida au magazeti yaliyokuwa maktabani. Hivyo, tunaona mchango wa Mtandao katika kuendeleza utafiti wa wanafunzi wa vyuo vikuu ikilinganishwa na rasilimali zilizoko katika maktaba. Bankole & Babalola (2012) walipofanya utafiti kuhusu matumizi ya mtandao miongoni mwa wanafunzi wa shahada ya kwanza wa Chuo Kikuu cha Olabisi Onabanjo, walipata kuwa wanafunzi wengi (Asilimia 97.6) waliutumia mtandao kufanya utafiti na kuwasiliana na wenzao lakini wachache (Asilimia 2.4) hawakuutumia. Hii ni ishara kuwa wengi wa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Maseno na wa Chuo Kikuu cha Olabisi Onabanjo waliutumia mtandao kufanya utafiti. Haya ni maoni sawa na yale ya wataalamu Jones and Madden (2012); Dave (2012) na (Osunade 2003). Kando na kuutumia mtandao kufanya utafiti, baadhi ya wanafunzi wa vyuo vikuu waliutumia kutuma na kupokea barua pepe, kuwasiliana na wenzao au wahadhiri wao (Dave 2012; Bankole & Babalola 2012; Awoleye 2008). Hivyo, ikiwa wanafunzi wa Kiswahili walitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia waliweza kukuza tafiti zao.

Wanafunzi wa Kiswahili wanapotumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia, wao hutumia lugha kuzitambua ili kuzitumia. Hivyo, lugha inayotumiwa na wanafunzi wa Kiswahili kuzitambua rasilimali za Kiswahili ilishughulikiwa.

**Jedwali 5: Lugha inayotumiwa na wanafunzi wa Kiswahili katika mtandao kufanya utafiti**

| **Lugha** | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Kiswahili | 20 | 37.0 |
| Kiingereza | 34 | 62.9 |
| Jumla | 54 | 100 |

Swali la nne lilihusu lugha inayotumiwa na mwanafunzi kufanya utafiti wa Kiswahili. Mtafiti alitaka kujua lugha wanayotumia ili afahamu mchango wa lugha katika suala zima la rasilimali za Kiswahili katika mtandao. Jedwali hili linaonyesha kuwa wanafunzi 20 (Asilimia 37.04) walidai kuwa walitumia lugha ya Kiswahili katika mtandao na wengine 34 (Asilimia 62.96)

walitumia lugha ya Kiingereza. Hii ni ishara kwamba wanafunzi wa Kiswahili wamegawika kuwili kuhusu matumizi ya lugha fulani wanapofanya utafiti. Kuna wale hutumia Kiswahili na wale wanaotumia Kiingereza muradi wapate kile wanachokitafuta ili kutosheleza mahitaji yao. Sababu iliyowafanya kutumia Kiingereza ilhali wao ni wanafunzi wa Kiswahili ni kuwa walipata majibu yaliyotosheleza mahitaji yao ikilinganishwa na walipotumia lugha ya Kiswahili ambayo imetumika kwa uchache katika mtandao.

Wanafunzi wa Kiswahili walipozitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia, walitumia muda fulani. Hivyo, mtafiti alitaka kujua muda uliotumiwa na wanafunzi hawa walipozitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia.

**Jedwali 6: Muda wa matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili**

| **Muda** | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Kila siku | 14 | 25.9 |
| Mara 2 – 3 kwa wiki | 25 | 46.3 |
| Mara 2 – 3 kwa mwezi | 13 | 24.1 |
| Mara moja kwa mwezi | 2 | 3.7 |
| Jumla | 54 | 100 |

Swali la nne katika hojaji lilihusu muda unaotumiwa na wanafunzi wa Kiswahili kuzitumia rasilimali za Kiswahili ili kufanya utafiti wao. Wanafunzi 14 (Asilimia 25.9) walizitumia kila siku, wanafunzi 25 (Asilimia 46.3) walizitumia mara 2-3 kwa wiki, wanafunzi 13 (Asilimia 24.1) walizitumia mara 2-3 kwa mwezi na wanafunzi 2 (Asilimia 3.7) walizitumia rasilimali za Kiswahili mara moja kwa mwezi. Wanafunzi wengi wa Kiswahili wanazitumia rasilimali za Kiswahili mara 2-3 kwa wiki. Hii ni ishara kuwa, wao hutumia kwa kiwango cha wastani rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia. Wanafunzi wanaotumia rasilimali hizi mara moja kwa mwezi wanaweza kuvifikia vitabu maktabani hivyo hawana haja sana na mtandao au hawana ujuzi wa kuwawezesha kuzitumia rasilimali hizi kufanya utafiti wao. Fasae & Aladeniyi (2012) wanakubaliana na maoni haya pale ambapo walitambua kuwa wanafunzi wa kisayansi wa vyuo vikuu viwili kule Nigeria waliutumia mtandao mara 2-3 kwa wiki (asilimia 4) mara 2-3

kwa mwezi (asilimia 34) kila siku (asilimia 19) na mara moja kwa mwezi (asilimia 3). Hivyo, wengi wa wanafunzi wa vyuo vikuu hivi vitatu hutumia rasilimali za mtandao wa kiakademia mara 2-3 kwa wiki. Ni vyema wanafunzi wa Kiswahili kuzitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia kila mara ili waweze kupata habari nyingi zinazoweza kutosheleza mahitaji yao hasa ya kiakademia.

Wanafunzi wa Kiswahili walipotumia rasilimali za Kiswahili za mtandao walikuwa na tajriba ya kuzitumia. Hivyo, kulikuwa na haja ya kujua tajriba ya wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno na matokeo yalikuwa yafuatayo;

**Jedwali 7 : Tajriba ya kuzitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia**

| **Tajriba** | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Chini ya mwaka mmoja | 5 | 9.3 |
| Mwaka 1 | 10 | 18.5 |
| Miaka 2 – 3 | 26 | 48.1 |
| Zaidi ya miaka 3 | 13 | 24.1 |
| Jumla | 54 | 100 |

Swali la tano lilihusu tajriba waliyokuwa nayo wanafunzi wa Kiswahili ya kuzitumia rasilimali za Kiswahili**.** Wanafunzi 26 (Asilimia 48.1) walikuwa na tajriba ya kati ya miaka 2-3, wanafunzi 13 (Asilimia 24.1) zaidi ya miaka 3, wanafunzi kumi (Asilimia 18.5) mwaka mmoja na wanafunzi 5 (Asilimia 9.3) chini ya mwaka mmoja. Wengi wa wanafunzi wa Kiswahili walikuwa na tajriba ya kuzitumia rasilimali za Kiswahili kwa muda wa miaka kati ya miwili na mitatu.

Hili linaonyesha kuwa walianza kuutumia mtandao wakiwa miaka kati ya wa pili na wa tatu. Wanafunzi 5 (Asilimia 9.3) ambayo ilikuwa ndogo sana walizitumia rasilimali za Kiswahili katika kipindi kisichozidi mwaka mmoja. Hivyo, walianza kuzitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia wakiwa mwaka wa nne. Hii inamaanisha kuwa miaka mitatu aliyokuwa amesoma hakuzitumia sana rasilimali za Kiswahili kufanya utafiti wa Kiswahili. Hii ni tofauti na utafiti wa Waithaka (2013) ambaye alitambua kuwa,wengi wa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Nairobi walikuwa na tajriba ya miaka 3-4 (asilimia 37.9) na miaka 4-5 (asilimia 43.3). Wengi wa

wanafunzi wa vyuo vikuu wanaosoma shahada ya kwanza wana tajriba ya kuutumia Mtandao kwa zaidi ya miaka mitatu kama walivyotambua Fasae & Aladeniyi (2012). Wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno wanapaswa kuelekezwa na wahadhiri kuzitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia wakiwa mwaka wa kwanza ili wanapofika mwaka wa nne wawe wamekua zaidi na wanaweza kuwa na ujuzi wa kutosha wa kuzifikia rasilimali za mtandao zilizopo wakati fulani. Tajriba ni muhimu katika kuwawezesha wanafunzi wa Kiswahili kuzitumia zaidi rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia. Ujuzi wa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno ulikadiriwa kiasilimia kujua ikiwa walikuwa na ujuzi wa juu, wastani na chini.

**Jedwali 8 : Ujuzi wa wanafunzi wa Kiswahili wa kuzitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia**

| **Asilimia ya ujuzi** | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| 0 – 40 (Chini) | 4 | 7.4 |
| 40 – 70 (Wastani) | 34 | 62.9 |
| Zaidi ya 70 (Juu) | 12 | 22.2 |
| Sifahamu | 4 | 7.4 |
| Jumla | 54 | 100 |

Swali la sita lilimwezesha mtafiti kupata data zaidi kuhusu ujuzi walionao wanafunzi wa kuzitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia. Swala hili lilinuia kujua kiwango cha ujuzi wa wanafunzi wa Kiswahili. Sehemu ya 0 – 40 ikiwa ya chini, 40 – 70 wastani, zaidi ya 70 juu na sifahamu ni yule ambaye hangeweza kukadiria. Hivyo, wanafunzi 34 (Asilimia 62.9) ni wa kiwango cha wastani, wanafunzi 12 (Asilimia 22.2) kiwango cha juu, wanafunzi wanne (Asilimia 7.4) kiwango cha chini na wanafunzi wanne (Asilimia 7.4) hakufahamu kiwango chao..

Hili linaonyesha kuwa, nusu ya wanafunzi wa Kiswahili waliohojiwa walikuwa na ujuzi wa wastani wa namna ya kutumia mtandao. Hata hivyo kuna wale waliodai kuwa ujuzi wao ulikuwa wa juu ambao ni zaidi ya robo ya idadi ya waliohojiwa. Wanafunzi wachache wana ujuzi wa kiwango cha chini au pia hawawezi kukadiria ujuzi wao. Ikiwa wanafunzi wa Kiswahili wana ujuzi wa wastani au juu wa kutumia mtandao basi ni rahisi wao kupata habari zinazowasaidia

kufanya utafiti. Haya ni tofauti na Oduor (2010) aliyefanya utafiti katika Chuo cha Masomo ya Kitaaluma nchini Kenya kuhusu matumizi na utoshelezi wa mtandao kwa wanafunzi hawa. Alipata kuwa wengi wa wanafunzi alioweza kuwahoji hawakuutumia mtandao kwa sababu hawakuwa na ujuzi, hali iliyopelekea wao kuwa na ugumu wa kutafuta habari katika mtandao. Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Malaysia wa shahada ya kwanza walikuwa na ujuzi wa wastani (Asilimia 70) na wa juu (Asilimia 27) asemavyo Muniandy (2010). Ni wazi kuwa ili wanafunzi wa Kiswahili wazitumie rasilimali za mtandao, wanapaswa kuwa na ujuzi fulani. Hivyo, ilikuwa nia ya mtafiti kujua namna walivyopata ujuzi huu ili kusaidia kutimiza malengo ya utafiti. Ujuzi wa matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili ni muhimu kwani ni rahisi kuzitambua rasilimali hizo hivyo, kupata habari zinazokuza tafiti zao.

Ujuzi wa wanafunzi wa Kiswahili ulimpelekea mtafiti kutaka kujua njia za ujifunzaji wa namna ya kuzitumia rasilimali za Kiswahili. Hivyo, matokeo yalikuwa ifuatavyo;

**Jedwali 9 : Njia za ujifunzaji wa namna ya kuzitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia**

| Njia | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| Kuhudhuria mihadhara ya kozi Habari na Teknolojia | 14 | 25.9 |
| Maktaba | 5 | 9.3 |
| Marafiki | 20 | 37.0 |
| Binafsi | 15 | 27.8 |
| Jumla | 54 | 100 |

Swali la saba lilichangia kuwepo kwa data kuhusu njia ambazo wanafunzi walizitumia kujua rasilimali za Kiswahili. Swala hili lililenga kufahamu namna wanafunzi wa Kiswahili walivyopata ujuzi wa kutumia rasilimali za Kiswahili katika mtandao. Jedwali linaonyesha wanafunzi 20 (Asilimia 37.0) walipata ujuzi kutoka kwa marafiki, wanafunzi 14 (Asilimia 25.9) kutoka kwa mihadhara ya kozi za Habari na Teknolojia, wanafunzi 15 (Asilimia 27.8) kutoka kwa juhudi za kibinafsi na wanafunzi watano (Asilimia 9.3) kutoka kwa maktaba.

Ni dhahiri shahiri kuwa asilimia kubwa ya wanafunzi wa Kiswahili waliohojiwa walipata ujuzi wa kutumia mtandao kutoka kwa marafiki. Hii ina maana kuwa marafiki wana mchango mkubwa katika kuwapa ujuzi wenzao kuhusiana na matumizi ya rasilimali za mtandao. Kozi ya Habari na Teknolojia inayofunzwa Chuo Kikuu cha Maseno pia imechangia kuwapa wanafunzi wa Kiswahili ujuzi wa kutumia mtandao. Kozi hii ni ya lazima kwa wanafunzi wote wa chuo hiki. Hufunzwa mwaka wa tatu ambapo somo maalumu huwa ni matumizi ya mtandao. Hata hivyo, kuna wale wamefanya juhudi za kibinafsi kujifunza kutumia mtandao ili kupata habari zitakazowasaidia kufanya utafiti.

Haya ni tofauti na Bankola & Babalola (2010) walipotafiti kuhusu matumizi ya mtandao miongoni mwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Olabisi Onabanjo kule Nigeria, walipata kuwa wanafunzi wengi walipata ujuzi kwa juhudi za kibinafsi (Asilimia 48.2), marafiki (Asilimia 20.8), kuhudhuria makongamano (Asilimi 19.4), kusoma vitabu katika mtandao (Asilimia 9.1), mihadhara (Asilimia 6.4) na maktaba (Asilimia 2.4). Tafiti hizi mbili zinaonyesha kuwa, njia kuu zilizotumiwa kupata kujua namna ya kutumia mtandao na wengi wa wanafunzi ni kupitia marafiki na juhudi za kibinafsi. Njia iliyokuwa na mchango mdogo ni kupitia maktaba. Ni wazi kuwa maktaba katika chuo Kikuu cha Maseno haina mchango mkubwa wa kuwapa wanafunzi wa Kiswahili ujuzi wa kuutumia mtandao. Ni vyema kuwa vyuo vikuu vingi vinajizatiti kuwapa wanafunzi wao kozi za TE(KNO)HAMA ili waweze kufahamu maendeleo ya teknolojia yaliyopo hasa matumizi ya mtandao. Wanafunzi wa Kiswahili waliosema kuwa kozi ya Habari na Teknolojia iliwasaidia kujifunza kuzitumia rasilimali za Kiswahili walitoa sababu zifuatazo;

**Jedwali 10: Umuhimu wa kozi ya mtandao ya Habari na Teknolojia kwa wanafunzi wa Kiswahili**

| **Umuhimu** | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Kupata habari za utafiti | 50 | 92.6 |
| Kupata nadharia mbalimbali | 5 | 9.3 |
| Namna ya kutumia mtandao | 15 | 27.8 |
| Kusoma katika mtandao | 20 | 37.0 |
| Hawakujibu | 2 | 3.7 |

Kutokana na hali kuwa huenda wanafunzi wengine walijifunza matumizi ya mtandao kupitia kozi za Habari na Teknolojia, mtafiti alitaka kujua ikiwa wanafunzi hawa walifaidika na kozi hii. Hivyo, swali la saba lilipelekea ufahamu wa umuhimu wa kozi hii kwa wanafunzi wa Kiswahili. Suala hili lililenga kujua namna wanafunzi wa Kiswahili walifaidika kwa kuhudhuria mihadhara ya kozi ya Habari na Teknolojia. Majibu yaliyotolewa yalikuwa zaidi ya moja. Matokeo ni kwamba wanafunzi 50 (Asilimia 92.6) walifaidika kwa kupata habari za kufanya utafiti, wanafunzi 15 (Asilimia 27.8) iliwasidia kujua namna ya kutumia mtandao, wanafunzi 20 (Asilimia 37.0) waliweza kusoma katika mtandao, wanafunzi 5 (Asilimia 9.3) waliweza kupata nadharia mbalimbali na wanafunzi 2 (Asilimia 3.7) hawakujibu.

Ni wazi kuwa kozi ya matumizi ya mtandao ya Habari na Teknolojia inayotolewa kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Maseno yaani wanaosomea Kiswahili ni yenye manufaa. Wanafunzi wanaweza kupata habari zinazowasaidia kufanya utafiti, kujua namna ya kutumia na kusoma katika mtandao na kupata nadharia mbalimbali. Kwa hivyo, ni muhimu ikiwa kozi hii itaendelea kusisitizwa ili wanafunzi waweze kufaidika pakubwa kupitia matumizi ya mtandao. Isipokuwa njia ya kujifunza kuzitumia rasilimali za Kiswahili, wanafunzi wa Kiswahili walikuwa na msukumo wa kuwafanya kuzitumia rasilimali za Kiswahili. Hivyo, maelezo ni yafuatayo;

**Jedwali 11: Kinachowasukuma wanafunzi wa Kiswahili kuzitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia**

| **Msukumo** | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Binafsi | 32 | 59.3 |
| Wahadhiri | 17 | 31.5 |
| Marafiki | 5 | 9.3 |
| Jumla | 54 | 100 |

Swali la tisa liliundwa kwa kusudi la kujua msukumo wa wanafunzi kuzitumia rasilimali za Kiswahili katika mtandao. Sehemu hii ilinuia kufahamu kinachowasukuma kutumia mtandao kufanya utafiti wa Kiswahili kwa kutumia mtandao. Je, walipata msukumo kutoka kwa nani? au nini? Matokeo ni kuwa wanafunzi 32 (Asilimia 59.3) wanapata msukumo wa kibinafsi,

wanafunzi 17 (Asilimia 31.5) kutoka kwa wahadhiri na wanafunzi 5 (Asilimia 9.3) kutoka kwa marafiki.

Haya ni tofauti na maoni ya Oduor (2010) katika utafiti wake wa wanafunzi ambapo alipata kuwa, wanafunzi hawakupata motisha kutoka kwa wahadhiri wao. Hivyo, ikawa vigumu wao kuutumia mtandao, itakuwa muhimu ikiwa wanafunzi watahimizwa na kuelekezwa na wahadhiri katika matumizi zaidi ya rasilimali za mtandao.

Wanafunzi wengi wa masomo ya Kiswahili hutumia mtandao kwa maoni yao. Hawaambiwi na mtu wautumie mtandao bali ni juhudi za kibinafsi za kutaka kupata habari kutoka kwenye mtandao. Ni dhahiri shahiri kuwa wahadhiri wana mchango pia katika kuwaelekeza wanafunzi kutumia mtandao kufanya utafiti. Hii inaamanisha kuwa baadhi ya wahadhiri wanawahimiza wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno kuzitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademi kufanya utafiti.

**Jedwali 12: Mahali wanafunzi wa Kiswahili wanapata huduma na rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia**

| **Mahali** | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Maktaba | 4 | 7.4 |
| Mikahawa ya mitandao | 30 | 55.6 |
| Tarakilishi za kibinafsi | 20 | 37.0 |
| Jumla | 54 | 100 |

Data hii ilipatikana katika swali la kumi ambapo mtafiti alitaka kujua ikiwa wanafunzi walipata huduma za mtandao chuoni wanakosomea au nje ya chuo au kupitia tarakilishi za kibinafsi. Swala hili lilinuia kupata habari kuhusu mahali wanafunzi wa Kiswahili wanapata huduma au rasilimali za Kiswahili. Matokeo ni kuwa wanafunzi ishirini (Asilimia 37.0) hupata huduma za mtandao kutoka kwa tarakilishi za kibinafsi, wanafunzi 30 (Asilimia 55.6) kutoka mikahawa ya mitandao na wanafunzi 4 (Asilimia 7.4) kutoka maktabani.

Haya ni sawa na maoni ya Bankole na Babalola (2012) waliopata kuwa, wanafunzi wengi wa Chuo Kikuu cha Olabisi Onabanjo kule Nigeria, walipata kufikia mtandao kupitia mikahawa ya

nje (Asilimia 66.1), maktaba ya chuo (Asilimia 8.5), idarani (Asilimia 6) na maeneo ya Habari na Teknolojia katika chuo (Asilimia 2.6). Haya ni maoni sawa ya Fasae & Aladeniyi (2012) ambao walipata kuwa asilimia 99 waliutumia mtandao kwenye mikahawa ya mitandao na asilimia 19 ambayo ni ya chini walitumia maktaba ya Chuo.

Hii ni tofauti na maoni ya Salaam & Adegbore (2010) walipofanya utafiti wa wanafunzi wa chuo cha kibinafsi kule Ogun, Nigeria ambapo wanafunzi wengi waliutumia mtandao kwenye maktaba ya chuo (Asilimia 59.2) Maeneo ya TE(KNO)HAMA chuoni (Asilimia 35.4) na ofisi za wahadhiri (Asilimia 5.3). Hii inamaanisha kuwa chuo cha kinfsi cha Ogun kinawapa wanafunzi wake huduma za mtandao kwa wingi. Nchini Kenya wanafunzi wengi wa Chuo Kikuu cha Nairobi waliutumia mtandao kwenye mikahawa ya nje asilimia 97.7 (Waithaka, 2013). Baadhi ya wanafunzi wa Kiswahili wana tarakilishi za kibinafsi. Wao wanazitumia tarakilishi hizi kupata habari za kufanya utafiti wa Kiswahili. Wanafunzi wengine hupata huduma hizi kutoka kwa mikahawa ya mitandao nje na ndani ya chuo. Hivyo, mikahawa ya mtandao huwawezesha wanafunzi wa Kiswahili kupata huduma na rasilimali za mtandao. Maktaba ina mchango mdogo katika kuwapa wanafunzi wa Kiswahili nafasi ya kuzifikia huduma na rasilimali za Kiswahili.

Maktaba za Chuo Kikuucha Maseno hazitumiwi na wengi wa wanafunzi wa Kiswahili kuzifikia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia. Hivyo, Chuo Kikuu cha Maseno kinapaswa kuajibika katika kuhakikisha maktaba zote zina tarakilishi zilizounganishwa kwenye mtandao na wanafunzi wa Kiswahili wanaweza kuzifikia kwa urahisi. Miundo msingi ya kutosha iendelezwe katika chuo hiki ili kurahisisha upatikanaji wa huduma na rasilimali za mtandao wa kiakademia katika maktaba.

**Jedwali 13: Rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia zinazotumiwa zaidi na wanafunzi wa Kiswahili**

| Rasilimali | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| Majarida | 34 | 62.9 |
| Magazeti | 8 | 14.8 |
| Kamusi | 6 | 11.1 |
| Mitandao ya Kiswahili | 6 | 11.1 |
| Jumla | 54 | 100 |

Data hii ilipatikana katika swali la kumi na moja ambapo mtafiti alitaka kujua rasilimali iliyotumiwa zaidi. Suala hili lilinuia kutambua rasilimali ya Kiswahili inayotumiwa sana na wanafunzi wa Kiswahili. Wanafunzi 6 (Asilimia 11.1) walitumia kamusi katika mtandao, wanafunzi 34 (Asilimia 62.9) walitumia majarida, wanafunzi 8 (Asilimia 14.8) walitumia magazeti na wanafunzi 6 (Asilimia 11.1) walitumia mitandao ya Kiswahili. Llo & Ifijeh (2010) walipofanya utafiti kuhusu athari za matumizi ya mtandao kwa utafiti wa wanafunzi, walipata kuwa rasilimali zilizotumiwa sana na wanafunzi ni kama vile majarida (Asilimia 36.9), vitabu (Asilimia 24.1), makala yaliyoandikwa (Asilimia 9.9), miradi (Asilimia 11.3), magazeti (Asilimia 14.9) na machapisho (Asilimia 2.9). Haya ni sawa na tulivyopata katika utafiti wa wanafunzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Maseno ambao walitumia sana majarida ikilinganishwa na maoni ya Llo & Ifijeh (2010) ambaye alipata walitumia sana majarida. Wanafunzi wa Kiswahili hawakutumia vitabu, kamusi kwa sababu hawazijui na hawajui kuvipata. Fasae & Aladeniyi (2012) wanasema kuwa wengi wa wanafunzi hutumia majarida katika mtandao ikilinganishwa na rasilimali nyingine. Kutokana na utafiti wao, walitambua kuwa asilimia 83 ya wanafunzi waliohojiwa waliyatumia majarida na asilimia 45 ambayo ilikuwa ya chini walivitumia vitabu. Majarida yalitumiwa kwa sababu yalikuwa na habari za kutosha.

Wanafunzi wa Kiswahili hutumia sana rasilimali ya majarida kupata habari za kufanya utafiti. Hii inamaanisha kuwa wao hutumia majarida yanayowawezesha kutosheleza mahitaji yao ya kimasomo. Kamusi katika mtandao hutumiwa na wanafunzi wa Kiswahili ingawa ni wachache mno. Magazeti na mitandao ya Kiswahili ni rasilimali ambazo hazitumiwi sana na wanafunzi wa

Kiswahili katika mtandao. Hivyo, ni muhimu wanafunzi wa Kiswahili kuzitambua na kuzitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia.

**Jedwali 14: Njia zinazotumiwa na wanafunzi wa Kiswahili kudurusu kwenye mtandao wa kiakademia**

| **Njia za kudurusu** | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Injini pekuzi | 49 | 90.7 |
| Kuandika anwani wavuti | 5 | 9.3 |
| Jumla | 54 | 100 |

Swali la kumi na mbili lilihusu njia wanazotumia wanafunzi wa Kiswahili kuzifikia rasilimali za Kiswahili. Wanafunzi 49 (Asilimia 90.7) walitumia injini pekuzi na wanafunzi 5 (Asilimia 9.3) waliandika anwani moja kwa moja. Wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno walitumia sana injini pekuzi kama njia ya kuzifikia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia kama vile majarida, magazeti, kamusi na vitabu. Hata hivyo baadhi yao waliandika anwani ya makala waliyohitaji. Hii inamaanisha kuwa ili kuzipata baadhi ya rasilimali ni muhimu kujua anwani yake. Injini pekuzi hahitaji haswa anwani ya wavuti bali unaweza kuandika swali moja kwa moja na ukapata majibu unayohitaji. Luambano & Nawe (2004) wanakubaliana na haya wanaposema kuwa, wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam walitumia injini pekuzi na kuandika anwani ya wavuti kama njia za kudurusu katika mtandao. Wanafunzi wa Kiswahili wanapaswa kujua anwani za rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia ili kuzipata haraka kwa kutumia injini pekuzi.

**Jedwali 15: Injini pekuzi inayotumiwa zaidi na wanafunzi wa Kiswahili**

| **Injini pekuzi** | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| *Google* | 45 | 83.3 |
| *Yahoo* | 5 | 9.3 |
| Nyingine | 4 | 7.4 |
| Jumla | 54 | 100 |

Swali la kumi na tatu liliulizwa ili kupata data kuhusu injini pekuzi iliyotumiwa zaidi na wanafunzi wa Kiswahili. Hili ni kutokana na hali kuwa huenda wengine walizitumia. Hivyo, waliochagua kuwa walitumia injini pekuzi walipewa nafasi hii kuitaja. Swala hili lilinuia kufahamu injini pekuzi inayotumiwa zaidi na wanafunzi wa Kiswahili. Hii ni kwa sababu ni njia iliyotumiwa na wengi wa wanafunzi wa vyuo vikuu asemavyo Waithaka (2013). Wanafunzi 45 (Asilimia 83.3) walitumia *Google*, wanafunzi 5 (Asilimia 9.3) walitumia *Yahoo* na wanafunzi 4 (Asilimia 7.4) walitumia injini pekuzi nyinginezo.

Injini pekuzi ni programu inayowasaidia watumizi kupata habari kutoka kwa mfumo enezi wa habari. Majukumu ya injini pekuzi ni kama vile, kukubali maswali kutoka kwa vitafutaji, kuchukua kurasa za wavuti zinazofaa kutoka kwa mfumo enezi wa habari, kuonyesha kurasa za mfumo enezi wa habari na kuleta pamoja kurasa za wavuti kutoka kwa mfumo enezi wa habari (Gathoni, 2010). *Google* ni injini pekuzi inayotumiwa sana na wanafunzi wa Kiswahili kupata habari zinazowawezesha kufanya utafiti. *Yahoo* haina mchango mkubwa kwa wanafunzi wa Kiswahili. Wale waliotumia injini pekuzi nyingine walitaja *Opera Mini*. King'ori (2012) anasema kuwa, wanafunzi wa vyuo vikuu nchini Kenya walitumia mtandao kupitia simu ya rununu. *Opera Mini* ni mojawapo wa wavuti durusu katika simu rununu.

Malik & Mahmood (2009) walipofanya utafiti wa tabia za wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Punjab kuhusu matumizi ya wavuti. Maoni yao ni sawa na yale ya wanafunzi wa Kiswahili ambapo walipata kuwa, injini pekuzi iliyotumiwa sana ni *Google* (Asilimia 97) na kufuatiwa na *Yahoo* (Asilimia 72). Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Maseno hawatofautiani na wa Chuo Kikuu cha Punjab kwa sababu wengi wao walitumia injini pekuzi ya *Google*. Tofauti ni kuwa baadhi ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Maseno walitaja kuwa walitumia *Opera mini*.

Haya ni maoni sawa na Edem & Offre (2010) walipofanya utafiti kuhusu matumizi ya mtandao miongoni mwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Calabar. Walipata kuwa, wanafunzi walitumia sana injini pekuzi ya *Google* (Asilimia 78.9), *Yahoo* (Asilimia 26.7) na *Alta vista* (Asilimia 19.8). Hivyo kwa jumla ni kuwa wengi wa wanafunzi wa vyuo vikuu hutumia sana injini pekuzi ya *Google* kutafuta habari. Wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno waliohojiwa walitoa sababu zilizowafanya wao kutumia injini pekuzi ya *Google*. Nazo ni kuwa, hutoa majibu kwa haraka (Asilimia 60), hutoa maelezo kwa kina (Asilimia 13), ni rahisi kutumiwa (Asilimia

13), majibu ni sahihi (Asilimia 3) mazoea (Asilimia 3) na kuna ambao hawakujibu (Asilimia 11). Hivyo, injini pekuzi ya *Alta Vista* inaweza kutumiwa na wanafunzi wa Kiswahili ili kuzifikia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia.

Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Calabar kule Nigeria walitumia injini pekuzi ya *Google* kwa sababu, ni wazi, rahisi kutumia, hutoa majibu, haihitaji ujuzi maalum, na pia hurekebisha sarufi (Edem & Offre, 2010). Wanafunzi wa shahada ya kwanza wa Chuo Kikuu cha Namibia wanaosomea uuguzi hutumia *Google* kwa sababu ya upana wa habari, ni haraka na habari huwa kila mara za kisasa asemavvyo Ndinoshiho (2010). Hivyo ni wazi kuwa injini pekuzi ya *Google* hutumiwa sana na wanafunzi wa vyuo vikuu kwa sababu ni rahisi kuitumia, ina majibu na majibu haya hutolewa kwa haraka. Wanafunzi wa Kiswahili watafaidika pakubwa ikiwa watatumia injini pekuzi kadhaa kuzitambua rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia.

**Jedwali 16: Sababu za wanafunzi wa Kiswahili kutumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia**

| **Sababu** | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Huokoa wakati | 20 | 37.0 |
| Rahisi kutumia | 14 | 25.9 |
| Zina habari nyingi | 45 | 83.3 |
| Si ghali | 19 | 35.2 |
| Ni muhimu kuzitumia kufanya utafiti | 28 | 51.9 |

Swali la kumi na tano liliulizwa ili kuelezaa sababu za wanafunzi wa Kiswahili kutumia rasilimali za Kiswahili za mtandao. Swala hili lilinuia kujua sababu zilizowapelekea wanafunzi wa Kiswahili kuamua kuzitumia rasilimali za Kiswahiliza mtandao wa kiakademia. Majibu zaidi ya moja yalitolewa na wahojiwa. Wanafunzi wa Kiswahili 20 (Asilimia 37.0) wanazitumia rasilimali katika mtandao kuokoa wakati, wanafunzi 14 (Asilimia 25.9) walizitumia kwani ilikuwa rahisi kuzitumia, wanafunzi 45 (Asilimia 83.3) walizitumia kwa sababu zilikuwa na habari nyingi wanafunzi 19 (Asilimia 35.2) walizitumia kwa sababu si ghali na wanafunzi 28 (Asilimia 51.9) walisema ilikuwa muhimu kuzitumia kufanya utafiti katika Kiswahili.

Wengi wa wanafunzi wa Kiswahili hutumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia kwa sababu rasilimali hizi zina habari za kutosha zinazotosheleza mahitaji yao. Hii inamaanisha kwamba rasilimali za Kiswahili zimekuwa na mchango mkubwa katika kuwapa wanafunzi habari za kuwawezesha kufanya utafiti wao. Pia baadhi ya wanafunzi waliona ni muhimu kuzitumia rasilimali za Kiswahili kufanya utafiti. Hivyo, ni wazi kuwa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno wametambua mchango wa mtandao katika kuimarisha kozi yao.

Wengi wa watafiti wa Chuo Kikuu cha Guru Gubind Singh Indraprastha kule India waliutumia mtandao kwa sababu muda uliokolewa (asilimia 75), ilikuwa rahisi wao kuutumia (Asilimia 65.4), ulikuwa muhimu wao kuutumia kufanya utafiti (Asilimia 51.9) na waliutumia mtandao kwa sababu ilikuwa na habari nyingi ( Sharma, 2009). Haya yote yana mashiko ya ni kwa nini wanafunzi wa vyuo vikuu waliutumia mtandao. Muhimu ni kwa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno kuendelea kuutumia mtandao kwa sababu una manufaa makubwa kwa utafiti wao.

### 4.3.3 Umuhimu wa matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia kwa utafiti wa Kiswahili

Matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia yana umuhimu kwa utafiti wa Kiswahili. Utafiti ni sehemu kubwa ya maisha ya mwanafunzi yeyote hasa wa kiwango cha juu cha elimu yaani chuo kikuu. Hivyo, ikiwa wanafunzi wana ufahamu na wanazitumia rasilimali za Kiswahili basi wanafaa kuzitumia kufanya utafiti. Rasilimali za Kiswahili zina umuhimu kwa utafiti wa Kiswahili, hivyo wanafunzi wa Kiswahili wanapata utoshelezi katika utafiti wao. Mhimili wa utoshelezi wa chombo cha habari katika nadharia ya Mawasiliano inayorejelea matumizi na utoshelezi ulisaidia katika kueleza umuhimu wa matumizi ya rasilimali za mtandao wa kiakademia za Kiswahili na wanafunzi wa Kiswahili kwa utafiti wa Kiswahili. Matokeo yake yaliwasilishwa ifuatavyo;

**Jedwali 17: Umuhimu wa matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia kwa utafiti wa Kiswahili**

| **Athari** | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Ubora utafiti | 48 | 88.9 |
| Kurahisisha utafiti | 32 | 59.3 |
| Kasi ya kuandika utafiti | 21 | 38.9 |
| Usasa wa maandishi | 16 | 29.6 |

Matumizi ya rasilimali za Kiswahili yamekuwa na umuhimu kwa utafiti wa Kiswahili. Hivyo, swali la kumi na sita lilieleza umuhimu wa matumizi ya rasilimali za mtandao kwa utafiti wa Kiswahili. Wanafunzi 48 (Asilimia 88.9) walisema rasilimali hizi zilifanya utafiti au kazi ya Kiswahili kuwa bora zaidi, Wanafunzi 32 (Asilimia 59.3) walisema utafiti ulirahisishwa na wanafunzi 21 (Asilimia 38.9) walisema rasilimali za Kiswahili katika mtandao ziliwafanya wao kuandika ripoti au miradi kwa haraka. Mwisho, rasilimali za Kiswahili katika mtandao ziliwezesha utafiti kuwa na makala au maadishi halisi. Haya ni madai ya wanafunzi 16 (Asilimia 29.6).

Wengi wa wanafunzi wa Kiswahili walisema kuwa matumizi ya rasilimali za Kiswahili yaliathiri utafiti wa Kiswahili hasa kwa kuhakikisha kuwa kazi za Kiswahili zilikuwa bora. Ubora wa utafiti ulitokana na habari za kisasa walizopata kutoka kwa Mtandao kutoka kwa wataalamu mbalimbali. Habari katika rasilimali hizi za Kiswahili ziliwawezesha wanafunzi kuandika tafiti zilizokuzwa za kisasa. Pia wanafunzi wa Kiswahili waliweza kurahisishiwa utafiti kupitia rasilimali hizi. Walipata habari za kutosha ambapo utafiti wao ulirahisishwa na kuwa komavu. Hili lilipelekea baadhi yao kuweza kuandika utafiti wao kwa haraka kwa sababu ya kuwa na ujuzi wa kutumia mtandao (Luban, 2000). Utafiti huu ulishughulikia umuhimu wa rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia kwa utafiti wa Kiswahili.

Baadhi ya wataalamu kama vile Jones and Madden (2012) Usun (2003), walikubali kuwa mtandao ulitumiwa sana na wanafunzi wa vyuo vikuu kufanya utafiti. Agil & Ahmad (2011) wanakubaliana na maoni haya ingawa walishughulikia wanafunzi wa uzamili na uzamifu na wakapata kuwa walizitumia rasilimali za mtandao kufanya utafiti. Baadhi ya watafiti waliopata maoni sawa ya wanafunzi kufaidika kiutafiti walipotumia rasilimali za mtandao ni kama vile

Fasae & Aladeniyi (2012) na LlO & Ifijeh (2010) ambapo utafiti ulikuwa bora, waliandika utafiti kwa kasi, walipata habari za kisasa, ongezeko la habari na urahisi wa kuandika utafiti. Wanafunzi wa vyuo vikuu walitumia rasilimali za mtandao kufanya kazi ya ziada, kuwasiliana na wenzao au wahadhiri, kukuza usomaji, kuwa na matokeo mazuri katika mitihani yao na kubadilishana maoni na wanafunzi wengine. Ikiwa wanafunzi wa Kiswahili walizitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia kufanya utafiti basi kulikuwa na haja kujua utoshelezi wao na matokeo yalikuwa kama ifuatavyo;

**Jedwali 18: Utoshelezi wa matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia**

| **Utoshelezi** | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Ndiyo | 42 | 77.8 |
| La | 10 | 18.5 |
| Sifahamu | 2 | 3.7 |
| Jumla | 54 | 100 |

Majibu yalitolewa zaidi ya moja na wahojiwa**.** Swali la kumi na saba lilihusu utoshelezi wanaopata wanafunzi wa Kiswahili wanapotumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia. Matokeo ni kuwa, wanafunzi 42 (Asilimia 77.8) walitosheka, wanafunzi 10 (Asilimia 18.5) hawakutosheka na wanafunzi 2 (Asilimia 3.7) hawakufahamu. Wengi wa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno walikuwa na utoshelezi walipotumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia. Idadi ndogo ya wanafunzi hawakufahamu utoshelezi wao kwani huenda hawakuzitumia sana rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia. Sababu za wanafunzi wa Kiswahili kutosheka na rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia ni kuwa, utafiti wao ulirahisishwa, walipata habari za kutosha, masomo yao yaliimarika, walipata habari kwa urahisi na walikuwa hadhira tendi hasa walipokuwa wakizitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia.

Haya ni sawa na maoni ya Parameshwar & Patil (2000) ambao walifanya utafiti wa watafiti wa Chuo Kikuu cha Gulbarga na kutambua kuwa, watafiti walitosheka na ralisimali zilizokuwepo hasa katika kuimarisha utafiti wao. Asilimia 44.9 walitosheka kabisa, asilimia 28.5 walitosheka kidogo, asilimia 14.5 walitosheka kidogo sana na asilimia 14.9 hakufahamu utoshelezi wao.

Watafiti wengi walitosheka na rasilimali za mtandao ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi wawaliofanya kozi ya Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno. Hivyo, watafiti wanafunzi wa Kiswahili wanapaswa kutosheleza mahitaji yao ya kiutafiti kwa hali ya kuridhisha na hili litawezekana ikiwa rasilimali za Kiswahili zitaongezeka katika Mtandao.

Utafiti wa wanafunzi wa shahada ya kwanza wa Chuo Kikuu cha Bostwana asemavyo, Tella (2007) ulionyesha kuwa, rasilimali za mtandao ziliwawezesha wanafunzi kupata habari, kuwasiliana na wenzao ili kuimarisha masomo yao. Haya ni sawa na maoni ya Adegboji & Toyo (2006) wanasema kwamba mtandao hurahisisha utafiti wa wanafunzi kwa kupata habari. Hivyo, maoni haya yote yanakubaliana na ya utafiti huu kuwa wanafunzi wanatosheka na matumizi ya rasilimali za Kiswahili katika utafiti wao kwa sababu walipata habari za kutosha.

Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Nairobi walikuwa na utoshelezi wa wastani katika kuutumia mtandao kama ilivyo wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno. Waithaka (2013) aligawa utoshelezi kwa viwango vya asilimia ambapo wanafunzi 48 (Asilimia 18.2) walitosheka chini ya asilimia kumi, wanafunzi 122 (Asilimia 46.2) walitosheka asilimia 11-50 na wanafunzi 94 (Asilimia 35.6) walitosheka zaidi asilimia 50. Hivyo wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno wanatarajiwa kuzitambua rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia ili kujitosheleza vilivyo.

### 4.3.4 Changamoto zinazowakumba wanafunzi wa Kiswahili walipotumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia

Wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno walipozitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia, walikumbwa na changamoto zifuatazo;

**Jedwali 19: Changamoto zinazowakumba wanafunzi wa Kiswahili walipotumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia**

| Tatizo | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| Habari chache | 20 | 37.0 |
| Majibu kwa lugha ya Kiingereza | 38 | 70.0 |
| Kutopata majibu | 14 | 25.9 |
| Kutohusiana kwa majibu na swali lililoulizwa | 24 | 44.4 |
| Majibu yasiyo kamili | 10 | 18.5 |
| Uchache wa rasilimali za Kiswahili | 35 | 64.8 |
| Habari zenye dosari | 18 | 33.3 |
| Baadhi ya kazi hazipatikani | 12 | 22.2 |
| Maelezo yanayotofautiana baina wa wataalamu | 16 | 29.6 |

Swali la kumi na nne liliulizwa kwa nia ya kujua matatizo yanayowakumba wanafunzi wa Kiswahili wanapotumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia kufanya utafiti wa Kiswahili. Matumizi ya rasilimali za Kiswahili na wanafunzi wa Kiswahili yamekuwa na manufaa. Hata hivyo, wao walikumbana na matatizo kadha walipokuwa wakizitumia rasilimali hizi za Kiswahili. Baadhi ya matatizo waliyokumbana nayo ni kama vile; Wanafunzi 20 (Asilimia 37.0) walidai kuwepo kwa habari chache, wanafunzi 38 (Asilimia 70.0) walisema kuwa majibu yalitoka kwa lugha ya Kiingereza, wanafunzi 14 (Asilimia 25.9) wakasema kwamba wakati mwingine hawakupata majibu wanayotarajia, wanafunzi 24 (Asilimia 44.4) waliona kuwa majibu hayakuhusiana na swali lililoulizwa, wanafunzi 10 (Asilimia 18.5) walipata majibu yasiyo kamili, wanafunzi 35 (Asilimia 64.8) walidai kuna uchache wa rasilimali za Kiswahili, wanafunzi 18 (Asilimia 33.3) walisema kuwa maelezo ya habari yalikuwa na dosari, wanafunzi 12 (Asilimia 22.2) baadhi ya kazi hazipatikani na wanafunzi 16 (Asilimia 29.6) walisema kuwa kulikuwa na maelezo yanayotofautiana baina ya wataalamu.

Haya ni maoni tofauti na yale ya Okinda (2007) alipofanya utafiti kuhusu matumizi na utoshelezi wa mtandao miongoni mwa wanafunzi wa vyuo nchini Kenya. Alitambua kuwa baadhi ya matatizo waliyokuwa nayo ni; hawakufahamu rasilimali zozote za kielimu, hawakupata himizo kutoka kwa wahadhiri na hawakujua kutumia mtandao.  Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Punjab walikumbwa na matatizo haya; kujikokota kwa mtandao, habari nyingi kupita kiasi, habari zisizostahili na habari zisizo bora. Hivyo, ingawa mtandao uliwafaidi wanafunzi wa vyuo vikuu katika kupata habari nyingi, matatizo haya yaliwakumba. Hawajafa moyo, kwani wameibua mbinu za kukabiliana na matatizo haya. Tofauti katika tafiti hizi ni kuwa wengi wa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno walitatizika na yaliyomo katika mtandao ikilinganishwa na wale wa chuo cha Punjab. Ni wazi kuwa data nyingi katika mtandao zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza hivyo imewawia vigumu wanafunzi wa Kiswahili kupata data iliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Ingawa wanafunzi wa Punjab wana matatizo ya yaliyomo katika mtandao wametaja pia suala la kujikokota kwa mtandao lakini wanafunzi wa Kiswahili hawakutaja tatizo hili.

Mbinu wanazotumia kuhakikisha kuwa matatizo haya yanapungua ni; hawazitegemei tu habari za mtandao bali wanazilinganisha na zile za vitabu maktabani, wanaelewa mada ya utafiti kabla ya kutafuta habari, wanaelewa injini pekuzi zinazojulikana na kufaa kutumiwa kupata habari, walitumia injini pekuzi zaidi ya moja na walirekodi maeneo waliyotumia kupata habari kwa sababu ya marejeleo ya baadaye. Hili litafanya utafiti wa Kiswahili kukuzwa zaidi.

Tofauti nyingine ni kuwa Bankole & Babalola (2012) wanataja baadhi ya matatizo yaliyowakumba wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Olabisi Onabanjo ni kama vile seva kujiunga kwenye mitandao polepole, uhaba wa huduma za mtandao katika chuo, uhaba wa umeme na gharama ya juu ya matumizi ya mtandao. Fasae & Aladeniyi (2012) wanakubaliana kwa kiasi na Bankole na Babalola (2012) kuwa, baadhi ya matatizo yaliyowakumba wanafunzi wa vyuo viwili vya Nigeria ni, kuchelewa kwa uunganishaji wa mtandao (Asilimia 74), gharama ya juu ya mtandao (Asilimia 64), ugumu wa kupata habari katika mtandao (Asilimia 62) na uhaba wa umeme (Asilimia 82). Utendi wa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno ulilenga kutosheleza mahitaji yao ya kiakademia. Hata hivyo, katika harakati za kutosheleza mahitaji haya walikumbana na channgamoto ambazo zikitatuliwa, wanafunzi wa Kiswahili watatoshelezwa vilivyo kwani watazitumia rasilimali za Kiswahili vyema.

### 4.4 Ufaafu wa rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia zinazotumiwa na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno

Wanafunzi walitoa mifano ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia ambapo walitaja majarida, magazeti, idhaa za redio, kamusi na mitandao ya Kiswahili. Wanafunzi wa Kiswahili waliweza kusema kuwa rasilimali za Kiswahili ziliwafaa kwa sababu walipata habari halisi zilizotosheleza mahitaji yao ya kielimu. Kuna wale wanafunzi waliopinga wakisema kuwa baadhi yazo hazikufaa. Baada ya mtafiti kuelewa maoni hayo aliona umuhimu wa kudhibitisha ufaafu wa rasilimali za Kiswahili kwa kuzingatia maoni ya wataalamu kama vile; Sahin, Batta & Ercan (2010), Harris (2010), Lee et al (2012). Hivyo vigezo vilivyotumiwa na mtafiti kueleza ufaafu wa rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia ni;

Rasilimali yenye waandishi walio na tajriba ya zaidi ya miaka mitano katika uandishi wa makala ya Kiswahili, taasisi iliyosimamia makala ya waandishi iwe inayojulikana, maandishi katika rasilimali hiyo yawe na marejeleo, maandishi yawe bora na yenye uhalisia, maandishi yawe na uhusiano na taaluma ya Kiswahili ili kutosheleza mahitaji ya kiakademia ya wanafunzi wa Kiswahili na rasilimali hizo ziweze kufikiwa kwa haraka ili wanafunzi wa Kiswahili wafanye utafiti wao kwa haraka. Pia rasilimali hiyo iwe na tovuti ya kuifikia. Hivyo, vigezo hivi vilisaidia kueleza kuwa rasilimali za Kiswahili zinazotumiwa na wanafunzi wa Kiswahili zinafaa. Maoni ya wanafunzi kuhusu ufaafu wa rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia yalijadiliwa ifuatavyo;

**Jedwali 20 Ufaafu wa rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia zilizotumiwa na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno**

| | **Idadi ya wanafunzi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Ndiyo | 40 | 74.1 |
| La | 8 | 14.8 |
| Hawakujibu | 6 | 11.1 |
| **Jumla** | 54 | 100 |

Wengi wa wanafunzi waliohojiwa yaani asilimia 74.1 walisema kuwa rasilimali za Kiswahili katika mtandao zinafaa ikilinganishwa na asilimia 14.8 waliopinga. Wanafunzi waliounga

mkono walitoa sababu zao kwa kusema kuwa nyingi ya rasilimali za Kiswahili katika mtandao ziliandikwa na wataalamu waliobobea katika taaluma zao mbalimbali. Baadhi walitoa mfano wa Said A. Mohammed ambaye amechangia pakubwa katika makala ya fasihi. Pia makala ni halisi na wanaweza kupata habari za kutosha zilizokuzwa vilivyo. Waliopinga ufaafu wa rasilimali za Kiswahili nao walisema kuwa baadhi ya rasilimali zilikuwa na mawazo yaliyopingana na yaliyo vitabuni lakini hawakutoa mfano. Kwa maoni yao, baadhi ya rasilimali za Kiswahili hazikufaa kwa sababu hazikuwa na mhariri au wahariri wa makala yaliyotolewa. Hili limefanya kuwepo kwa misamiati mingi katika lugha ya Kiswahili ambayo haijasanifishwa. Hata hivyo, walikubali kuwa rasilimali za Kiswahili katika mtandao zinapaswa kuhaririwa ili kuwe na usawa wa matumizi ya misamiati iliyosanifishwa.

### 4.4.1 Majarida

Rasilimali za Kiswahili kama tulivyotaja hapo awali ni kama vile, majarida, magazeti, idhaa za redio, kamusi na mitandao ya Kiswahili. Kwa kuzingatia vipengele vilivyotajwa hapo juu kuhusiana na ubora wa rasilimali za mtandao, tutaona ikiwa rasilimali za Kiswahili katika mtandao zinafaa kutumiwa na wanafunzi wa Kiswahili. Kuna majarida kadhaa yaliyo na makala mbalimbali ya Kiswahili aidha katika lugha ya Kiswahili au Kiingereza.

*Swahili Forum* ni mojawapo wa jarida la Kiswahili ambalo linaweza kutumiwa na wanafunzi wa Kiswahili. Mtafiti alitambua kuwa, jarida hili lilianzishwa mwaka wa 1994. Ubora wake ni kuwa, lina wahariri ambao hupitia kazi mbalimbali kabla hazijachapishwa katika jarida hili. Kazi hukubalika ikiwa zimeandikwa katika lugha tatu, nazo ni; Kiswahili, Kijerumani na Kifaransa. Jarida hili huzingatia uhalisia na kuna maagizo wanayopewa waandishi wa makala tofauti kuhusu namna kazi yao inapaswa kuwa. Mwanzo, mwandishi wa kazi yoyote anapaswa kuwa na ikisiri isiyozidi maneno 250, aandike tawasifu yake, aandike marejeleo kwa kufuata mtindo uliopendekezwa na maendelezo ya herufi yazingatie Kiingereza cha Uingereza kama ni makala ya Kiingereza. Kwa sasa kuna toleo jipya la 19 (2012) ambalo ni la kisasa. Jarida hili huongeza makala mwezi wa Machi kila mwaka. Waandishi wengi wa makala katika jarida hili wana tajriba ya kutosha katika lugha ya Kiswahili hivyo mengi ya makala haya yana uhusiano na taaluma ya Kiswahili kwa kiwango kikubwa. Jarida la *Swahili Forum* ni rahisi kufikiwa kwani

mwanafunzi yeyote anaweza kuandika anwani yake katika injini pekuzi na kupata makala hayo moja kwa moja.

Baadhi ya kazi za Kiswahili zilizomo katika jarida la *Swahili Forum* ni kama ifuatavyo*; Swahili Forum* 14 (2007) 'The Swahili Novelist at the Crossroads: The Dilemma of Identity and Fecundity na Said A. Khamis. *Swahili Forum* 17 (2010) Uhalisia na Uhalisia mazingaombwe mshabaha kati ya Dunia yao na The Tin Drum na Ken Walibora. *Swahili Forum* 18 (2012) Mielekeo ya Wasomi na Viongozi Kuhusu Lugha ya Kiswahili na Sangai Mohochi. *Swahili Forum* 19 (2012) Launi za Kiswahili sanifu na Kiswahili fasaha kwa Tanzania bora na Zanzibar na Ahmad Kipacha.

Kwa kuzingatia mifano iliyotolewa hapo juu, waandishi wa makala haya ni wa elimu ya kiwango cha juu. Kazi zao zinafaa kwa sababu zinapatikana katika jarida linalojulikana hasa na wasomi wengi wa Kiswahili. Hoja katika kazi hizi zina mtiririko unaoeleweka kwa urahisi. Makala haya yamefuata kaida zote za uandishi za kuwa na marejeleo na ikisiri. Kazi mbalimbali zilizomo katika jarida hili zitawafaa wanafunzi wa Kiswahili hasa katika utafiti wao. *Swahili Forum* ni jarida linalofaa kutumiwa na wanafunzi wa Kiswahili ili kukuza utafiti wao na lugha ya Kiswahili kwa jumla.

*Nordic Journal of African Studies* ni jarida lingine ambalo huwa na kazi mbalimbali za Kiswahili. Jarida hili linahusu lugha, fasihi na utamaduni wa waafrika. Kazi zinazohusu Kiswahili zimeandikwa katika lugha ya Kiiingereza au Kiswahili. Ubora wa jarida hili ni kuwa, lina mhariri mkuu ambaye ni Axel Fleisch. Kwa sasa toleo la jarida hili limefikia toleo la 21 nambari 1 (2012). Lina makala kuhusu mambo ya kisasa na makala yaliyoandikwa kwa lugha sanifu. Jarida hili lina maagizo kwa waandishi wa makala mbalimbali ambapo linawapa muundo wa kuandika marejeleo na ikisiri na wengi wa waandishi wana tajriba ya kutosha hasa wale walioandika makala kuhusu lugha ya Kiswahili. Makala mengi yana marejeleo ambayo yanaweza kutumiwa na mwanafunzi wa Kiswahili kwa maelezo zaidi. Mwisho ni jarida linalojulikana na ni rahisi kulifikia kwa kuandika jina hili katika injini pekuzi kisha makala yanajitokeza hivyo itakuwa kazi ya mwanafunzi wa Kiswahili kuchagua makala anayotaka.

Mifano ya makala katika jarida hili yanayoweza kumfaa mwanafunzi wa Kiswahili ni; Toleo la 16 nambari ya 3 (2007); Upekee wa Utenzi wa Swifa ya Nguvumali: Utenzi wa mpito, mseto wa imani za jadi na usasa na Mukuthuria Mwenda. Lugha kama Kitambulisho: Changamoto ya Sheng nchini Kenya na King'ei K. na Kobia J. Uuundaji wa Istilahi za Kiswahili Kileksikografia na Athari zake na Sewangi, S.S. Jarida hili linawafaa wanafunzi wa Kiswahili kwa sababu waandishi ni wa elimu ya juu na wamehitimu katika taaluma wanazoandikia. Hivyo, ikiwa mwanafunzi atatumia rasilimali hii, atafaidika pakubwa kwani atapata maarifa yatakayozidisha ujuzi wake kuhusu lugha ya Kiswahili.

*Journal of Pan African Studies* ni jarida lingine lililo na makala kuhusu lugha ya Kiswahili. Mengi ya makala yameandikwa katika lugha ya Kiingereza. Jarida hili lina wahariri na linasisitiza kuwepo kwa marejeleo katika kazi yoyote ile. Pia linafuata sheria zote zinazopaswa kufuatwa katika uandishi wa kazi yoyote ya kiakedemia. Hutokea mara nne kwa mwaka, Machi, Juni, Septemba na Disemba. Toleo la sasa ni toleo la 5 nambari 10 (2013). Jarida hili pia linajulikana na makala yanazingatia usanifu wa lugha.

Mifano ya makala niliyopitia ya baadhi ya waandishi wa Kiswahili katika toleo la 2 nambari 8 (2009) ni kama vile; *The Role of Kiswahili in the Intergration of East Africa* na John Habwe, *Islam and Development of Kiswahili* na Mwenda Mukuthuria, *The Pragmatics of Kiswahili Literacy Political Discourse* na Indede Florence, *The Effect of Sheng in the Teaching of Kiswahili in Kenyan Schools* na Momanyi Clara na *The role Kiswahili in Enhancing the Potential of Science and Technology* na Isaac Ipara na Bob Mbori. Hawa ni baadhi ya wataalamu wa Kiswahili walio na ujuzi wa hali ya juu. Wao ni wasomi wa Kiswahili na wameandika makala mbalimbali na kuhudhuria makongamano kuhusu lugha ya Kiswahili. Hivyo jarida hili litawafaa wanafunzi wa Kiswahli ikiwa watarejelea baadhi ya makala haya kufanya tafiti zao.

*African Journal Online* ni jarida linguine linalofaa kutumiwa na wanafunzi wa Kiswahili kwa sababu lina makala yanayohusu lugha ya Kiswahili na waandishi wana tajriba ya kutosha. Makala haya yana marejeleo na lugha iliyotumiwa na waandishi hawa ni sanifu. Baadhi ya makala ni kama vile; Nafasi ya lugha za Asili katika Shirikisho la Afrika Mashariki na Msanjila Y.P. Mkanganyo wa Dhana za mzizi, Kiini na Shina katika Mofolojia ya Kiswahili na

Gambarange J.J. Athari na Dhima ya Vijenzi Nomino katika Vitenzi vya Kiswahili na Malangwa P.

### 4.4.2 Magazeti

Magazeti kama vile, Swahili News, Taifa Kenya, Habari Newsletter, Majira, Alasiri, Nipashe na Raia Mwema ni rasilimali zilizo katika mtandao. Rasilimali hizi zinafaa mwanafunzi wa Kiswahili kwa sababu mambo mengi yanayozingatiwa ni ya uhalisia. Kiswahili hukuzwa kupitia magazeti ambapo mijadala mbalimbali huandikwa ambayo huweza kuwafaa sana wanafunzi wa Kiswahili. Baadhi ya makala katika magazeti yanaweza kutumiwa na wanafunzi wa Kiswahili kuendeleza taaluma zao.

### 4.4.3 Idhaa za redio

Idhaa za redio/runinga kama vile Sauti ya Marekani, Redio Ujerumani, Redio Uingereza, Idhaa ya Kiswahili KBC, Citizen, K24, KTN, Nation na kadhalika ni rasilimali zilizo bora kwa sababu huzungumzia mambo ya kisasa. Vipindi huundwa ili kusaidia kukuza Kiswahili. Wataalamu mbalimbali wa Kiswahili hualikwa ili kuzungumzia maswala katika lugha, fasihi na utamaduni. Idhaa ya redio ya BBC ina makala kama vile, lahaja za Kiswahili, Sheng inanajisi Kiswahili, Kiswahili na Kiarabu zinaoana na mengi zaidi. Haya ni muhimu kwa mwanafunzi wa Kiswahili kwa sababu atapata ujuzi na maarifa zaidi.

### 4.4.4 Kamusi

Kamusi ni rasilimali zingine katika mtandao ambazo ni muhimu kwa wanafunzi wa Kiswahili. Maandishi mengi kuhusu lugha ya Kiswahili yameandikwa katika lugha ya Kiingereza. Hivyo, itakuwa muhimu ikiwa mwanafunzi wa Kiswahili atatumia rasilimali hii kufafanua, kuelewa au kutafsiri maana mbalimbali za maneno. Kuna kamusi mbalimbali zinazoweza kutumiwa na wanafunzi wa Kiswahili nazo ni kama vile; Kamusi ya Kiswahili- Kiingereza, Kiingereza-Kiswahili, *Kamusi Project* na Wikipedia. Kamusi hizi zinafaa kutumiwa na wanafunzi wa Kiswahili kwa sababu waandalizi ni wataalamu wa lugha ya Kiswahili na wa kiteknolojia.

Wadhamini wa kamusi hizi ni taasisi zinazojulikana. Kwa mfano kuna baadhi ya vyuo vikuu vya kimataifa vinavyofadhili miradi hii ya kuwepo kwa kamusi katika Mtandao. Kwa mfano, Chuo Kikuu cha Yale kinafadhili mradi wa *Kamusi Project* na kamusi ya Kiswahili-Kiingereza. Ingawa maneno yote ya Kiswahili hayajaingizwa katika kamusi hizi, angalau kuna kiwango fulani cha maneno na maana yake yanayoweza kumfaidi mwanafunzi wa Kiswahili.

Kamusi ya Wikipedia elezi huru ni mtandao wavuti ambao hujumuisha makala ambazo hupatikana katika lugha mbalimbali Kiswahili kikiwemo. Wikipedia Kiswahili ina maandishi yanayohusu lugha ya Kiswahili kwa upana mno. Maelezo haya aidha yako katika lugha ya Kiswahili au Kiingereza. Ni bora kwa wanafunzi wa Kiswahili kwa sababu haimzuii yeyote kupata habari. Ni rahisi kupata data na nzuri kwa elimu ya jumla. Habari zilizomo ni wazi na rahisi kuelewa. Pia maandishi haya yana marejeleo na mitandao inayopatikana (Goess, 2008). Kuna makala zaidi ya 15,000 yaliyotafsiriwa na waandishi kuhusu uchumi, biashara, michezo, elimu na historia za watu. Udhaifu wake ni kuwa mtu yeyote anaruhusiwa kuhariri makala zinazowekwa katika wavuti huu.

Sifa hizi ni ishara ya ubora wake. Hivyo, ni muhimu ikiwa wanafunzi wote wa Kiswahili atatumia kamusi hii ili kurahisisha uelewa wa baadhi ya mambo katika lugha ya Kiswahili. Hata hivyo hakuna kizuri kisichokuwa na ubaya. Kamusi ya Wikipedia elezo huru haina mhariri maalum bali mtu yeyote anaweza kuwa mhariri. Hakuna kizuizi kuhusiana na kiwango cha elimu. Mtu yeyote anaruhusiwa kuweka makala yake katika Kamusi elezo huru ya Wikipedia hivyo wanafunzi wanaweza kupata makala mengi yaliyotafsiriwa katika lugha ya Kiswahili. Goess (2008) anasema kuwa kamusi ya Wikipedia si ya kiakademia kwa hivyo ni muhimu kwa watumiaji wake kuhusisha makala mbalimbali na yale ya kamusi ya Wikipedia ili kupata habari zilizokamilika.

### 4.4.5 Mitandao ya Kiswahili

Mitandao ya Kiswahili inawafaa wanafunzi wa Kiswahili kwa sababu wao wanaweza kupata makala ya halisi baadhi yao yakiwa yametafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili. Ni muhimu kwa wanafunzi wa Kiswahili kutambua kuwa, mitandao ya Kiswahili ina habari nyingi zinazohusu lugha, fasihi na isimu ambazo ni muhimu katika taaluma yao ya Kiswahili. Mengi ya Makala

yameandikwa kwa lugha sanifu ya Kiswahili na waandishi maarufu wa Kiswahili. Mitandao ya Kiswahili ina tovuti zinazoweza kutumiwa kuzifika habari mbalimbali. Ni rahisi kufikiwa kwani mwanafunzi anaandika 'Mitandao ya Kiswahili' kwa injini pekuzi yoyote kisha anapata habari ambazo yeye atateua ni zipi zitamfaa. Makala katika mitandao hii yana marejeleo ya chanzo cha habari.

Ufaafu wa rasilimali yoyote utategemea utoshelezi wa mahitaji ya watumiaji wake. Rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia ziliwafaa wanafunzi wa Kiswahili kwani walifaidika kwa kupata habari zitakazowawezesha kufanya utafiti wao. Hata hivyo, zaidi ya utoshelezi wanafunzi wanapaswa kuzingatia sifa zilizotolewa hapo awali kuhusu rasilimali iliyo bora yaani, uhalisia, waandishi walio na ujuzi, imehaririwa, taasisi inayojulikana na kadhalika.

Wanafunzi wanapaswa kutumia njia na marejeleo mbalimbali ili kuongeza ujuzi, ufahamu na undani wa uchunguzi wanaofanya (SAS, 2004). Hivyo, ni muhimu kwa wanafunzi wa Kiswahili kujaribu kutumia rasilimali tofauti tofauti ili kuzidisha maarifa katika lugha ya Kiswahili. Hili litawasaidia kukomaza utafiti wao ili kuendeleza zaidi kozi ya Kiswahili. Hivyo, tumetambua kuwa rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia zimechaguliwa na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno kwa sababu zinafaa na zinawasaidia kukuza tafiti zao.

## 4.5 Hitimisho

Sura hii imeeleza matokeo ya utafiti kuhusu matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno. Mtafiti ametambua kuwa kuna rasilimali za Kiswahili za mtandao wa Kiakademia na zinafaa kutumiwa na wanafunzi wa Kiswahili. Wanafunzi wa Kiswahili wanazitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na zina umuhimu mkubwa kwa utafiti wao kwani kazi yao imerahisishwa na utafiti wao ni wa kihalisia. Hata hivyo, wanapozitumia rasilimali hizi za mtandao wao hukumbwa na changamoto kama vile baadhi ya data ni chache na zinapatikana katika lugha ya Kiingereza. Rasilimali za Kiswahili zipo katika mtandao na zinawafaa wanafunzi wa Kiswahili wanapofanya utafiti wao. Utendi wa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno umewafanya kuchagua chombo cha habari ambacho ni mtandao wa kiakademia ulio na rasilimali za Kiswahili zilizowatosheleza kwa kuimarisha utafiti wao katika Kiswahili.

## SURA YA TANO

## MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.1 Utangulizi

Sura hii inahusu muhtasari wa yale yaliyojadiliwa katika sehemu zilizotangulia na pia mtafiti alieleza hatima ya utafiti huu kisha mapendekezo kutolewa kuhusu namna ya kuimarisha matumizi zaidi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili.

### 5.2 Muhtasari

#### 5.2.1 Rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia

Rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia zipo na hili limedhihirishwa na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Maseno. Rasilimali hizo ni kama vile; majarida, magazeti, idhaa za redio, kamusi na mitandao ya Kiswahili. Rasilimali hizi zina tovuti ambazo ziliwawezesha wanafunzi wa Kiswahili kuzifikia.

#### 5.2.2 Matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno

Wanafunzi wa Kiswahili wana ufahamu wa baadhi ya rasilimali za Kiswahili na hutumia rasilimali za Kiswahili kufanya utafiti wa Kiswahili. Kuna wanafunzi wanaotumia Kiswahili na wengine Kiingereza wanapotumia rasilimali za Kiswahili katika mtandao. Wengi wa wanafunzi wa Kiswahili hutumia rasilimali za mtandao mara 2-3 kwa wiki. Pia wengi wana tajriba ya miaka kati ya 2-3 katika kuzitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao. Ujuzi wao wa kutumia mtandao ni wa wastani. Wengi walidai kuwa waliupata ujuzi huu kutoka kwa marafiki na kuhudhuria mihadhara iliyotolewa na chuo kuhusu kozi za Habari na Teknolojia. Wanafunzi wa Kiswahili wanazitumia rasilimali za Kiswahili kwa sababu za kibinafsi kwani wahadhiri walikuwa na mchango mdogo katika kuwahimiza kuutumia mtandao kufanya utafiti.

Wanafunzi wa Kiswahili walizitumia rasilimali za Kiswahili katika mikahawa ya mitandao nje na ndani ya chuo. Rasilimali inayotumiwa sana ni majarida ikilinganishwa na kamusi. Njia kuu

iliyotumiwa kuzifikia rasilimali za Kiswahili ni injini pekuzi. Injini pekuzi inayotumiwa sana na wanafunzi wa Kiswahili ni ile ya *Google*. Hii ni kwa sababu injini pekuzi hii huwawezesha kupata habari kwa haraka, ya kina, sahihi na kwa urahisi. *Google* kwa upande mwingine haina makala mengi kuhusu lugha na fasihi ya Kiswahili na habari zake ni nyingi ambapo wakati mwingine wanafunzi wana ugumu wa kuzichambua.

Wanafunzi wa Kiswahili hutumia rasilimali za Kiswahili katika mtandao kwa sababu wao huweza kutosheleza mahitaji yao kwa kupata habari zinazowawezesha kufanya utafiti, muda uliokolewa kwa sababu utafiti wao ulirahisishwa. Hata hivyo, wanafunzi hawa hukumbwa na changamoto walipozitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia kama vile, uchache wa maelezo, majibu katika lugha ya Kiingereza, majibu yasiyostahili na uchache wa rasilimali za Kiswahili. Utoshelezi wa matumizi ya rasilimali za Kiswahili ni wa wastani.

Rasilimali za Kiswahili za mtandao zilikuwa na umuhimu kwa utafiti wa Kiswahili. Mwanzo, kazi au miradi mbalimbali imeboreshwa kwa kupata habari za kutosha za kufanya utafiti. Pili, utafiti umerahisishwa kwa sababu habari zinapatikana kwa urahisi na kwa wingi. Tatu, utafiti uliweza kufanywa haraka kwa sababu habari zipo wakati wowote ule. Wanafunzi wa Kiswahili walinufaika walipotumia rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia kufanya utafiti wa Kiswahili. Mwanzo, walipata habari nyingi na kufanywa hadhira tendi.

### 5.2.3 Ufaafu wa rasilimali za Kiswahili za mtandao zilizotumiwa na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno

Wengi wa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno hutumia mtandao ili kupata data inayowawezesha kufanya utafiti wa Kiswahili. Wengi wa wanafunzi wa Kiswahili waliohojiwa wana ufahamu wa baadhi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia. Rasilimali za Kiswahili za mtandao zipo lakini kwa uchache mno. Mifano ya rasilimali hizi ni kama vile; majarida, magazeti, kamusi, idhaa za redio na mitandao ya Kiswahili. Rasilimali hizi za Kiswahili ni bora kutumiwa na wanafunzi wa Kiswahili kufanya utafiti wao.

Mtandao ni chombo kilicho na rasilimali nyingi zinazomwezesha msomi yeyote kupata habari. Wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno wametuthibitishia haya. Wale ambao hawautumii wanapaswa kuhimizwa kuhusu matumizi yake ili kupata habari zitakazokuza utafiti

na lugha ya Kiswahili kwa pamoja. Rasilimali za Kiswahili katika mtandao ni njia mbadala ya kutumiwa ili kuchukua nafasi ya uchache wa vitabu vya Kiswahili katika maktaba. Hata hivyo, rasilimali zote katika mtandao au maktabani zinapaswa kuzingatiwa na wanafunzi katika tafiti zao ili kukuza kozi zao.

## 5.2 Hitimisho

Teknolojia ni muhimu katika maisha ya sasa kwani imerahisisha kazi ya binadamu katika nyanja mbalimbali kama elimu, kilimo, sayansi na kadhalika. Teknolojia kama rasilimali imetumiwa na watu wengi wakiwemo wanasayansi, wanaakademia na watafiti. Hivyo, imekuwa na umuhimu mkubwa katika sekta mbalimbali za maisha. TE(KNO)HAMA ni mojawapo ya teknolojia ambayo imechangia pakubwa katika kukuza taaluma mbalimbali. TE(KNO)HAMA inatumiwa sana katika sekta ya elimu kwa kupitia utafiti, ujifunzaji na ufundishaji wa maswala mengi. Hivyo, ni rasilimali moja ambayo haipaswi kupuuzwa na mtu yeyote au nchi yoyote ile.

Mtandao umetokana na kuimarika na kukuzwa kwa teknolojia ambapo sasa habari zinasambazwa kwa wepesi na kwa watu wengi kwa wakati mmoja. Hivyo, mtandao umesaidia kupunguza gharama za usafiri zilizotumiwa hapo awali kufikia habari fulani. Kwa mfano ni rahisi sasa kwa wasomi kufanya utafiti au kusoma kupitia mtandao na vilevile wafanyibiashara wamerahisishiwa mambo kwani wanapata soko kwa wakati unaofaa. Hali hii imepelekea mataifa mengi kuhakikisha kuwa mataifa yao yameunganishwa katika mtandao ili kujua kwa haraka kinachoendelea katika mataifa mengine. Vyuo vikuu havijaachwa nyuma kwa kuhakikisha kuwa wao pia wameunganishwa katika mitandao ili kukuza masomo ya wanafunzi wao. Mtandao ni muhimu katika kutoa habari zinazoweza kutumika katika kufanya tafiti mbalimbali. Wanafunzi wa vyuo vikuu wanashauriwa kuutumia mtandao ili waweze kujua mapya katika taaluma wanazosomea.

Rasilimali za mtandao ni za aina nyingi. Ndio maana watumiaji wake wanazichagua. Kila mtumiaji wa mtandao anaweza kupata rasilimali hizi ili aweze kujitosheleza. Kuna rasilimali zinazohusu lugha, kilimo, sayansi, teknolojia, biashara na kadhalika. Hivyo, ni muhimu kwa mtumiaji wa chombo cha habari kujua rasilimali hizi ili aweze kuzitumia na kuweza kutosheleza mahitaji yake. Mtafiti alithibitisha rasilimali katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza na zina

mambo ya Kiswahili ambazo zinatumiwa na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno. Ni wazi kuwa lugha nyingine kama vilie Kifaransa, Kijerumani na Kichina haziwezi kukosa rasilimali zao kwani zimeorodheshwa kama lugha kuu zinazotumiwa katika mtandao. Hivyo, mtumiaji atachagua rasilimali katika mtandao zitakazomwezesha kutosheleza mahitaji yake kama ilivyo wanafunzi wa Kiswahili waliotambua rasilimali za injini pekuzi, vitabu na majarida na kuzitumia kufanya tafiti za Kiswahili.

Matumizi ya rasilimali za mtandao kwa wanafunzi ni jambo la kila siku. Utendi wa wanafunzi wa Kiswahili uliwawezesha kutafuta kwa upana habari za tafiti wanazopaswa kufanya. Marafiki wenzao wana mchango katika kuwaelekeza namna ya kupata habari hizi na wengine wameelekezwa kupitia mafunzo wanayopewa katika kozi mbalimbali za mtandao aidha chuoni au nje ya chuo. Isitoshe wengi wa wanafunzi wameweza kununua tarakilishi za kibinafsi hivyo, wana muda wa kutosha wa kudurusu zaidi katika mtandao ili kupata habari wanazohitaji. Hili limesaidia wengi kutosheleza mahitaji yao kwa urahisi. Wanafunzi wa Kiswahili wanazitumia rasilimali za Kiswahili kwa usaidizi wa wanafunzi wenzao na ari yao ya kutaka kujua mambo mengi kuhusu kozi zao.

Matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia yamekuwa na umuhimu kwa wanafunzi wa Kiswahili. Tafiti zao sasa zinazohusisha mtandao zinahusishwa na uhalisia. Baadhi ya wahadhiri wanawahimiza wanafunzi wa Kiswahili kuutumia mtandao ili kusasanisha tafiti zao. Kadhalika, tafiti hizi zimekuzwa kwani maoni ya watu wengi yameweza kuwekwa pamoja ili kuelezea dhana mbalimbali kwa urahisi. Habari hizi zinapatikana kwa urahisi na wanafunzi wengi wa Kiswahili kwani wameweza kuokoa wakati wao hivyo, wana muda wa kusoma mambo mengine zaidi.

Hata hivyo, rasilimali katika mtandao zimewafanya watumiaji wake kuzembea kusoma vitabu vilivyo katika maktaba. Imekuwa nadra kwa baadhi ya wanafunzi wa Kiswahili kwenda maktabani kusoma kwani habari wanazozitaka zinapatikana kwa urahisi katika mtandao wa kiakademia. Kwa maoni yangu, baadhi ya watumiaji wa mtandao wanaiba kazi za wenzao bila kuwatambulisha katika kazi zao hali ambayo imepelekea kuchipuka kwa tafiti ghushi. Hata hivyo, changamoto hizi ni nadra sana kwani wahalifu hao wanashtakiwa hivyo, kila mtu anajitahidi kufanya kazi yake. Matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na

wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Maseno ni muhimu kwani mahitaji yao ya kiusomi yalitoshelezwa kwani rasilimali zipo na zinafaa.

## 5.4 Mapendekezo na Mapendekezo kuhusu utafiti zaidi

### 5.4.1 Mapendekezo kiujumla

Utafiti huu ulichunguza matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili wa chuo Kikuu cha Maseno. Wanafunzi wanazitumia rasilimali hizi kwa sababu walifaidika pakubwa katika kufanya tafiti zao. Hivyo mapendekezo yafuatayo yametolewa ili kusisitiza matumizi zaidi ya mtandao na wanafunzi wa vyuo vikuu nchini Kenya hasa wa Kiswahili.

Wahadhiri wa Kiswahili wanapaswa kuendelea kuwahimiza na kuwaelekeza wanafunzi wao wa Kiswahili kuhusu namna ya kuzitumia rasilimali za Kiswahili za mtandao ili kuwasaidia kujua habari za ziada katika mtandao na kupanua mawazo yao. Wahadhiri wa Kiswahili wawape wanafunzi wa Kiswahili kazi za ziada zinazohitaji kudurusu habari katika mtandao. Pia wawahimize wanafunzi hawa kuzoea kupata habari za ziada katika mtandao ili ziingiliana na habari wanazopewa na wahadhiri. Wanafunzi wanapaswa kuwa na tarakilishi za kibinafsi ili kukuza zaidi matumizi ya mtandao.

Chuo Kikuu cha Maseno kipange mikakati ya kuwasaidia wanafunzi wake kupata tarakilishi hizi kwa bei nafuu kama ilivyo katika mradi wa Wezesha ambao hutoa kwa bei nafuu. Ni muhimu kwa Chuo Kikuu cha Maseno kuchukua hatua zitakazosisitiza matumizi zaidi ya mtandao miongoni mwa wanafunzi kwa kuandaa programu za mafunzo ili kuimarisha matumizi zaidi ya mtandao. Kozi za Habari na Teknolojia zinazofunzwa kwa wanafunzi wote katika chuo ziambatanishwe na kozi zingine za tarakilishi pamoja na mazoezi zaidi.

### 5.4.2 Mapendekezo kuhusu utafiti zaidi

Utafiti mwingine ufanywe kwa;

1. Kujadili athari za matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao kwa matokeo ya mtihani wa mwisho wa muhula.

2. Kuchanganua rasilimali zaidi za Kiswahili katika mtandao

3. Kutambua mielekeo ya wahadhiri na wasomi wa Kiswahili kuhusiana na rasilimali za Kiswahili za mtandao.

**MAREJELEO**

Adithya, K.H. , Mahadevamurthy, M. & Hydarali, (2003). Awareness and Use of Internet Facilities by students of Vidya Vikas Institute of Management Studies in Mysore city: A Study

Agil, M. & Ahmad, P. (2011). Use of the Internet by Research Scholars and Post Graduate Students of Science Faculty of Aligarh Muslim University, Library Philosophy and Practise, http//un/lib.un/edu4, Retrieved on 26th June, 2013.

Ambeka, A. (2008). Advantages and Disadvantages of the Internet, Buzzle.com.

Ani, O.E. (2010). Internet Access and Use: A Study of Undergraduate students in three Nigerian Universities. *The Electronic Library, 28(4), 555-567.*

Anunobi, C.V. (2006). Dynamics of Internet Usage: A case study of students of the Federal University of Technology Owerri (FUTO) Nigeria. *Educational Research and Reviews*, 1 (6), 192-195

Awoleye, O.M. (2008). Adoption Assessment of Internet Usage amongst Undergraduate Students in Nigeria Universities – A Case Study Approach. http://www. jotml:org/index.php/GT/article/ViewFile/Cas11/44/ Retrieved on 3rd July 2013.

Badu E.E. & Markwei E.D. (2005). Use of Internet and Resources by Academic Staff and Postgraduate Students of University of Ghana: *SAGE Journal Online*, 211(4) 260-268.

Bankole, O.M. & Babalola, S.O. (2012*). Internet Use Among Undergraduate Students of Olabisi Onabanjo University*, Ago Iwoye, Nigeria

Baran, S.J., & Davis, D.K. (2006*).* Mass Communication Theory: Foundation Ferment and Future, Australia, Wardsworth.

Bashir, S., Mahmood, K. & Shafique, F. (2001). Internet Use Among University Students*:* A Survey in University of the Punjab, Lahore

Blumler, J., & Katz, E. (1974). The Uses of Mass Communication, Beverly Hills: CA Sage Publications.

.

Charney, T.R. (1996). *Uses and Gratification of the Internet*. (Masters thesis, MichiganState University, 1996). Masters Abstract International, 35, 0612.

Chigona, S. Kankwenda, G & Manjoo, S.  (2008). Uses and Gratification of Mobile Internet among South African students, *Peer Reviewed Article*, vol. 10, no. 3

Chinwe M.T.N. (2010). The Use of ICT IN Nigeria University: A Case Study of Obafemi Awoloyo University, Ile – Ife, *Library Phylosophy and Practise*.

Cho, V. (2009). Data Quality on the Internet, Hong Kong University, Hong Kong www.irma-international/org/viewtitle/30507

Clavio, G. (2008). *Uses and Gratification of Internet Collegiate Sport Message Board Users*, *http://www. Researchgate.net/…uses-and-gratification… Internet* Retrieved on 20th June 2014.

Crystal, D. (2001). Review of Language and the Internet, Cambridge University Press,*110 Midland Avenue Portcheste*, vol. 7, no. 2, pp 24-27 http://uk.cambridge.org/ Retrieved on 22nd July 2014.

Dave, R. (2012). An Exploratory Study on Measuring Impact of Internet on Students' Academic life of S.P University, *EXCEL International Journal of Multidisciplinary Management Studies, vol 2*, *issue 5,* http://zenithresarch.orrg.in/images/stories/pdf/2012/may/ELJMM/13 Retrieved on 4th July 2013.

David, B.R. (2011). What is Ethics in Research and Why it is Important http://www.niehs.nih.gov/research/resourcesbioethics/whatis/

December, J. (1996*).* Units ofAnalysis for Internet Communication. *Journal of Communication*, 46(1), 14-38.

Defleur, M.L & Ball-Rokeach, S.J. (1988). Theory of Mass Communication, (5th ed.). New York: Longman.

Defleur, M.L., & Denis, E.E. (2002). Understanding Mass Communication*:* A Liberal Arts Persective, Boston: Houghton Mifflin Company.

Ebersole, S. (1999).*Adolescents' use of the World-Wide Web in ten public schools: A uses and gratifications approach*. Unpublished doctoral Dissertation, Regent University. http://faculty.uscolo.edu/ebersole/diss/index.html/ Retrieved on 10th April, 2012.

Ebersole, S. (2000). Uses and Gratification of the Web among students, *Journal of Computer Mediated Communication*, 6(1),

Edem M.B. & Offre E.T. (2010). Reading and Internet Use Activities of Undergraduate students of the Univversity of Calabar, Nigeria, *African Journal of Library Archirves and Information Science*, 20 (1) , 11-18

Farrell, G. (2007*). ICT in Education in Kenya: Survey of ICT and Education in Africa: Kenya country Report,* Ddp-ext.worlbank.org/EdStats/KENpro007.pdf. Retrieved 3rd July, 2013.

Fasae, J.K. & Aladeniyi, F.R. (2012). Internet Use by Students of Faculty of Science in Two Nigerian Universities, *Library Philosophy and Practise* http://un/lib.un/edu/lpp.

Ferguson, D., & Pearse, E. (2000). The World Wide Web as a Functional Alternative to Television, *Journal of Broadcasting and Electronic Media*, 44(2), 155-174.

Foster, S. (2003). Australian Undergraduate Internet Usage: Self- taught, self- directed and self- limiting? *Educationand Information Technologies*, 5(3), 165-175.

Gathoni, N. (2010). *Understanding Search Engines*, Digital Oracle Magazine for Optical Results, July-September, pg 18.

Goess, L. (2008). *The Pros and Cons of using Wikipedia to Research your College papers*, http://www.helium.com/items/909883-the-pros-and-cons Retrieved on 2nd July, 2013.

Gurevitch, M. & Haas, H. (1973). On the Use of Mass Media for Important Things, *American Sociological Review,* 38, 164-181

Harris, R. (2010*). Evaluating Internet Resources,* http//www.virtualsalt.com/evalu8it.htm. Retrieved on 1st July, 2013.

Herzog, H. (1944). *What Do We Really Know About Daytime Serial Listeners?* In Lazarfield P.F. (Ed.) Radio Research 1942-3 (pp. 2-23). London: Sage.

Internet World Stats (2013). Usage and Population Statistics – The Internet World Users by Language. Top ten Languages. http://www.internetworldstats.com/stats7.htm Retrieved on 28th October, 2014.

James, M.L., Wotring, C.E., & Forrest, E.J. (1995). An Exploratory Study of Perceived Benefits of Electronic Bulleting Board, Use and their Impact on other Communication Activities, *Journal of Broadcasting and ElectronicMedia*.

Jere, M.G. & Davis S.V. (2011). An Aplication of Uses and Gratification Theory to compare Consumer Motivation for Magazine and Internet Usage among South African Women Magazine Readers, *South African Business Review*, vol. 15, no. 1

Jones, S. & Madden, M. (2002). *The Internet Goes to College*: How Students are Living in the Future with Todays's Technology, PW Internet & American Life Internet, www.pewinternet.org/.../2002/PL *Retrieved on 1st August 2014*

Johnson, R.B. & Onwuegbuzie, A.J. (2004). Mixed Methods Research: A Research Paradigm Who's Time has Come. *Educational Researcher*, vol. 33, no.7, pp. 14-26.

Katz, E., Guveritch, M., & Haas, H. (1973). On the Use of Mass Media for Important Things. *American Sociological Review*, 38,164-181.

Katz, E., Blumler, J., & Gurevitch, M. (1974). *Uses of Mass Communication by the Individual In Davinson, W.P & Yu, F.T.C (Eds.).* Mass Communication Research: Major issues and Future Directions, pp.11-35 New York: Praeger.

Kaye, B.K. (1998). Uses and Gratification of the World Wide Web: From Couch Potato to Web Potato, *Journal of Communication*, The New Jersey, 6(1) 21-40.

Kenya ICT Strategy (2006). Collaboration and Outsourcing for Economic growth http://www.information .go.ke/docs/Kenya/20 strategy Retrieved on 25th May 2015

Khan, S.A., Khan, A.A. & Bhatti, R. (2011). *Internet Access Use and Gratification Among Undergraduate students: A Case Study of the Islamia University of Bahawalpur, Pakistan,* http://www.iclc.us/cliej/ci32KKB.pdf Retrieved on 30th October, 2014.

Kiai, W. (2013). *Uses and Gratification of the Internet*: A survey study of Mount Kenya and GRETSA Universities in Thika Municipality, uonbi.ac.ke/node/122 Retrieved on 20th June, 2013.

King'ori, M.A. (2012). *Adoption of Internet Among University Students in Kenya,* http://erepository.uonbi.ac.ke:8080/xmlui/handle/123456789/6833 Retrieved on 25th June, 2013.

Kothari, C.R. (2004). Research Methodology: Methods and Techniques, 2nd edition. New Delhi. Wishwa Pakistan.

Kombo, K.D., & Tromp, D.L. (2006). *Proposal and Thesis Writing*: An introduction.Nairobi: Paulines Publication Africa.

Korpela, J. (2014). *English the Universal Language on the Internet*, http://www.cs.tut.fi/korpela/lingua Retrieved on 1st November, 2014.

Lazarfeld, P.F., & Stanton, F. (1944). *Radio Research* 1942-3. NY- Duell, Sloan & Pearce.

Lee Y.W. , Strong A. , Kahn, H. & Wang, R.Y. (2002). *AIMQ: A Methodology for Quality Information Assessment*, Information Management

Leedy, P.D. & Ormorod, J.E. (2005). *Practical Research Planning and Design*, 2nd edition, Upper Saddle river, NJ, Pearson Education.

Lin, C.A (1999). Online Service Adoption Likehood, *Journal of Advertising Research*, 39(2), pp. 79-89.

Llo, P.I. & Ifijeh, G.I. (2010). Impact of the Internet on Final Year Students's Research: A Case Studyof Covenent University, Ota, Nigeria, *Library Philosophy and Practise*.

Luambano, I., & Nawe, J. (2004). Internet Use by Students of Dar es Salaam, *Library High Technology News*, 10.

Lubans, J. (1999). *Key Findings on Internet Use among students* http://www.key-findings-use-among-students.com.html Retrieved on 8th September, 2012.

Luban, J. (2000). *Summary of Graduate Students View points about Effects of the Internet on Student work*, http://www.indians.org/study5a.html Retrieved on 28th June, 2013.

Luo, X. (2002*).* Uses and Gratification Theory and e-consumer behaviors: A Structural Equation Modelling study*, Journal of Interactive Advertising*, 2(2).

Luvaha, J. (2009). *Mshikamano wa Kileksia katika Insha za Kiswahili za Wanafunzi walio na matatizo ya Kusikia katika Shule za Sekondari za Viziwi zilizoteuliwa Nchini Kenya,*Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Maseno.

Malik, A. & Mahmood, K. (2009). *Web Search Behavior of University Students*: A case study University of Punjab. *Webology*, 6(2), 1-14.

Mc Quail, D. (1983). *Mass Communication Theory*. (1st ed.). London: Sage.

Mohochi, S.E. (2011). Mielekeo ya Wasomi wa Kiswahili na Viongozi wa Afrika Mashariki Kuhusu lugha ya Kiswahili, *Swahili Forum* 18 (3) pp.24-36 http://www.qucosa.de/fileadmin/data/qucosa/document/9053/18-03-mohochi.pdf.

Momanyi, C. (2007). *Nafasi ya Lugha ya Kiswahili katika Vyuo Vikuu Nchini Kenya* katika Njogu, K. (2007) Kiswahili na Elimu Nchini Kenya, Kolbe Press, Nairobi.

Mouton, J. (2006). *How to Succed in your Masters and Doctoral Studies*: A South African Guide and Resource Book 10th edition, Pretoria, Van.

Mugenda, O.M & Mugenda, A (1999). Sample Size Determination, http://www.pdfsdocument.com/mugenda Retrieved on 25th July 2015

Muniandy, B. (2010). Academic Use of Internet among Undergraduate Students: A Preliminary Case of Malaysian University. www.researchgate.net/publication

Nazaryan, A. & Gridchin, A. (2006). *The Influence of Internet on Language and 'Email Stress'*, University of Belgorod, Russia.

Ndinoshiho, J.M. (2010). The Use of Electronic Information Services by Undergraduate Nursing students at tha University of Namibia's Northern Campus: *A descriptive study Information Development* 26:57-65.

Nyambongo, C. M. & Ongondo, M. A. (2004). Experiences in the Use of the Internet at Egerton University. Publications.drdo.gov.in/../2047 Retrieved on 25th June 2015

Oduor, P. (2010). *Kenya: How Students Use Technology*, http://www.Ictcradle.com/kenyacurrent/?p=836 Retrieved on 23th june 2011.

Okello-Obura, C. & Magara, E. (2008). Assessment of the Problems that Post Graduate Face in Accessing E - resources in Makerere University, Uganda, *Collection Building* 29 (3): 98-105.

Okinda, T.I. (2007). *Uses and Gratifications of the Internet among Collge Students in Kenya:* A Case Study of Kenya School of Professional Studies, Master of Arts Thesis, University of Nairobi.

Okite- Amughoro, F.A. & Lefose, M.S. (2014). The Use of Electronic Resources to Academic Research by Post Graduate Students atDelta State University, Abraka, Nigeria, South African *Journal of Library & Information Science*

Ongwae, E. (2011). *Maseno UniversityTranslate E- Learning into Reality*, *Daily Nation*, May 30, 2011, pg 30.

Onwuegbuzie, A.J. & Collins, K.M.T. (2007). A Typology of Mixed Sampling Designs in Social Research, *The Qualitative Report* 12(2). http://www.nova.edu/ssss/QR/QR12.2/onwuegbuzie 2. pdf.

Osunade, O. (2003). *An Evaluation of the Impact of the Internet Browsing on Students Academic Performance at Tertiary Level of Education in Nigeria*, http://www.nspb.net/index.php/nspb/article/view/13/10, Retrieved on 27th June, 2013.

Oyieke, L.I. (2008). *Technologies in Teaching and Learning*: A Comparative Evaluation of two Libraries in Kenya, A Dissertation of Master of Information Science Upetd.up.ac.za/thesis/available/etd-092220008153304/unrestricted/disseratation.pdf Retrieved on 22nd June 2013.

Parameshwar, S. & Patil D.B. (2009). Use of Electronic Resources by Faculty members and Research scholars in Gulbarga University: Gulbarga: *A Survey Journal of Information Management* 46 (10), 51-56.

Rodriques, A.J. (2008). *ICT Research Capacity:* Challenges and Strategies in Kenya-Euro-Africa Awareness Workshop October 2008.

Ruggiero, T.E. (2000). *Uses and Gratification Theory in the 21st Centuary. Mass Communication and Society*, 3(1), 3-37. http://www.scribd.com/doc/49768511/Uses-and-Gratification-Theory Retrieved on 28th November, 2011.

Ryan, J. (1995). *Uses and Gratification Study of the Internet Social Interaction Site LambdaMOO*: Talking with 'Dinos' Master Arts Thesis, Ball State University, Muncie, IN.

Sahin, Y.G. et al (2010). The Use of the Internet Resources by University students during Course Projects Elicitation: A case study. *The Turkish Online Journal of Educational Technology*, volume 9, pg. 234.

Salaam, M.O. & Adegbore, M. (2010). Internet Access and Use by Students of Private University in Ogun State, Nigeria, *Library Philosophy and Practice.*

SAS, (2004). *The Research Basis for Curriculum Pathways from SAS in school:* Web based educational Resources for grades 8-14.NC.USA: Institute Inc.

Severin, W.J., & Tankard, J.W. (2001). *Communication Theories*: *Origins, Methods and Uses in the Mass Media*. ( 5th ed.) New York: Longman.

Shabaya, P. (2009). *The Changing Role of Information and Communication Technology (ICTS) For Institutions in Higher Education in Kenya*, Paper submitted to Strathmore ICT 2009 Conference, Nairobi.

Sharma, C. (2009). Use and Impact of E resources at Guru Gubind Sigh Indraprastha university India, A case study, *Electronic Journal of Academic and Special Librainiaship*, vol. 10, no. 1 http://www.sourthernlibraniaship.icaap.org/content/vol10no1/sharma.c.01.html Retrieved on 14th June 2014.

Shibanda,G.G. (2006). *Enhancing E journal Use in Kenyan Universities,* Paper presented at the CODESSRIA ASC Conference on Electronic Publishing and Dissemination 6-8 September, Leiden, The Netherlands.

Strauss, A. & Corbin, J. (1990). *Basics of Qualitative Research; Grounded Theory Procedures & Techniques.* Newbury Park. SAGE Publications.

Stutzer, A. (2010*). InternetUse by University Students*. *http://www.ehow.com/facts-6170385-internet-use-university-students.html*. Retrieved on 8th April, 2012.

Suhail, K. & Bargees, Z. (2006). Effects of Excessive Internet use on Undergraduate Students in Pakistan. *Cyber Psychology and Behavior*. 9, 297-307

Tella, A. (2007). University of Botswana Undergraduate Uses of the Internet*:* Implications On Academic Performance, *Journal of Education Media and Library Sciences* 45:2 161-185.

Usun, S. (2003*).* Undergraduate Students Attitudes towards Educational Uses of Internet. *Interactive Educational Multimedia*, 7, 46 – 62. http://www.ub.edu/multimedia/iem/down/c7/IEM - number 7.pdf

Waithaka, M.W. (2013). *Internet Use Among University Students in Kenya:* A Case Study of University of Nairobi http://uir.unisa.ac.za/bitstream/handle/10500/13284/thesis-waithaka.mw.pdf? Retrieved on 3rd June 2015

Wand, Y. & Wang, R.Y. (1996*).* Anchoring Data Quality Dimension in Ontological Foundations Communication of ACM, Web.mit.edu/…/wandwangCACM…

Waner, W.L. & Henry, W.E. (1948). The Radio Day time Serial: A Symbolic Analysis. Psychological Monographs,37(1). http://en.m.wikibooks.org/wiki/communication theory/ Uses and Gratification. Retireved on 21st June 2015

Zhixian, Y. (2008). *Internet Use Patterns in the United States.* http://www.iclc.us/cliej/c125Yi.htm Retrieved on 30th October, 2011.

**VIAMBATISHO**

a) **Hojaji ya mwanafunzi**

Mimi ni mtafiti wa Chuo Kikuu cha Maseno, utafiti huu unahusu matumizi ya rasilimali za Kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Maseno. Nakuomba ujaze hojaji hii ili nipate data nitakayotumia kuandika tasnifu. Unapaswa kutumia alama (    ) ikiwa ni jibu sahihi na katika maswali mengine nafasi imeachwa ili ujibu kwa kina. Nashukuru kwa muda na mchango wako utakaonisaidia kutimiza lengo la utafiti huu.

1. a.Je, wewe ni wa jinsia ipi?

   Kike    (    )

   Kiume (    )

   b.Je, wewe una ufahamu wa rasilimali za Kiswahili katika mtandao?

   Ndiyo

   La

c. Ikiwa ni ndiyo zitaje rasilimali za Kiswahili katika mtandao?

2.a. Je, wewe unatumia rasilimali za Kiswahili katika mtandao? Eleza.

b. Je, rasilimali za Kiswahili zinafaa

   Ndiyo    (    )

   La    (    )

c. Ikiwa ndiyo toa sababu

d. Ikiwa la toa sababu

3. Je, ni lugha ipi unayotumia unapozitumia rasilimali za Kiswahili katika mtandao?

Kiswahili ( )

Kiingereza ( )

Nyingine ( )

4. Wewe hutumia rasilimali za Kiswahili kwa muda upi?

Kila siku ( )

Mara 2-3 kwa wiki ( )

Mara 2-3 kwa mwezi ( )

Mara moja kwa mwezi ( )

5.Tajriba yako ya kuzitumia rasilimali za Kiswahili za Mtandao ni ipi?

Chini ya mwaka mmoja ( )

Miaka 1-2 ( )

Miaka 2-3 ( )

Zaidi ya miaka 3 ( )

6.Je, ujuzi wako wa kutumia rasilimali za Kiswahili mtandao unaweza kuwa wa asilimia ipi?

0 – 40 ( )

40 – 70 ( )

Zaidi ya 70 ( )

Sifahamu ( )

7. Njia za ujifunzaji wa namna ya kuzitumia rasilimali za Kiswahili za Mtandao?

` Kuhudhuria mihadhara ya habari na teknolojia chuoni ( )

Maktaba ( )

Marafiki ( )

Binafsi ( )

8.Ikiwa ni kozi ya Habari na Teknolojia chuoni Maseno ilikuwa na umuhimu upi kwako kama mwanafunzi wa Kiswahili?

9. Je, ni nini kinachokusukuma kuzitumia rasilimali za Kiswahili katika mtandao?

Binafsi ( )

Wahadhiri ( )

Marafiki ( )

10.Je, huwa unapata wapi huduma za mtandao kufanya tafiti zako za Kiswahili?

Maktaba ( )

Mikahawa ya mtandao (Cybercafés) ( )

Tarakilishi ya kibinafsi ( )

11. (a) Je, ni rasilimali ipi ya Kiswahili unayotumia sana katika mtandao?

Majarida ( )

Vitabu ( )

Magazeti ( )

Kamusi ( )

(b) Eleza sababu za kutumia rasilimali uliyoteua hapo juu.

(c ) Eleza sababu za kutotumia zingine.

12. Njia zipi unazotumia kudurusu katika mtandao?

Injini pekuzi ( )

Kuandika tovuti ( )

Nyingine ( )

13. Je, ni injini pekuzi gani unayotumia sana kufanya tafiti za Kiswahili?

Google ( )

Yahoo ( )

Nyingine(Itaje) ( )

(b) Kwa nini wewe huitumia sana injini pekuzi hiyo?

(c ) Je, injini pekuzi ina dosari gani unapoitumia kufanya utafiti wa Kiswahili?

14. Je, ni matatizo yapi uliyokumbana nayo ulipokuwa ukitumia rasilimali za Kiswahili katika mtandao kufanya utafiti wa Kiswahili?

15. Sababu zipi zinazokufanya kuzitumia rasilimali za Kiswahili?

16. Je, rasilimali za Kiswahili zina umuhimu upi kwa utafiti wa Kiswahili?

17. Je, wewe hutosheka unapotumia rasilimali za Kiswahili katika mtandao kufanya utafiti wa Kiswahili?

Ndiyo ( )

La ( )

Sifahamu ( )

**B. Orodha ya uchunguzi**

Rasilimali za Kiswahili katika mtandao

Majarida

Kamusi

Magazeti

Idhaa za redio

Mitandao ya Kiswahili